# USAWIRI WA WAHUSIKA KATIKA DAFINA YA UMALENGA (H.M MBEGA) NA JICHO LA NDANI (S.A MOHAMED)

**Tasnifu Ya**

**TIMOTHY KINOTI M'NGARUTHI**

**Iliyotolewa kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu Cha Kenyatta**

M'ngaruthi, Timothy
*Usawiri wa wahusika katika Dafina ya*
08/322532



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.

TIMOTHY KINOTI M'NGARUTHI

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu kwa idhini yetu kama wasimamizi.

DKT. EDWIN MASINDE

DKT. SHEILA RYANGA

## TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mke wangu Hellen K. Kinoti kwa kunisaidia kwa hali na mali tangu mwanzo hadi mwisho wa masomo yangu.

## YALIYOMO

Mada ........................................................................ i

Ikirari........................................................................ I

Tabaruku.................................................................... iii

Yaliyomo.................................................................... iv

Shukrani..................................................................... vii

Ikisiri........................................................................ viii

**SURA YA KWANZA**

**UTANGULIZI WA TASNIFU**

1.0 Ufafanuzi wa dhana muhimu.............................................. 1

1.1 Utangulizi............................................................... 3

1.2 Swala la utafiti.......................................................... 5

1.3 Maswali yaliyojibiwa na utafiti........................................... 5

1.4 Malengo ya utafiti......................................................... 5

1.5 Nadharia tete.............................................................. 6

1.6 Sababu za kuchagua mada................................................... 6

1.7 Upeo wa utafiti............................................................ 8

1.8 Udurusu wa maandishi...................................................... 9

1.9 Msingi wa nadharia........................................................ 14

1.10 Mbinu za utafiti.......................................................... 17

a) Ukusanyaji wa data..................................................... 17

b) Uchanganuzi na uwasilishaji wa data..................................... 18

**SURA YA PILI**

**UTEUZI WA WAHUSIKA**

2.0 Utangulizi........................................................21

2.1 Mazingira ya kihistoria........................................22

2.2 Mazingira ya kijiografia.......................................31

2.3 Mazingira ya kijamii...........................................47

2.4 Mazingira ya kisiasa...........................................73

2.5 Mazingira ya kiuchumi.........................................80

2.6 Kiishilio.............................................................91

**SURA YA TATU**

**WAHUSIKA NA UMBUJI KISHAIRI**

3.0 **Utangulizi**........................................................94

3.1 Wahusika binadamu..............................................94

3.2 Wahusika wanyama..............................................101

3.3 Sehemu za mwili.................................................107

3.4 Maumbile na vitu vingine......................................110

3.5 Kiishilio............................................................116

**SURA YA NNE**

**JINSI WASHAIRI WALIVYOWATUMIA WAHUSIKA**

**KUDHIHIRISHA HISIA MBALIMBALI**

4.0 Utangulizi........................................................119

4.1 Mapenzi...........................................................120

4.2 Hasira..............................................................126

4.3 Hofu................................................................130

4.4 Kiishilio............................................................134

**SURA YA TANO**

**MAHITIMISHO**

5.0 Utangulizi……………………………………………………………..136

5.1 Muhtasari……………………………………………………………....136

5.2 Matokeo ya utafiti………………………………………………………138

5.3 Mafanikio na changamoto ……………………………………..……....146

5.4 Mapendekezo……………………………………………………………146

**MAREJELEO**………………………………………………………………148

**SHUKRANI**

Ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu katika utafiti huu, Dkt. Edwin Masinde na Dkt. Sheila Ryanga kwa kunishauri na kunivumilia nilipojikaza kuogelea katika bahari hii, ambayo waliiogelea awali na hivyo kukifahamu kina chake.

Shukrani za dhati pia zimfikie Daniel Mutiiria Mbajo, aliyenipa changamoto ya kurejea chuoni baada ya kuwa 'huru' kwa miaka chungu nzima.

Nawashukuru pia wahadhiri wa Idara ya Kiswahili walionifaa kwa mengi, hususan Dkt. Richard Wafula na Njagi Matti ambao ushauri wao ulinipa msukumo wa kuendelea.

Wanafunzi wenzangu, hasa Lewis Mutegi wafikiwe na shukrani hizi kwani kwa kutiana shime hata mambo yalipotuwia magumu tuliweza kusonga mbele kama askari waliokula kiapo cha kuihami lugha ya taifa lao tukufu.

Kwako wewe uliyeniombea na kunitakia heri, japo sijakutaja ninakiri hivi:

Hongera kwa kunijali, na kuenzi Kiswahili
Hakika nimekubali, sitoficha jambo hili
Kwani ndilo la hakika
Singeweza
bila
WEWE!

Haya yote yamewezekana kwa mapenzi yake **MUNGU**. Jina lake litukuzwe.

**IKISIRI**

Utafiti huu umeshughulikia swala la usawiri wa wahusika katika mashairi ya Kiswahili. Mtafiti ameyahakiki mashairi teule ya washairi wawili kwa lengo la kutathmini jinsi washairi hawa walivyowateua wahusika wao, aina za wahusika na *jinsi* wahusika hawa walivyotumiwa kutolea hisia za washairi. Diwani zilizochaguliwa ni mbili; moja ya Hassan Mwalimu Mbega **Dafina ya Umalenga** (1984) na nyingine ya Said Ahmed Mohamed **Jicho la Ndani** (2002).

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni ile ya Ulimbwende ambayo hujaribu kueleza umuhimu wa wahusika katika ushairi, hasa katika kutolea hisia za mshairi badala ya kujifunga na arudhi. Nadharia hii pia hueleza umuhimu wa kuzingatia mazingira ya aina mbalimbali katika utunzi wa mashairi.

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza ni utangulizi wa utafiti ambapo mtafiti ameifafanua mada ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo wa utafiti. Sura hii pia inao ufafanuzi juu ya udurusu wa maandishi yanayohusu mada hii pamoja na nadharia iliyoongoza utafiti. Hatimaye pana maelezo juu ya mbinu za utafiti zilizotumika.

Katika sura ya pili pamejadiliwa vigezo vinavyozingatiwa na washairi katika uteuzi wa wahusika wao. Mtafiti ameshughulikia aina mbalimbali za mazingira ambayo huchangia katika uteuzi wa wahusika.

Sura ya tatu imejadili aina za wahusika wanaopatikana katika mashairi teule na jinsi washairi walivyowaunga kwa ubunifu wa hali ya juu kwa lengo la kuuwasilisha ujumbe wao kikamilifu.

Mtafiti ameangalia jinsi wahusika hawa wanavyohusiana na kuathiriana na hivyo kusaidia katika ujenzi wa maudhui.

Katika sura ya nne mtafiti amejadili jinsi washairi walivyowatumia wahusika kudhihirisha hisia mbalimbali.

Sura ya tano ni hitimisho linalotoa muhtasari na matokeo ya utafiti, pamoja na mapendekezo ya mtafiti.

Mwishoni mwa tasnifu kuna marejeleo ya utafiti huu.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA TASNIFU

## 1.0 Ufafanuzi wa *Dhana* Muhimu

Mhusika – Huyu ni kiumbe anayepatikana katika kazi ya kifasihi na ambaye *anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Mhusika anaweza kuwa binadamu*, mnyama au kitu kisicho hai. Maumbile ya aina mbalimbali yatazingatiwa kama wahusika, bora tu yawe yamepewa uwezo wa kusababisha kitendo au hali fulani. Katika utafiti huu tutazingatia pia sehemu za mwili zilizosawiriwa kama wahusika katika mashairi kadha.

Shairi – Huu ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalum wa lugha ya mkato katika usemi. Mtungo huu hueleza wazo au mawazo, hisi au tukio juu ya maisha. Utafiti huu utazingatia mashairi ya kiarudhi pamoja na mashairi huru yaliyo na wahusika mahsusi.

Arudhi – Ni kanuni au sheria zinazozingatiwa katika utunzi wa mashairi, kama vile kuwepo kwa beti zenye mpangilio maalum wa mishororo, vina, mizani na kibwagizo. Mashairi ya kiarudhi hupewa majina maalum kama vile tathlitha, tarbia na takhmisa kutegemea idadi ya mishororo katika kila ubeti.Mashairi yasiyojifunga na kanuni *hizi hujulikana* kama *mashairi huru*.

Mashairi ya Hisia – Ni mashairi yanayotungwa kwa lengo la kudhihirisha hisia nzito za mshairi kuhusu hali zinazowakumba wahusika mbalimbali katika hali na matukio tofauti maishani. Katika mashairi ya aina hii *wahusika, mazingira yao* na *hisia* zao husisitizwa.

Soniti –Aina ya mashairi mafupi ya kihisia yanayoimbwa kwa nia ya kudhihirisha mikabala mbalimbali ya wazo moja au hisia, ambayo wakati mwingine hupata suluhu katika aya za mwisho mwisho au kufikia mwisho wa shairi.

Sitiari/ Istiari- Ni mbinu ya ulinganishi ambapo kitu hulinganishwa na kingine kitabia, kwa msingi wa sifa fulani iliyopo kati ya vyote viwili bila kutaja wazi sifa yenyewe. Kwa mfano mtu shujaa anaweza kuitwa simba.

Metonumia - Ni mbinu ya usemaji na uandishi ambapo neno hutumika kuwakilisha dhana, kitu au mtu. Kwa mfano *kifo* kinaweza kuashiria kuangamia kwa taifa au *moyo* kumwakilisha mtu.

Masafa Ujumi- Ni umbali wa kihisia ulioko kati ya msikilizaji au msomaji wa kazi ya sanaa na kazi yenyewe, hasa kwa kuzingatia ubunifu wa kazi hiyo.

Tanakuzi – Ni aina ya ulinganushi ambapo kitu kinachotanguliwa hupingwa na kile kinachokifuatia. Kwa mfano, maisha ya kitajiri yanaweza kujitokeza katika beti za mwanzo mwanzo za shairi, kisha maisha ya kimaskini yakasawiriwa katika beti zinazofuatia kwa lengo la kuwalinganua wahusika wake kitabaka.

Tashbihi – Aina ya ulinganishi ambapo mtu au kitu hulinganishwa na mwingine au kingine kwa mujibu wa sifa fulani. Vilinganishi kama vile 'kama', 'kana kwamba', 'kama vile', 'ja' na 'sawa na' hutumika. Mtumiaji wa tashbihi huongozwa na hali fulani zinazolingana baina ya watu au vitu hivyo. Kwa mfano, mtu mrefu sana *anaweza kulinganishwa na mlingoti kitashbihi kwa kusema kuwa yeye ni mrefu* kama mlingoti. Katika utafiti huu, wahusika wa kitashbihi ni wale wanaolinganishwa na wengine kwa kuzingatia mifanano fulani.

Taswira-Ni picha ya mambo au vitu inayomjia mtu mawazoni mwake anaposoma au kusikiliza kazi ya sanaa. Msomaji au msikilizaji huweza kuyaona matukio, mazingira yanayotendekea pamoja na wahusika wake mawazoni mwake kana kwamba mambo hayo yanatendeka hasa. Taswira hutokea vyema iwapo matukio, mazingira na wahusika vimesawiriwa kwa ubunifu wa hali ya juu.

## 1.1 Utangulizi

Swala la wahusika limezingatiwa sana na wahakiki mbalimbali wa kazi za fasihi. Njogu na Chimerah *(1999)* wameshughulikia wahusika katika tanzu za fasihi simulizi na fasihi andishi. Watafiti hawa wamejaribu kuainisha wahusika kama *wanavyodhihirika katika tanzu hizi za fasihi. Wamezingatia aina mbalimbali za* wahusika, sifa zao, mazingira yao na umuhimu wao katika kazi husika. Hawa wanashikilia pia kuwa wahusika wanapatikana tu katika mashairi marefu ya kimasimulizi na yale ya aina ya ngonjera, na kuyapuuza mashairi mafupi ambayo baadhi yake yana wahusika muhimu.

Mawazo ya wataalamu hawa yanatokana na dhana kuwa mashairi ya kimasimulizi kama vile tendi huwa na wahusika mashujaa ambao hupewa nafasi ya kukua na kupitia hatua mbalimbali za maisha. Kwa kuwa masimulizi haya huwazungumzia binadamu halisi waliopata kuishi, tabia zao huwa dhahiri na za kusadikika.

Wahusika katika ngonjera nao huwa dhahiri zaidi kwa kuwa mpangilio wa mashairi haya huwa kama ule wa tamthilia, ambapo maneno na matendo yao yanaweza hata kuigizika. Hata hivyo, utafiti huu unanuia kudhihirisha kuwa yapo mashairi ya aina nyinginezo yaliyo na wahusika muhimu ambao hawafai kupuuzwa kamwe.

Msokile (1993) pia amezingatia swala la wahusika kama mojawapo wa misingi ya uhakiki wa fasihi. Amedokeza juu ya umuhimu wa kuzingatia aina kadha za wahusika katika uhakiki wa riwaya, tamthilia na mashairi.

Aidha, Mazrui na Syambo (1992) wamezingatia kwa kina uhakiki wa wahusika katika fasihi simulizi na fasihi andishi kwa jumla. Sawa na wenzao tuliowataja hapo juu, wameshughulikia wahusika wa aina mbalimbali.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Swala kuu hapa ni kwamba wataalamu hawa wanatudhihirishia kuwa wahusika ni nguzo muhimu katika kazi yoyote ya fasihi. Hata hivyo, kadiri ya ufahamu wa mtafiti, swala *hili* halijapewa uzito wa kutosha katika ushairi kwani uchambuzi ambao umefanywa aghalabu umejikita sana katika dhamira, maudhui na umbo.

Utafiti huu unadhamiria kuchunguza na kudhihirisha umuhimu wa wahusika katika kutolea hisia za mshairi, na hivyo kusaidia kujenga dhamira na maudhui katika ushairi wa Kiswahili. Wahusika wanasisitizwa hapa kwa kuwa ndio malighafi ya kujengea vipengele hivyo vingine. Hali hii inatokana na misingi kwamba kazi *yoyote ya fasihi inadhamiriwa binadamu, na hivyo sharti imsawiri binadamu jinsi* alivyo au jinsi anavyopaswa kuwa katika mazingira yake halisi.

Mshairi, sawa na msanii mwingine yeyote huitumia sanaa kuelezea hisia zake kuhusu maswala mbalimbali ambayo amepata kuyashuhudia, kuyasikia au kuyafikiria. Maswala haya aghalabu huhusiana na binadamu na mienendo yake katika mazingira yake na namna anavyohusiana na wenzake. Tabia za binadamu *hawa huwasilishwa kupitia uumbaji wa wahusika, na hivyo* kuwafanya kuwa kipengele muhimu cha kuzingatiwa katika uhakiki wa kazi za fasihi, ukiwemo ushairi.

Utafiti huu umeshughulikia kwa kina usawiri wa wahusika katika mashairi ya Hassan Mwalimu Mbega (1984) na Said Ahmed Mohamed (2002) katika diwani zao, **Dafina ya Umalenga** na **Jicho la Ndani** mtawalio.

Katika kuchunguza swala hili tumeshughulikia wahusika binadamu, wahusika wanyama na wahusika vitu na kudhihirisha jinsi wanavyochangia katika kutolea hisia za washairi na hivyo kusaidia katika kuendeleza dhamira na maudhui.

## 1.2 Swala la Utafiti

Utafiti huu umechunguza usawiri wa wahusika katika taaluma ya ushairi wa Kiswahili. Kadiri ya ufahamu wa mtafiti, umuhimu wa wahusika katika kuendeleza dhamira na maudhui haujashughulikiwa vilivyo katika tahakiki za watafiti wengi. Tafiti nyingi zimeshughulikia zaidi maswala ya arudhi na maudhui. Ingawa hatuwezi kamwe kupuuza umuhimu wa umbo la nje la shairi, ni vyema pia kupanua mawanda ya uhakiki kwa kuzingatia umbo lake la ndani, hasa usawiri wa wahusika wake. Utafiti huu umechunguza jinsi washairi mbalimbali huwateua wahusika wanaowasawiri katika mashairi yao, vigezo vinavyoongoza uteuzi huu na umuhimu wao katika uendelezaji wa dhamira na maudhui.

## 1.3 Maswali Yaliyojibiwa na Utafiti

Utafiti huu uliyajibu maswali yafuatayo:

a) Je, washairi mbalimbali huwachagua vipi wahusika wao?
b) Ni wahusika wa aina gani wanaopatikana katika mashairi ya Kiswahili?
c) Je, wahusika hawa wanatekeleza wajibu gani katika ushairi?
d) Je, usawiri wa wahusika huakisi vipi hali ya mazingira ya mshairi?

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Uhakiki wa mashairi teule ya Kiswahili ulifanywa kwa kuzingatia malengo yafuatayo:

**a)** Kuonyesha namna washairi tofauti huwachagua wahusika wao.
**b)** Kuchunguza na kuainisha wahusika mbalimbali katika mashairi ya Kiswahili.
**c)** Kuonyesha umuhimu wa wahusika katika udhihirishaji wa hisia za mshairi kupitia ujumbe wake.
**d)** Kubainisha kwamba usawiri wa wahusika huakisi hali ya mazingira kwa mujibu wa wakati.

## 1.5 Nadharia Tete

a) Uchaguzi wa wahusika hutegemea mazingira ya mshairi.

b) Kuna aina kadha za wahusika katika mashairi ya Kiswahili.

c) Wahusika ni chombo muhimu cha kudhihirishia hisia za mshairi.

d) *Usawiri wa wahusika huakisi hali mbalimbali za mazingira* kwa *mujibu* wa wakati.

## 1.6 Sababu za Kuchagua Mada

Mada hii imechaguliwa kwa kuzingatia kuwa kwa miaka mingi ushairi wa Kiswahili umekuwa ukihakikiwa kwa kuzingatia mipaka ya kiuhakiki iliyowekwa na washairi na wahakiki wa kimapokeo. Hata baada ya kuzuka kwa washairi na wahakiki wa *kimapinduzi, matapo haya mawili yamekuwa yaking'ang'ania swala la kuzingatia* au kutozingatia arudhi za ushairi na hivyo kutoshughulikia kikamilifu mbinu nyinginezo za ubunifu za kulihakikia shairi la Kiswahili. Ndiposa vipengele muhimu katika sanaa hii kongwe kama vile wahusika vikakosa kuangaziwa kwa kina.

Utafiti huu umefanywa ikizingatiwa kwamba kadiri ya ufahamu wa mtafiti, mada hii haijachunguzwa kikamilifu na watafiti waliotangulia. Baadhi ya watafiti wa awali walijikita zaidi katika maswala ya maudhui, umbo na mtindo bila kufungamanisha maswala haya na usawiri wa wahusika.

Mtafiti pia alinuia kuchunguza ufaafu wa maoni ya Njogu na Chimerah (1999) kwamba mashairi mengi hayana wahusika na kuwa ni mashairi ya masimulizi tu yaliyo na wahusika. Utafiti huu umedhihirisha kuwa yapo mashairi mafupi yaliyo na wahusika dhahiri walio na dhima sawa na wahusika katika mashairi marefu ya kimasimulizi.

Ili kuishughulikia hoja hii kikamilifu, mtafiti aliyachunguza mashairi ya kiarudhi na pia mashairi huru. Kigezo kilichotuongoza hapa ni kuwa mashairi ya aina zote mbili yanapewa uzito sawa katika mtalaa wa shule za upili. Utafiti huu ulinuiwa kuitumia dhana ya wahusika na dhima yao katika ushairi kama kiunganishi kati ya wahakiki *na watunzi wa mashairi ya kiarudhi na wale wa mashairi huru na hivyo kusaidia* katika kuukomesha mgogoro wa ushairi.

Pili, mtafiti alizingatia kuwa usawiri wa wahusika katika mashairi ya aina zote mbili huenda ukatofautiana kutokana na swala la kufungwa au kutofungwa na arudhi. Utafiti huu umeonyesha jinsi washairi teule wamewatumia wahusika wa aina mbalimbali kutolea hisia zao, na hivyo kuendeleza dhamira na maudhui bila *kukinzwa na kuwepo au kutokuwepo kwa arudhi. Hili limedhihirisha kuwa usawiri* wa wahusika katika mashairi ya Kiswahili hautegemei umbo la nje, bora tu mshairi autumie ubunifu wake vyema.

Kupitia utafiti huu, mtafiti alinuia kuwapa wahakiki wa mashairi ya Kiswahili changamoto ya kukizingatia kwa kina kipengele cha wahusika katika uhakiki wao. Mtafiti alinuia kuonyesha kwamba, kinyume na maoni ya wanafunzi na wahakiki wengi, utanzu wa ushairi wa Kiswahili si 'mkavu' kwani umesheheni vipengele kadha vinavyouhuisha.

Utafiti huu vilevile ulichochewa na sababu kwamba ujumbe katika kazi yoyote ya fasihi hushughulikiwa kwa njia mbalimbali kiubunifu. Jamii itasawiriwa katika kazi za fasihi kupitia wahusika kwani ndio wawakilishi na viwakilishi vya hali halisi za wanajamii. Wahusika hawa wanayo dhima kuu ya kuwasilisha ujumbe mahsusi kwa *wanajamii. Jinsi mshairi akatavyowasawiri wahusika wake itatufanya kuyapenda au* kuyachukia matendo na tabia fulani za wanajamii waliowakilishwa na wahusika hao.

Kupitia matokeo ya utafiti huu, inatarajiwa kwamba watunzi mbalimbali watapata changamoto ya kuzingatia dhima ya wahusika katika uendelezaji wa maudhui watungapo. Ni matumaini ya mtafiti kuwa patatungwa mashairi mengi yanayolenga kuwasawiri wahusika waliopewa nafasi ya kukua kikamilifu na kuendeleza *maudhui, badala ya kutilia mkazo zaidi upande wa maumbo.*

## 1.7 Upeo wa Utafiti

Usawiri wa wahusika katika mashairi unaweza kutazamwa kwa mikabala ya fasihi simulizi na pia fasihi andishi. Utafiti huu ulijikita katika usawiri wa wahusika *katika mashairi andishi ya Kiswahili kama mojawapo wa vipengele muhimu* vinavyofaa kuzingatiwa katika uhakiki wake.

Utafiti huu umeangazia mashairi ya kiarudhi na mashairi huru.
Mtafiti alijikita katika diwani mbili. Diwani hizi ni:

i. **Dafina ya Umalenga** (Hassan Mwalimu Mbega, 1984).
ii. **Jicho la Ndani** (S.A. Mohamed, 2002).

Vitabu hivi viliteuliwa kutokana na vigezo kadha. Kwanza, watunzi wa mashairi yaliyomo wamebobea katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili, huku wakizingatia wahusika wa aina mbalimbali katika mashairi yao. *Pili*, usawiri wao wa wahusika umekita katika vipindi na mazingira tofauti ya kihistoria. Hassan Mwalimu Mbega *ni mshairi mkongwe aliyeyatunga mashairi kutokana na tajriba aliyoipata katika* mazingira ya Waswahili ilhali Said Ahmed Mohamed ni mshairi msomi ambaye huenda ameathiriwa na nadharia za kiusomi na mazingira tofauti tofauti.

Kigezo cha tatu ni kuwa washairi hawa wamekulia katika maeneo tofauti ya kijiografia (wa kwanza akiwa mzaliwa wa Kwale nchini Kenya na wa pili akiwa

mzaliwa wa Tanzania), na hivyo uteuzi wao wa wahusika huenda uliathiriwa na maswala ya mazingira tofauti kama yale ya kihistoria, kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Nne, washairi hawa wamezingatia mashairi ya aina tofauti. Hassan Mwalimu Mbega ametunga mashairi ya kiarudhi pekee huku S.A. Mohamed akitunga yale ya kiarudhi na pia mashairi huru. Hili limempa mtafiti nafasi ya kuyahakiki mashairi ya aina zote mbili.

## 1.8 Udurusu wa Maandishi

Swala la wahusika katika ushairi limeshughulikiwa na wahakiki kadha. Wahakiki hawa wamezingatia mitazamo kadha katika uhakiki wao kutegemea malengo yao. Wapo pia wahakiki ambao wamejaribu kueleza maana ya shairi la Kiswahili na ushairi kwa jumla.

Senkoro (1988) amelishughulikia swala la maana ya shairi la Kiswahili kwa kuyanukuu maoni ya washairi na wahakiki mbalimbali. Anayazingatia maoni ya wanamapokeo na wanamapinduzi kuhusu vipengele vinavyopaswa kuzingatiwa katika kulifasili shairi la Kiswahili. Anawanukuu wanamapokeo kama vile Abdalla (1973) wanaosisitiza kuwa shairi la Kiswahili sharti liwe na sifa zifuatazo:

a) Urari wa vina na mizani

b) Maneno machache na ya mkato

c) Uimbikaji

d) Ufasaha wa lugha au lugha nzito

e) Lidhihirishe mawazo, maono na fikira za ndani zinazovuta moyo kwa namna ya ajabu.

Anawanukuu pia wanamapinduzi kama vile Kezilahabi (1974), Mulokozi (1975) na Kahigi (1975) wanaosisitiza sifa zifuatazo katika shairi:



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

a) Kuwepo kwa wazo lililoelezwa vyema

b) Upangaji mzuri wa maneno katika kulieleza wazo hilo

c) Lugha ya mkato

d) Maelezo mafupi yanayolenga ukweli fulani wa maisha

*e) Maelezo hayo yatolewe kwa njia inayoburudisha na kugusa moyo.*

Maoni haya ni muhimu kwa kuujengea msingi utafiti huu kwani yanaiangalia mitazamo ya matapo mawili ambayo hukinzana kuhusu maana ya shairi la Kiswahili. Utafiti huu umeonyesha jinsi wahusika katika mashairi ya aina zote mbili wamesawiriwa kwani unayatambua mashairi ya aina zote mbili kuwa mashairi kamili.

Kuhusu wahusika, Senkoro (1988) anafafanua juu ya ujenzi wa taswira kupitia wahusika watu, wanyama, wadudu, majini na mashetani. Kazi hii imechangia utafiti huu kwa kuwa inagusia juu ya aina za wahusika na ujenzi wa taswira, ambavyo vimeshughulikiwa katika utafiti huu. Hata hivyo, kutokana na udadisi wa mtafiti, *imesadifu tu kwamba mhakiki huyu hangeweza kushughulikia taswira bila kuwataja* wahusika bali hakuudhamiria uhakiki wa wahusika.

King'ei na Kemoli (2001) wanawafasili wahusika kama viumbe, vitu au watendi wanaotumiwa na mshairi katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Wanaeleza kuwa washairi huwatumia wahusika kwa nadra sana, isipokuwa katika tenzi na mashairi ya masimulizi, hasa mashairi ya kimapinduzi. Kuhusu uhakiki wake, *wataalamu hawa wanapendekeza kuwa vigezo kama vile sifa, tabia na taswira ya* wahusika vizingatiwe. Wanautambua vyema umuhimu wa wahusika katika kusawiri matukio ya shairi na kushadidia maudhui na dhamira ya shairi. Hata hivyo, waliacha nje swala la udhihirishaji wa hisia za mshairi kupitia wahusika ambalo limeshughulikiwa katika utafiti huu.

Njogu na Chimerah (1999) wamewashughulikia wahusika wakiongozwa na maswali yafuatayo:

i. Wahusika hao wana sifa gani? Tabia zao zinawabainisha kama wahusika wa aina gani?
ii. *Je, wahusika hao wanaingiliana vipi?*
iii. Tunapata taswira ya aina gani tukizingatia matendo yao au maneno yao? (1999:92)

Hawa wamechangia utafiti huu kwa kuwa wamegusia sifa za wahusika, jinsi wanavyoingiliana na taswira tunayopata kutokana na matendo au maneno yao. Hata hivyo, hawakuzingatia umuhimu wa mazingira katika uteuzi wa wahusika na jinsi wahusika hao wanavyoakisi hali ya mazingira ya mtunzi kwa mujibu wa wakati.

Msokile (1993) amelichunguza swala la wahusika katika mashairi ya Kiswahili kwa kuzingatia aina mbalimbali za wahusika. Ameyahakiki mashairi kadha na kuainisha wahusika watu, wahusika vitu na wahusika wanyama. Katika kuhakiki wahusika wanyama na wahusika vitu, mhakiki amechukua mtazamo wa kitamathali ambapo wanyama na vitu wanawakilisha watu na dhana mbalimbali. Kazi hii imechangia utafiti huu kwa kuwa baadhi ya wahusika aliowashughulikia mhakiki ni wale wa kitamathali. Tofauti na utafiti huu, mhakiki huyu hakuangazia jinsi washairi huwateua wahusika wao kwa kuzingatia mazingira wanamoishi na pia jinsi wahusika hutumiwa kudhihirisha hisia za mshairi.

Mazrui na Syambo (1992) wamewachunguza wahusika binadamu katika tungo za kujibizana. Wanarejelea historia ya usemezano katika ushairi wa Kiswahili kwa jumla na kuzingatia hasa uhusika katika ngonjera. Katika uhakiki wao wamezingatia ngonjera ya Abdilatif Abdalla iitwayo 'Mnazi Vuta N'kuvute', ambapo pana majibizano kati ya mhusika Alii na Badi. Huu ni mfano wa wahusika dhahiri katika shairi lenye muundo wa kitamthilia. Utafiti huu haukuzingatia

mashairi yoyote ya ngonjera (ambayo wahusika wake ni dhahiri) kwani ulinuia kuonyesha kuwa mashairi ya aina nyinginezo pia yanao wahusika muhimu.

Njogu (2004) ametafiti kwa mapana kuhusu usemezano katika ushairi. Ameuangalia usemezano kwa kuzingatia nadharia ya U-Bakhtin na kutambulisha aina mbili kuu za usemezano katika ushairi. Aina ya kwanza ni usemezano kati ya washairi wawili au zaidi, ambapo washairi hupimana nguvu za kiutunzi kupitia *maswali na mafumbo. Aina ya pili ni usemezano kati ya wahusika wawili au zaidi* katika shairi lililotungwa na mshairi mmoja. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwa vile mtaalamu huyu hakuzingatia swala la utoaji wa hisia, ujenzi wa dhamira, maudhui na taswira bali amejikita zaidi katika usemezano.

Ndungo (1985) ameshughulikia maswala ya wanawake katika fasihi ya Kiswahili kwa kuongozwa na nadharia ya Kifeministi. Ameutazama usawiri wa mwanamke katika **Utendi wa Mwanakupona** (1860) na kudhihirisha jinsi mhusika wa kike anavyonyanyaswa katika miktadha ya kidini na ndoa. Lengo lake hapa halikuwa *kuwachunguza wahusika katika ushairi kwa jumla bali mhusika wa kike na matatizo* yanayomkabili. Wahusika wa jinsia na aina nyingine hawakushughulikiwa kama utafiti wetu unavyofanya.

Momanyi (1998) naye ametafiti kuhusu usawiri wa mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili katika ushairi wa Kiswahili. Sawa na Ndungo (1985), mtafiti huyu alilenga maswala ya kifeministi katika utafiti wake. Amefaulu katika udhihirishaji wa jinsi mwanamke Muislamu anavyodunishwa kupitia mafunzo ya dini ya Kiislamu. Yeye pia aliwaacha nje wahusika wa aina nyinginezo. Utafiti wetu unashughulikia wahusika binadamu, wahusika wanyama, sehemu za mwili, maumbile na vitu vingine.

Babusa (2005) amegusia mashairi ya hisia ambapo mshairi hujitia katika nafsi ya mtenda au mtendewa ambaye huwa mhusika wa kubuni na kusimulia yanayomsibu katika nafsi ya kwanza. Mashairi hayo aghalabu huwa mafupi kama vile wimbo, utumbuizo, shairi la huzuni au soniti. Wahusika wake hudhihirisha tabia zao za kibinafsi kupitia maisha na matamko yao. Kazi hii inachangia utafiti huu kwani inagusia maswala ya hisia na tabia za wahusika sawa na utafiti huu. Hata hivyo, mhakiki huyu aliacha nje wahusika katika mashairi ya kimasimulizi na mashairi huru ambayo yameshughulikiwa katika utafiti huu.

Wafula (1992) akimnukuu Wordsworth (1798) anasema kuwa mshairi hutunga kudhihirisha hisia nzito zinazotokana na tajriba anazopitia. Kwa mujibu wa Wordsworth, ushairi ni bubujiko la hisia ambazo hudhihirika vyema kupitia wahusika waliosawiriwa kupitia ubunifu wa hali ya juu. Makala haya ni muhimu katika utafiti huu kwa kuwa yanajadili juu ya umuhimu wa udhihirishaji wa hisia nzito kupitia wahusika kwa njia ya kiubunifu, sawa na utafiti huu. Pia yanagusia umuhimu wa kuzingatia tajriba anazopitia mshairi katika mazingira halisi, sawa na utafiti huu. Hata hivyo, mhakiki huyu hakuzingatia aina mbalimbali za wahusika na umbuji wao kishairi kama ulivyofanya utafiti huu.

Watafiti hawa kwa jumla wamechunguza uhusika katika mashairi katika mikabala tofauti. Wote wanadhihirisha kuwa wapo wahusika muhimu katika mashairi ya Kiswahili. Kazi zao zinauwekea msingi utafiti huu kwa kuwa zimezingatia wahusika wa aina kadha kutegemea mtazamo wa kila mtafiti. Kazi zote tulizotazama hapa zimejikita katika utafiti wa maktabani, sawa na utafiti huu. Pia zimezingatia kazi za fasihi andishi sawa na utafiti huu. Ingawa hivyo, kulingana na ufahamu wa mtafiti, kazi binafsi zilizorejelewa hazijalishughulikia swala la wahusika kwa kina kama unavyofanya utafiti huu. Utafiti huu unaangazia uteuzi wa wahusika, aina za wahusika, wajibu unaotekelezwa na wahusika na jinsi wahusika hawa wanavyoakisi hali ya mazingira kwa mujibu wa wakati.

Hata hivyo, kazi za kitafiti tulizogusia zinajikita tu katika wahusika binadamu. Wahusika hawa pia wameangaliwa katika mikabala ya kisemezano na kifeministi pekee. Ipo haja ya utafiti wa wahusika kuzingatia vipengele vinginevyo kama wanavyojitokeza katika mashairi mengi ya Kiswahili. Kipengele kimojawapo *muhimu ni umuhimu wao katika udhihirishaji wa hisia za mshairi na hivyo* kuendeleza maudhui.

Utafiti huu umewashughulikia wahusika binadamu, wahusika wanyama na wahusika vitu kwa lengo la kudhihirisha umuhimu wao katika udhihirishaji wa hisia za mshairi.

**1.9 Msingi wa Nadharia**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ulimbwende. Ousby (1992) anasema kuwa waasisi wa nadharia hii ni William Wordsworth na Samuel Taylor Coleridge ambao walihisi *kuwa fasihi, hasa ushairi, ilifaa kutumika kuelezea hisia nzito kupitia* ubunifu wa hali ya juu bila kutanzwa na arudhi za kijadi. Anaongeza kuwa mtazamo huu ulijaribu kuelezea mabadiliko yaliyodhihirika katika fasihi, sanaa na utamaduni huko Uropa kwa lengo la 'kuiokoa' fasihi kutokana na silisili za kiarudhi zilizoifanya kuwa vigumu kujieleza.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) istilahi hii ilitumiwa kuelezea sifa za sanaa, muziki, siasa, falsafa na fasihi za Ulaya na Marekani mwisho mwisho mwa karne ya 18 na mwanzo mwanzo mwa karne ya 19. Anaongeza kuwa mtazamo huu ulielekea kutukuza mtu binafsi katika ngazi za kijamii, kisiasa na kiakili. Pia ulisisitiza uhuru wa waandishi wa kujielezea kibinafsi kwa mitindo na mikabala yao bila kufungwa na sheria za kiutunzi zilizokuwemo kwa muda mrefu.

Hill (1977) anaeleza kuwa Wordsworth na Coleridge waliendeleza msimamo wa kilimbwende kupitia mashairi ya kihisia waliyoyaita *Lyrical Ballads*. Coleridge aliyatunga mashairi yaliyosisitiza kuwepo kwa matukio na wahusika wenye sifa za ukia-umbile. Hawa pia walifungamanishwa na hisia nzito ambazo zingejitokeza *endapo matukio hayo yangekuwa halisi huku yakisababishwa na nguvu zisizo za* kimaumbile.

Coleridge aliwateua wahusika na matukio kutokana na maisha ya kawaida kama ambavyo wangepatikana katika kijiji chochote na vitongoji vyake. Mshairi huyu angewatafakari, kuwafuatilia na kuwatambua wahusika hao pindi walipojitokeza ili aweze kuwasawiri katika mashairi yake katika uhalisia wao.

Katika mashairi yake, Coleridge alikita katika binadamu na wahusika wenye sifa zisizo za kimaumbile, au angalau wenye hisia nzito za kimapenzi kwa lengo la kudhihirisha hisia za ndani za binadamu katika uhalisia wake.

Wordsworth, kwa upande mwingine alilenga kuyatunga mashairi yaliyoyapa maisha ya kila siku uchangamfu usio wa kawaida, kwa kuzizindua akili na kuziondoa katika hali ya mazoea na kuziongoza hadi kwenye uchangamfu na maajabu ya ulimwengu uliotuzunguka. *Alihisi kuwa ulimwengu ni hazina kuu isiyomalizika lakini* binadamu ameidunisha kwa kuigubika ukawaida kupitia kuishi maisha ya kibinafsi *na ya kujitenga, kiasi kwamba tuna macho lakini hatuoni, tunayo masikio lakini* hatusikii, na pia tunazo nyoyo zisizohisi wala kutambua chochote.

Utafiti huu ulizingatia nadharia hii kwa kuongozwa na mihimili iliyofafanuliwa na Hill (1977), kuwa ni nadharia inayosisitiza:

i) Uteuzi wa matukio na hali kutokana na maisha ya kawaida
ii) Uteuzi wa aina mbalimbali za wahusika na vitendo vyao kwa

ubunifu wa hali ya juu, ambapo vitu vya kawaida huwasilishwa akilini kwa njia isiyo ya kawaida

iii) Utumiaji wa ubunifu kuwaunga wahusika pamoja, wawe viumbe vilivyo hai au vitu visivyo hai

iv) Kuyafanya matukio na hali zilizomo kuvutia kwa kuyahusisha na hali ya kimaumbile na ujenzi wa taswira

v) Kuwafanya wahusika waziakisi hali za mazingira kwa mujibu wa wakati

vi) Kuwafungamanisha wahusika na hisia nzito ambazo zingejitokeza iwapo matukio hayo yangekuwa halisi.

Nadharia hii ilifaa katika utafiti huu kwa kuwa inazingatia wahusika wa aina mbalimbali kama wanavyopatikana katika mazingira na hali tofauti. Nadharia hii pia inazingatia hisia za wahusika ambazo ni kipengele muhimu cha kuwahakikia wahusika katika mashairi ya Kiswahili.

Nadharia hii pia ni muhimu kwa kuwa inasisitiza juu ya ubunifu ambao ndio huongoza usawiri wa wahusika. Kwa kuwa ushairi ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu, usawiri bora wa wahusika sharti uhitaji ubunifu wa hali ya juu. Kwa jumla, inautambua ushairi kama sanaa isiyofaa kuwekewa mipaka ya kiarudhi, na badala yake kuutambua ubunifu kama nyenzo muhimu ya kumwongoza mtunzi. Kwa kufanya hivyo, nadharia hii inaupa uhakiki wa mashairi ya Kiswahili mwongozo wa kitaaluma na kuutoa katika misingi finyu ya kiarudhi iliyowekwa na wanajadi ambao hawakuwa wasomi.

Ufaafu wa nadharia hii pia unatokana na misingi kuwa inayapa mashairi uwanda mpana wa kihakiki usiopendelea upande wowote, hasa ikizingatiwa kuwa mtafiti ameyahakiki mashairi huru na yale ya kiarudhi. Ni nadharia inayojaribu kujenga

ngazi kati ya wanajadi na wanamapinduzi na hivyo kuchangia pakubwa katika usuluhishaji wa mgogoro wa ushairi.

## 1.10 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu umejikita katika mbinu moja kuu ya utafiti, ambayo ni ya maktabani. Mtafiti amedurusu vitabu, majarida, makala na tasnifu mbalimbali zilizohusiana na mada hii ili kupata maoni ya waandishi mbalimbali yaliyompa mwanga zaidi alipotafiti. Ni *kupitia udurusu huu ambapo mtafiti aliweza kutambua* kina walichofikia waandishi na watafiti wa hapo awali ili aweze kuzama zaidi katika utafiti wake.

Udurusu huu pia ulimwezesha mtafiti kupata mengi kuhusu msingi wa nadharia aliyoizingatia ili kuupa utafiti wake misingi shakiki ya kitaaluma.

Kwa kuzingatia yaliyoandikwa na wataalamu mbalimbali, mtafiti aliweza kutambua pengo la utafiti wa baadaye kuhusiana na mada hii na hivyo kuweza kutoa mapendekezo mwafaka kufikia mwisho wa utafiti huu.

### A. Ukusanyaji wa Data

Data yote imetolewa katika diwani mbili zilizoteuliwa. Mtafiti alishughulikia data ya kubainisha mambo mbalimbali yanayoathiri uteuzi wa wahusika katika mashairi ili kubainisha muktadha ambamo wahusika hawa wanatumika.

Data kuhusu aina mbalimbali za wahusika na jinsi walivyoungwa pamoja kiubunifu ilizingatiwa. Uteuzi huu ulifanywa kwa kuzingatia hisia kuwa wahusika muhimu wapatikanao katika mashairi ya Kiswahili wanaweza kujumlishwa katika makundi kadha. Wahusika hawa pia wanapatikana katika mazingira ya kawaida, na hivyo *mshairi huutumia ubunifu* wake *kuwaunga pamoja ili* wauwasilishe ujumbe alioukusudia.

Hatimaye utafiti huu ulishughulikia ukusanyaji wa data iliyoonyesha jinsi washairi teule walivyowatumia wahusika kudhihirisha hisia mbalimbali kwa lengo la kubainisha umuhimu wa wahusika katika mashairi. Mtafiti alizichunguza hisia kadha zilizotolewa na washairi katika mashairi teule na kubainisha jinsi wahusika walitumika kuzidhihirisha.

**Sampuli**

Kwa kuwa utafiti huu uliwalenga washairi waliotunga mashairi yenye sifa mahsusi, sampuli yakini ilitumika. Mashairi teule yalihakikiwa kutoka kwa diwani zilizotungwa na washairi kutoka maeneo na viwango tofauti vya elimu, kwa kuzingatia kuwa usawiri wao wa wahusika huenda ukatofautiana kutegemea viwango vyao vya elimu na mazingira ya utunzi.

**b) Uchanganuzi na uwasilishaji wa data**

Data iliyokusanywa kutoka vitabu vilivyoteuliwa ilipangwa katika makundi kwa kuzingatia malengo ya utafiti na vipengele mahsusi.

Kwanza, vigezo vinavyochangia uteuzi wa wahusika kwa jumla vilizingatiwa ili kubainisha kuwa mtunzi huwateua wahusika wake kutokana na mazingira anamoishi. Vigezo vilivyozingatiwa katika uchanganuzi wa data hii ni kama vile mazingira ya kihistoria, kijiografia, kijamii, kisiasa na kiuchumi pamoja na hali za kiwakati zilizoakisiwa na wahusika kama ilivyodhihirika kupitia mashairi kadha yanayopatikana katika diwani zilizoteuliwa.

Pili, uainishaji wa wahusika ulifanywa kwa kuzingatia wahusika wanaopatikana katika mashairi teule. Kigezo kilichozingatiwa hapa ni kile cha umbile la mhusika kwani mshairi huathiriwa katika utunzi wake na watu, wanyama na vitu vinavyopatikana katika mazingira yake. Hili lilifanywa katika kila diwani ili

kudhihirisha jinsi kila mshairi alivyozingatia aina mbalimbali za wahusika katika tungo zake.

Tatu, hisia zinazotolewa na mshairi kupitia wahusika wa aina mbalimbali zilifafanuliwa kwa kutolea mifano kutoka kwa diwani zote mbili. Hili lilifanywa kwa *kuzingatia hisia tatu kuu kama zinavyotambuliwa na wanasaikolojia. Hisia hizi* ni mapenzi, hasira na hofu. Hisia hizi zilibainishwa kwa kuzingatia jinsi wahusika wanavyozungumza, kuwaza, kuingiliana na wahusika wengine au kile mshairi anachosema kuwahusu.

Mtafiti alifanya uhakiki wa dhana zilizojitokeza kwa kuongozwa na nadharia iliyoteuliwa. Nadharia hii inasisitiza uteuzi wa aina mbalimbali za wahusika kutokana na maisha ya kawaida, hasa kwa kuzingatia mazingira wanamoishi watunzi. *Hali hizi za kimazingira pia huakisi mabadiliko ya kiwakati* kwani mazingira ya kiutunzi hubadilika jinsi muda unavyobadilika. Pia inazingatia kuwa washairi *huwawasilisha wahusika hawa kwa umbuji wa hali ya juu bila kujali* umbile lao. Hisia za mshairi pia hujitokeza kupitia wahusika wake kwani ndio wawakilishi wa hali halisi anazopitia mtunzi. Mambo haya yalibainika katika kazi zilizoteuliwa kwani watunzi wake wamezaliwa, kukulia na kufanya kazi katika mazingira tofauti. Hisia zao pia zimeathiriwa kwa kiasi kikubwa na hali na matukio waliyoyashuhudia, kuyasikia au hata kuyasoma.

Data iliyokusanywa kutoka kwa kazi nyinginezo muhimu zilizopatikana maktabani ilitumiwa kushadidia yaliyopatikana kwenye diwani teule. Kazi hizi ziliteuliwa kwa misingi kwamba zimeshughulikia kwa kiasi fulani swala la usawiri wa wahusika katika mashairi ya Kiswahili na ushairi kwa jumla, na hivyo kumsaidia mtafiti kubainisha pengo la utafiti na kukadiria kina cha utafiti huu. Ilibainika kuwa kadiri ya ufahamu wa mtafiti, kazi za hapo awali hazikulishughulikia swala la usawiri wa wahusika katika mashairi ya Kiswahili kwa kina kama ulivyofanya utafiti huu.

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maandishi ya kinathari kwa kuzingatia namna usawiri wa wahusika ulivyoendeleza umbuji wa maudhui na dhamira za watunzi.

# SURA YA PILI

# UTEUZI WA WAHUSIKA

## 2.0 Utangulizi

Uteuzi wa wahusika katika kazi yoyote ya fasihi huchangiwa na mambo kadha. Kezilahabi (1976) anasema kuwa washairi wengi wa Kiswahili hujishughulisha na utunzi wa mashairi kufuatana na matatizo au ufunuo uliowafikia wakati huo, au kufuatana na mkondo wa wakati na mabadiliko yake. Hivi ni kumaanisha kwamba mshairi hutunga kwa kuongozwa na mambo yanayotendeka katika jamii yake wakati wa utunzi au mabadiliko yanayoikumba jamii anayoishi. Changamoto zinazowakumba wanajamii kutokana na mabadiliko haya hudhihirishwa kupitia wahusika waliomo katika mashairi ya wakati huo. Mshairi pia anaweza kutabiri mambo yatakayokuja baadaye na hivyo kuyaakisi kupitia wahusika wake.

Kwa mujibu wa Hill (1977) usawiri bora wa wahusika huhitaji hali ya juu ya ubunifu ili kuwafanya wahusika hao wadhihirishe hali halisi zinazopatikana katika mazingira ya kawaida. Anasisitiza kuwa mshairi huwa mfasiri wala si muumbaji kwani hujihusisha zaidi na udhihirishaji wa vivutio ambavyo tayari tunavifahamu, wala sio ufichuaji wa yale tusiyoyazoea wala kuyaona. Hili linadhihirisha kuwa mshairi hawateui wahusika wake kiholela bali huwatumia kuakisi hali ya mazingira kwa mujibu wa wakati.

Kimani (2003) akiwanukuu Wellek na Warren (1949) anakariri kuwa maisha ya mwanafasihi na mazingira yake ya kihistoria, kisiasa, kijamii pamoja na hali za kiuchumi zina uhusiano mkubwa na uandishi wa kazi zake. Hivi ni kumaanisha kuwa mwandishi huathiriwa na tajriba zake za maisha, na hivyo wahusika wanaopatikana katika kazi yake ya kifasihi wanaweza pia kupatikana katika mazingira halisi anayoishi.

Kutokana na maoni haya, tunaweza kusema kuwa uteuzi wa wahusika utategemea mazingira ya mtunzi ya kihistoria, kijiografia, kijamii, kisiasa, na kiuchumi. Hii ni kwa sababu kazi ya fasihi haitoki katika ombwe tupu bali huyasawiri mazingira, matukio na hisia za msanii. Katika sura hii, hali mbalimbali za kimazingira *zinazochangia katika uteuzi wa wahusika katika mashairi ya Kiswahili* zimeangaziwa. Mtafiti pia amejadili mifano ya wahusika katika mashairi teule kutegemea hali hizo za kimazingira, kwa lengo la kuonyesha jinsi washairi mahsusi walivyofanikiwa katika usawiri wa wahusika wao.

## 2.1 Mazingira ya Kihistoria

Kupitia mashairi teule yaliyohakikiwa na mtafiti, imedhihirika kuwa baadhi ya wahusika wamesawiriwa kutokana na mazingira ya kihistoria walimokulia watunzi wake. Mazingira haya yanaweza kuwa yanahusiana na maisha ya kibinafsi ya *mtunzi au historia ya taifa lake.*

Katika **Dafina ya Umalenga,** Mbega (1984) amehifadhi kumbukumbu za maisha yake ya utotoni kupitia shairi liitwalo 'Chuchu' (uk. 34) ambapo anatusimulia juu ya mapenzi yake kwa mamake mzazi alipokuwa mtoto. Kwa mujibu wa Khan na Msami (*1984) katika utangulizi wa diwani hii, lengo la mshairi la* kuyatunga baadhi ya mashairi ni kutukumbusha mambo ambayo huenda tukayasahau.

Mshairi amefaulu kulisawiri chuchu kama mhusika aliyetangamana naye wakati wa utotoni. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema hivi:

> Chuchu nifumbatiapo, sioli nyuma
> Ndipo niifundiapo, kinywa kizima
> Sauti ningurumapo, pasi kusema

Katika shairi hili mshairi amelitumia chuchu kama mhusika wa kimetonumia, ambapo neno hutumika kuwakilisha dhana, mtu au kitu. Hapa chuchu linawakilisha mamake mzazi kama ishara ya mapenzi baina ya mtoto na mamake. Hali hii inathibitishwa katika ubeti wa nne mshairi asemapo:

> Sondoki chuchu ilipo, 'nganisukuma
> Sikomi unambiapo, ya kwamba koma
> Huilinganisha pepo, yenye huruma

Mshairi anatusawiria mtoto anayefaidi mapenzi ya mamake na ambaye hayuko tayari kuondolewa katika hali hii. Si ajabu kwamba anakilinganisha kitendo hiki cha kunyonya na pepo yenye huruma, kwa lengo la kutukumbusha mapenzi makuu tuliyopata tulipokuwa wadogo.

Katika ubeti wa mwisho mshairi anasema kuwa licha ya mapenzi haya huja wakati wa kila mtu kukomaa na kukoma kunyonya. Wakati huu ufikapo mhusika hufanya hivyo bila majuto yoyote wala lawama, kama anavyosisitiza mshairi hapa:

> Mara chuchu nikomapo, nimeshakoma
> Ndipo niiachiapo, nami hasema
> Nakuapia kiapo, sina lawama

Kwa jumla, mshairi anasisitiza hapa kuwa iwapo wakati umefika wa kuliacha jambo au tabia fulani, hatuna budi kufanya hivyo bila kinyongo na kuliacha jambo hilo kuwa historia.

Kupitia shairi liitwalo 'Mlezi' (uk. 38) mshairi anaturejesha pia katika siku za utotoni kwa kutufafanulia umuhimu wa mlezi. Mshairi anatusawiria hali ngumu ambazo humkumba mlezi katika harakati zake za kumshughulikia mtoto anayekua.

Majukumu ya mlezi yanajitokeza vyema kupitia ubeti wa pili mshairi asemapo:

Kulea nako ni kazi, japo i ndani ya nyumba
Mwana awapo mlizi, wakesha kucha kuimba
Akupaza usingizi, wagotea na kuyumba
Ajapokuwa mgumba, ana mashumu mlezi

Mshairi amemteua mlezi kama mhusika kwa lengo la kutukumbusha umuhimu wake kwani sote tulifaidi ulezi tulipokuwa wadogo, na hivyo kuufanya ulezi kuwa sehemu ya historia ya kila mtu. Mshairi anasisitiza kuwa mlezi ni muhimu na anafaa kuheshimiwa hata awapo hajajizalia mtoto.

Shairi hili pia linamkumbusha mlezi mambo aliyoyapitia alipokuwa akiwalea watoto kwa taabu. Katika ubeti wa nne mshairi anasema kuwa mtoto awapo mgonjwa mlezi hatulii bali hujaribu kila aina ya tiba. Anasema:

Mwana akiwa hawezi, mlezi huwa asamba
Ramli hizi na hizi, makombe na mitishamba
Na utanda wa hirizi, na miko ya kila vumba
Ajapokuwa mgumba, ana mashumu mlezi.

Mohamed (2002) katika **Jicho la Ndani** ameathiriwa kwa kiasi kikubwa na matukio ya kihistoria, hasa yaliyo na mtazamo wa kisiasa. Hili linadhihirika kupitia mashairi kama vile 'Mama'angu' (uk. 21), 'Kadhia ya mti' (uk. 34), 'Watendwa jana' (uk. 56) na 'Wingu' (uk. 100).

Katika shairi la 'Mama'ngu', mshairi anairejelea nchi yake iliyopitia hatua kadha za kihistoria zilizoifanya kudharauliwa hata na wageni. Shairi hili limejaa kumbukumbu za kipindi maalum alichoishi nje ya nchi yake, hasa ikizingatiwa

kuwa mshairi alikichapisha kitabu hiki akiwa mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Bayreuth, nchini Ujerumani.

Anailinganisha nchi yake na mamake kwa lengo la kudhihirisha mapenzi yake makuu na uzalendo kwa taifa lake. Katika ubeti wa tatu mshairi anairejelea nchi yake hivi:

Muda umepita
Kimya kimetugubika!
Kimya cha upweke na utengano!
Lakini ulikuwa, ulikuwa na 'mi
na bado umo na 'mi,
ndani ya tafakuri na hisia.
Usidhani sikujali
Usione sikubali
Sijaghuri
Sijahuni
Ningeliwezaje, ewe mama'angu?

Inadhihirika katika ubeti huu kwamba uhusiano kati ya mtoto na mamake ni wa karibu mno. Mtoto atenganapo na mamake kwa muda humtamani sana. Hivi ndivyo mzalendo halisi huhisi awapo ughaibuni kutokana na jinsi aipendavyo na kuitamani nchi yake.

Swala la kihistoria linajitokeza vyema kupitia ubeti wa kumi na nne ambapo mshairi anakariri:

Mzazi mama mama'angu,
waelea katika kina kirefu!

Mara umo shwarini,
kwa majilio ya bahari iliyopoa;
huku tamaa yetu ikiogelea juu yako
na *'si hukimbilia kuigwia!*
Na kabla hatujaishika,
*mara hiyo hudidimia!*
Lini ukweli utasimama juu yako?

Uteuzi wa aina hii ya wahusika aghalabu hutokana na hali ya juu ya ubunifu wa mshairi. Mtunzi hupendelea kuyasawiri matukio kijazanda au kiistiari badala ya usimulizi wa moja kwa moja. Mshairi hapa amewatumia wahusika wa kiistiari, ambapo nchi inachukuliwa kama mama mzazi na wananchi kama wanaye. *Anaulinganisha uhusiano wa karibu uliopo baina ya mtoto na mamake na ule* wa mwananchi mzalendo na nchi yake, hasa baada ya kutengana kwa kipindi fulani.

Shairi la 'Kadhia ya mti' (uk.34) linasimulia juu ya historia ya mataifa ya Kiafrika tangu siku za mwanzo mwanzo baada ya uhuru na ung'ang'aniaji wa rasilimali za taifa uliofuatia. Sawa na shairi tulilotangulia kutazama, wahusika hapa ni wa kijazanda. Mshairi amewatumia wahusika watu, wanyama, mti na sehemu zake *tofauti kutudhihirishia jinsi mazingira* ya kawaida *yanaweza kutumiwa kuwasilishia* ujumbe mahsusi.

Utangamano kati ya wahusika hawa unalinganishwa na ule wa binadamu halisi katika nyakati tofauti za kihistoria. Mshairi anaanza kwa kuusawiri mti mchanga unaovutia machoni kwa kutongoa hivi:

Mti uliposheheni    kwa utomvu wa ujana
Kiale hadi shinani    vyema umeviringana
Na kijani matawini    maua yakipachana

Ulialika wageni mtini kutulizana

Katika ubeti huu, mshairi analirejelea taifa changa la Kiafrika lililopendeza kabla ya kunajisiwa na watu waliojaa tamaa na inda. Beti zinazofuatia zinafafanua jinsi watu hawa walivyong'ang'ania rasilimali zake na kulifilisi taifa hilo. Mshairi anasema:

Punde 'kaanza nuhusi na pupa ziso maana
Wakaanza kuuasi na kuzizusha laana
Wanadamu wasikisi wakaanza kuvutana
Mti wakaufilisi tanzuze katatizana

Mshairi anawalinganisha nduli hawa na nyoka wenye sumu kali waliowaangamiza ndege wasio na hatia. Ndege hapa wanawakilisha watu wa tabaka la chini wasio na uwezo wa kujikomboa kutoka kwa mikono dhalimu ya matajiri. Katika ubeti wa nane mshairi anasema hivi:

Nyoka wenye sumu kali matawini 'kazongana
Wakioteya pahali 'kajificha wametuna
Ndege walipowasili wakapata kuwabana
'Kashamiri ujahili salama haiwa tena

Mshairi ameyasimulia matukio ya kihistoria kupitia wahusika kama vile mti mchanga na wanyama hatari. Ulinganishi wao na binadamu halisi unamsaidia kutolea hisia zake kuhusu swala la ukoloni mamboleo. Kwake mshairi, taifa la Kiafrika lililofilisiwa na viongozi wake ni sawa na mti uliopendeza ulipokuwa mchanga kabla ya kuvamiwa na wanyama hatari walioufanya kukaukia jangwani.

Kupitia shairi liitwalo 'Watendewa jana' (uk. 56) mshairi anadhihirisha jinsi watu waliodhulumiwa hapo awali wamegeuka na kuwa madhalimu. Mshairi anawatumia

wahusika kama vile 'watendewa jana' na 'watenda wa leo' ili kuturejesha nyuma katika historia ya mataifa yetu, ambapo baada ya kuungana pamoja na kuwaondoa wakoloni wakongwe, baadhi ya viongozi wa wakati huu wamewageuka wasio na vyeo na kuwa wakoloni mamboleo. Viongozi wa aina hii ndio mshairi anaita *'watendewa jana' na kushangaa imekuwaje kwamba hao ndio tunaopambana nao* leo. Anaanza kwa kusema hivi:

Watendewa jana ndio watenda wa leo
Waliosonona ndio wasononeshao
Hawajali tena ya jana ya mbali kwao
Imekuwaje?

Mshairi hapa anaonyesha jinsi watu hujisahau haraka punde tu wapatapo madaraka na kuanza kutenda kama viongozi dhalimu waliowaona kuwa wabaya sana. Hawa pia husahau kuwa wanaweza kuondolewa mamlakani jinsi madhalimu waliowatangulia walivyoondolewa. Ndio maana akayasawiri makundi mawili ya *wahusika viongozi, yaani wale waliotangulia na wale waliomo wakati huu ili* kuitolea picha kamili ya uongozi katika vipindi viwili vya kihistoria.

Ubeti wa tatu unaeleza jinsi viongozi wa leo walivyokandamizwa nyakati za kupigania uhuru. Mshairi anashangaa kesho itakuwaje kwani hawa madhalimu, ambao ndio waliotaabishwa hapo awali, wamejisahau kabisa baada ya kuwa mabwana. Anasema hivi:

Mrefu mchana walipoendeshwa mbio
Usiku kuguna kwa huzuni na vilio
Leo ni mabwana kama vile wao sio!
Kesho itakuwaje?



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Udhalimu wa wahusika hawa unaendelezwa katika ubeti wa tano ambapo mshairi anawataja wahusika wanaonyanyaswa. Usawiri wa kundi hili la tatu la wahusika pia unahusiana na historia kwani ndio wale wale waliopigania uhuru na badala ya kunufaishwa na uhuru huu wakapata mateso. Mshairi anashangaa:

Hutesa vijana hata na wazee wao
Kwa kikubwa kina huleta maangamio
Maafa bayana yasiyo na kadirio
Leo imekuwaje?

Usawiri wa aina hii ya wahusika kwa jumla unadhamiriwa kuonyesha taabu na dhiki ambazo wenyeji wa mataifa mengi ya Kiafrika wamepitia chini ya utawala wa kikoloni na wakoloni mamboleo, na jinsi jitihada za kupigania uhuru ziliwafaidi watu wachache tu walio madarakani wakati huu.

Mateso kwa wananchi pia yanaelezwa kupitia shairi liitwalo 'Wingu' (uk.100). Mshairi anarejelea tukio la kihistoria ambapo palizuka wingu la maangamizi lililodhaniwa kuwa lingepita baada ya muda mfupi. Wingu hapa limetumiwa kama mhusika wa kijazanda kuwakilisha kipindi kigumu cha kihistoria ambacho bado kimo kumbukumbuni mwa mshairi. Wingu hili lilileta maangamizi kama anavyofafanua mshairi katika ubeti wa kwanza:

Wingu kama li' masizi lilitanda kote anga
Radi na zake konyezi ziliwaka na kuwanga
Mvua na michirizi na pepo kubwa kupunga
Makubwa maangamizi kila pembe yalifunga
*Je, sasa wingu linapita?*

Mshairi amechagua aina hii ya mhusika kwani kwa kawaida hakuna wingu ambalo hudumu angani milele, liwe la heri au la shari. Wingu hutarajiwa kuondoka baada ya kuyeyuka na mvua kunyesha au likasukumwa na upepo na kwenda kwingineko. Baada ya hapo hubaki historia.

Wingu katika shairi hili haliondoki vivi hivi bali linaacha athari mbovu. Linazua utelezi unaowaangusha watu, pamoja na tope jingi, gharika na matatizo ya usafiri. Kazi pia hazifanyiki tena, hali inayowafanya waja kukosa riziki. Hali hizi ngumu zinaelezwa katika ubeti wa pili na wa tatu ambapo mshairi anasema hivi:

| | |
|---|---|
| Ulijaa utelezi | mno watu 'kaanguka |
| Na tope haziachizi | kila tunapozunguka |
| Mafuriko maenezi | gharika kwetu gharika |
| Ukasita uendezi | maisha yakasitika |

Je, sasa *wingu limepucha*?

| | |
|---|---|
| Mvua i shehenezi | ililala mapaani |
| Ikazima zote kazi | tukabaki tu wandani |
| Riziki haziwekezi | ufanyalo kisirani |
| Kwetu ukawa utwezi | sababu hujui nini |

Je, sasa wingu layoyoma?

Kama inavyosemwa kwamba historia hujirudia, mshairi anashangaa iwapo wingu hili limeondoka na hivyo kwisha maangamizi au bado linajipanga kushambulia tena. Mshairi anamalizia shairi lake kwa kuuliza hivi:

| | |
|---|---|
| Hivi wingu ni pitizi | au 'mebaki kufinga? |
| Limehama ng'ambu hizi | au bado linafunga? |
| 'Mekwisha uangamizi | au tena wajipanga? |

Tumechoka mazingizi na uwongo kutuvunga

Je, sasa wingu limeondoka?

Inaonekana mshairi amechoshwa na ahadi za uongo, kwamba matatizo yanayoikumba jamii yake ni ya muda tu, bali utatuzi wake haufikiwi. Kile kinachoweza kuonekana kama matatizo ya kawaida kimegeuka kuwa swala la kihistoria ambalo linajirudia.

Katika shairi zima tunawapata wahusika wanaoweza kupatikana katika mazingira ya kawaida, na hivyo kumwezesha mshairi kuwasilisha ujumbe wake kwa hali isiyotatiza. Wahusika hao ni kama vile wingu, mvua, upepo na tope. Wengine ni watu, mikizi na vidagaa. Aina hii ya wahusika kwa jumla imeteuliwa kwa lengo la kuelezea matukio ya kihistoria kimafumbo.

**2.2 Mazingira ya Kijiografia**

Baadhi ya mashairi yaliyohakikiwa katika utafiti huu yana wahusika walioteuliwa kutokana na mazingira ya kijiografia. Haya ni mazingira yanayohusiana na vitu na hali halisi zinazomzunguka mshairi kama vile milima, mabonde, mimea, mawe na hali ya hewa. Ni vigumu kwa mshairi yeyote kupuuza haya anapotunga kwani yanadhihirisha yale anayoshuhudia katika maisha yake ya kila siku, na hivyo kuweza kuyatafakari na kuyasawiri katika kazi zake.

Mshairi anaweza kuwatumia wahusika wanaopatikana katika mazingira yake ya kijiografia kufafanulia hisia zake. Kwa mfano, mshairi anaweza kumsifu mpenzi wake kwa kuulinganisha urembo wake na ule wa maua yanayopatikana katika eneo analoishi. Pia anaweza kuyasifia maumbile yake mengine kwa kuyalinganisha na yale ya ndege fulani, mimea au hata milima ya kwao.

Hili ni dhihirisho kuwa washairi huchukua muda kuyachunguza mazingira yao, kuyafurahia na kuyatathmini. Ndiposa kuna mashairi mengi yaliyo na usawiri wa wahusika wa aina hii hata katika maandishi ya kale kama vile **Biblia Takatifu**. Katika mfano ufuataο Mfalme Sulemani anamsifu mpenzi wake kwa kuyarejelea *mazingira yake ya kijiografia anaposema:*

Hua wangu, mafichoni mwa jabali,
Katika sitara za magenge,
Nitazame uso wako, nisikie sauti yako,
Maana sauti yako ni tamu na uso wako mzuri.

Tukamatie mbweha,
Wale mbweha wadogo,
Waiharibuo mizabibu,
Maana mizabibu yetu yachanua.
(Wimbo Ulio Bora 2:14-15)

Katika dondoo hili, mshairi anamwita mpenziwe hua. Huyu ni ndege maridadi sana, sio tu kwa sura bali pia mwendo wake wa hatua za hesabu. Hua anayerejelewa kajificha jabalini pale nchani mwake (magengeni) na mshairi anatamani kuuona uso wake na pia kuisikia sauti yake tamu.

Katika ubeti unaofuatia ambao ni kiitikio, mshairi anawalinganisha maadui wa mapenzi yao na mbweha wanaotaka kuwaharibia mizabibu yao inayochanua. Zingatia kuwa mshairi anaangazia ndege, mawe, wanyama na hata mimea inayopatikana katika mazingira yake. Katika vifungu vingine, mshairi huyu anawataja *wanyama wengine kama vile paa na ayala kuyasifia mapenzi. Hili ni* dhihirisho kuwa mazingira ya kijiografia yanaweza kuchangia pakubwa katika usawiri wa wahusika, hasa wale wa kiistiari.

Katika **Dafina ya Umalenga**, mshairi amelisawiri nazi kama mhusika katika shairi liitwalo 'Nazi' (uk.24). Uchaguzi huu unatokana na mazingira yake ya pwani yaliyo na mmea wa mnazi. Mshairi anamlinganisha mjinga na nazi ambalo hukunwa na tui kukamuliwa bila kumaizi analotendewa. Mazingira yenye minazi yanadhihirika zaidi pale mshairi anapozungumzia mambo mbalimbali yanayofanyiwa mnazi bila utambuzi wake kama vile ugemaji, ukwezi na ufuaji wa nazi. Mengine ni utayarishaji wa vifaa mbalimbali kutokana na fuvu la nazi, kusukwa kwa kuti, kutumiwa katika uezekaji na hatimaye mnazi kukatwa na gogo lake kukaliwa na watu.

Katika ubeti wa kwanza mshairi anaulinganisha ujinga wa mtu na ule wa nazi kwa kusema hivi:

> Mjinga ni nazi, agwae kuliwa
> Akunwe na mbuzi, na kukamuliwa
> Tui ni azizi, taki zikagewa
> Ni kutomaizi, atayotendewa

Ili msomaji ayaelewe vyema mambo yanayozunguziwa hapa, itambidi awe na ujuzi kiasi wa mazingira, sio tu ya mazingira ya kijiografia ya mshairi, bali pia yale ya kijamii ili kuelewa matumizi mbalimbali ya mnazi pamoja na bidhaa zake.

Katika **Jicho la Ndani** shairi kama vile 'Jicho la ndani' (uk.1) linaashiria tajriba kubwa aliyo nayo mshairi kuhusu mazingira yake ya kijiografia. Mshairi anaanza kwa kueleza jinsi hali ya hewa ilivyo. Mbingu zimetulizana kwa weupe unaoashiria ushwari. Wanyama wa aina mbalimbali, wadogo kwa wakubwa wanatangamana kule porini. Wapo wanaoishi kwa amani ilhali wengine wamo vitani. Anayafafanua pia maumbile kama vile milima na mabonde ambamo wanyama hawa wanasakini. Mshairi anaijenga taswira hii:

Tazama ukiiona

milima ya ukingoni

Na bonde lililo pana

na busati la kijani

Na *nyama wan'olishana*

walioko malishoni

Wadogo wal'ojazana

na wakubwa wa pembeni

Wote wamekitamana

kwa upole wa amani

Uwatazamapo sana

wamekutana kwa shani

Kama vile 'mepatana

*na amani 'mesaini*

Ila 'kitunga maana

utaona wa vitani

Mwenye nguvu ambana

dhaifu yu mautini

Simba anafukuzana

na paa yu hatarini

Chui na 'ye atafuna

windo na damu menoni

Na nyati wanapigana

wao kwa wao mbugani

Fisi wanasogezana

mafupa wayatamani

Vumbi linatifukana

mbwamwitu wa mbioni

Tai wanakimbizana

na walao mawindoni

Kishindo kuangushana

ni kanuni ya mwituni

Kanuni hii ya mwituni anayorejelea mshairi haiwezi kung'amuliwa na mtu yeyote asiyeyafahamu vyema mazingira ya porini. Sharti mshairi awe amechukua muda kuwachunguza wanyama wa porini na nyendo zao ili aweze kuwasawiri jinsi alivyofanya. Ndio maana akaweza kuwalinganisha na binadamu kama alivyofanya katika mishororo ifuatayo ya mwisho:

Wanadamu huvotana

bunduki zi mikononi

Amani tena hakuna

'kiona jicho la ndani!

Ili kuweza kuiona migogoro iliyoko baina ya wahusika hawa, sharti mshairi awe amelitumia jicho la nje mwanzo kabla ya kulitumia jicho la ndani kuyafasiri yanayotendeka mle porini. Mshairi amewatumia wahusika wanaotokana na mazingira ya kijiografia kama vile mto, ardhi na mimea kuwakilisha binadamu wa tabaka mbalimbali, tabia zao na jinsi wanavyotangamana. Mshairi amewasawiri wahusika wa tabaka la juu na lile la chini na kuonyesha jinsi binadamu wa tabaka la juu huwatumia wale wa tabaka la chini kujinufaisha. Binadamu wa tabaka la juu wanasawiriwa kama viumbe wasio na utu na ambao hawathamini kamwe hisia za wale walio katika tabaka la chini. Tabia za watu wa tabaka la juu ni kama zile za mto upitao kwa kishindo bila kujali iwapo unaiumiza ardhi au mimea iliyo karibu. Uhusiano kati ya watu wa tabaka hizi mbili ni ule wa kushukiana na kutoaminiana.

Katika shairi liitwalo 'Mto' (uk.105-106) mshairi anayasawiri mazingira ya mkondo wa maji ya mto na kingo zake. Anatumia mbinu ya tashihisi ambapo mto unapewa

Wawapi chiriku | wajuao tumbuiza?
Mramba, kasuku | ndege wan'o miujiza
Mabata na kuku | mno wan'otosheleza
Tausi ashiku | na ninga wan'opendeza
*Hawa mahuluku* | *wote tumewapoteza*
Alo baki huku | kunguru mviza!

Katika shairi hili, mshairi anadhihirisha weledi wake wa mazingira ya kijiografia kwa kuwataja ndege wa aina mbalimbali pamoja na umuhimu wao. Anawasifu chiriku kwa kujua kutumbuiza kwa sauti yake nyororo, mramba na kasuku kwa 'kutenda miujiza' na bata na kuku kwa kutosheleza. Bila shaka miujiza watendayo *chiriku na mramba ni ile ya kuiga sauti za binadamu. Mabata na kuku* nao wanatosheleza kwa kumpa binadamu chakula na mbolea, miongoni mwa manufaa mengine. Mshairi amewatumia wahusika hawa kiistiari kuwakilisha watu wa tabaka la chini lakini muhimu, ambao hudharauliwa na kuangamizwa na wale wa tabaka la juu. Nafasi yao huchukuliwa na binadamu hasidi wasiofaa kwa lolote ila kuzijali nafsi zao.

Mshairi pia anawasifu tausi na ninga kwa kupendeza. Lakini anahuzunika kwa kuwa ndege hao hawapo tena. Aliyebaki ni kunguru asiye na manufaa yoyote kwa binadamu, ila tu kuwaagamiza ndege wadogo. Huyu ndiye ndege mmoja tu mla nyama aliyetajwa katika shairi hili. Wengine wote ni rafikize binadamu wanaojulikana ama kwa kupendeza machoni, sauti zao nzuri au faida zao nyinginezo. *Ni kunguru tu asiyependeza hata kwa sauti yake.*

Wahusika hawa, kama tulivyoshuhudia katika sehemu nyinginezo, wanaweza kulinganishwa na binadamu kwa njia kadha. Ulinganishi huu utatokea tu iwapo mshairi na wasomaji wake watawachunguza kwa makini katika mazingira yao ya kijiografia. Ndege wanaovutia na wasiowaangamiza wengine wametumiwa

uwezo wa kutenda mambo sawa na binadamu na viumbe wengine waliopo. Madhara yanayosababishwa na mto unaoteremka kwa kasi yanafafanuliwa hivi katika ubeti wa tatu na wa nne mtunzi asemapo:

Niliposimama kando kuichunza chemuchemu
Kama mithili ya fundo 'mefunduka timtimu
Mikokoto na mishindo kama vile wendazimu
Ikakazana midundo kwenye mwamba maalumu
Mto, ewe mto kwa'ni hugeuzi njia?

Maji yakawa mtindo yameizonga aridhi
Mimea 'kashika tando ikapatwa na maradhi
Tibutibu na mipindo mto 'kazidisha ghedhi
Kwa kasi kapiga mwendo bila kujali baadhi
*Mto, ewe mto kwa'ni hugeuzi njia?*

Ubeti wa tatu unadhihirisha umuhimu wa kuyachunguza mazingira ya kijiografia kwa makini ili kuwapata wahusika wake kutoka humo. Katika mshororo wa kwanza mshairi anaeleza jinsi alivyosimama kando ya mto na kuitazama chemuchemu kwa jicho la upelelezi. Ni baada ya upelelezi huu ambapo aliutumia ubunifu wa hali ya juu na kuuhuisha mto, akaupa uwezo wa kutekeleza vitendo bila kujali na pia akaweza kuuzungumzia, kama inavyodhihirika katika kibwagizo.

Shairi lingine lililo na wahusika wanaohusiana na mazingira ya kijiografia linaitwa 'Ndege wamekufa' (uk. 110). Hili ni shairi fupi la ubeti mmoja tu lililo na ndege kama wahusika wake. Mshairi anawataja ndege wenye sifa chanya kama vile chiriku, mramba, kasuku, mabata, kuku, tausi na ninga ambao tayari wameangamizwa. Mahali pake pamechukuliwa na kunguru mviza. Mshairi anasema hivi:

kuashiria amani duniani na kufaana miongoni mwa wanajamii. Kunguru naye ni kiwakilishi cha binadamu hasidi asiyewafaa binadamu wenzake kwa lolote, hata maongezi. Lake ni kuwakosesha amani binadamu wasio na hatia kwa kelele zake zisizo na neno la tija.

Mshairi huyu pia amevutiwa na mimea katika mazingira yake. Katika shairi liitwalo 'Mtango' (uk. 130), mshairi anautumia mmea kama mhusika wake. Mtango ni mmea utambaao kama maboga wenye majani mapana, matunda marefu, membamba na yenye mbegu nyingi ambayo huliwa na binadamu. Uteuzi wa mhusika huyu unatokana *na mazingira ya kijiografia yaliyosababishwa na binadamu kupitia* shughuli ya kijamii, yaani kilimo. Mshairi anayafafanua manufaa ya mmea huu unaodharauliwa na matajiri katika ubeti wa kwanza kama ifuatavyo:

Ijapo hawautaki
Mtango na utambae      shehena usheheneke
Na siha nyingi uvae      daima uimarike
Na matawi yasambae      hata yasizuilike
Chakula cha masikini!

Mshairi hausifu tu mmea huu bali pia anauhami dhidi ya matajiri wasioudhamini kamwe. Katika ubeti wa tatu na nne mshairi anasema kuwa mmea huu haufai kamwe kung'olewa bali ubaki pale kiamboni ili uendelee kuwanufaisha maskini. Mshairi hapa anaashiria utengano wa kitabaka uliopo katika jamii. Anawasawiri *matajiri ambao watahiari kukiharibu chochote kinachowanufaisha maskini* - *bora tu* hawakihitaji wao - kwani wamejaa dharau na ubinafsi. Lengo lao ni kuwaangamiza kabisa wachochole. Ndio maana mshairi anawatetea wanyonge kwa kusema kuwa iwapo matajiri hawautaki mtango hawana haja ya kuuharibu bali wawaachie wajuao faida yake. Anasema:

Ijapo hawautaki
Kwenye kiambo ukae kwa mizizi ujishike
Ni kimo chake kikue Mpaka uzagaike
Majaniye yakozee viale mboga tupike
*Chakula cha watambaji!*

Ijapo hawautaki
Zuia wasiung'owe hawajui tija yake
Zuia wasiwondowe kabisa 'sifisidike
Wao ndu' yangu wajuwe wataka tudamirike
Chakula cha makabwela!

Ili kuweza kuusifu mmea huu jinsi alivyofanya mshairi, panahitajika kuwa na weledi wa hali ya kimazingira na jinsi mazingira hayo yanavyomnufaisha binadamu. Ni lazima mshairi awe amezichunguza sehemu mbalimbali za mmea huu na kuyatambua vyema matumizi yake. Pia ameuchunguza vyema jinsi unavyokua na *kutambaa kwa fahari licha ya pingamizi unazopata kutoka kwa matajiri.* Ndiposa anasema hivi katika ubeti wa pili:

Ijapo hawautaki
Kizazi chake kizae ujae ufufurike
Ukue hadi upee na mbolea uchuchuke
Na matango yazagae kila mtu atosheke
*Chakula cha wahitaji!*

Kwa kumalizia, mshairi anasisitiza kuwa mmea huu ni tegemeo la wanyonge na hivyo unafaa kukuzwa kiasi kwamba wasiouenzi hawatakuwa na uwezo tena wa kuuzuia. Anasema hivi:

Na kwamba hawautaki
Kumbuka hilo lijuwe tegemeo hilo peke
Mtango wasiuuwe tulilinde meo lake
Hadi kimo na kikuwe tena usizuilike
*Chakula cha wachochole!*

Ili kuweza kuutambua mmea huu kama tegemeo la pekee la wachochole, sharti mshairi awe ameichunguza mimea mingine inayopatikana katika mazingira yake na kuutambua upekee wa mmea huu. Sharti pia awe ameichunguza kwa makini mimea inayopendwa na matajiri na kuulinganisha umaarufu wake na mmea huu unaotegemewa sana na maskini.

Tunapolichambua shairi kama hili itakuwa vyema tukijiuliza ni nini kilichomvutia mshairi hadi akauzungumzia mmea huu wala si mimea mingine, ilhali mimea ni mingi. Ni vyema pia tujiulize ni kwa nini matajiri wakautweza huku wakiitwaza mimea mingine. Swali lingine muhimu la kujiuliza ni je, tabaka la mtu linahusianaje na mazingira yake ya kijiografia? Je, ni mimea ya aina gani inayopatikana katika mazingira ya watu wa tabaka mbalimbali? Je, watu hawa wanaithamini vipi mimea hii?

Kwa kuyajibu maswali kama haya tutakuwa tumepanua zaidi mawanda ya kuuhakikia ushairi wa Kiswahili.

Usawiri mwingine wa wahusika wanaotokana na mazingira ya kijiografia unajitokeza kupitia shairi liitwalo 'Juu ya mti' (uk. 150-152) ambapo mshairi anasimulia juu ya mazingira ya msituni. Anatusawiria mti mrefu ulionawiri kialeni, ukadhoofu chini na kukonda matawini. Juu yake wanajenga ngome vipanga nke kwa dume na kuwaangamiza ndege wengine pamoja na kuku walioukaribia mti ule. Lakini siku inawadia ambapo kipanga anapukutika kutoka juu ya mti baada ya

kuumwa na nyoka aliyemvizia na kutangaza mwisho wa maisha yake. Mshairi anasema hivi katika beti za kumi, kumi na moja na kumi na mbili kuhusiana na mauti ya kipanga:

Pu! Pu! Kitu 'kajitupa
Chini hicho 'kafusika
Hapo kikatapatapa
Kipanga siku 'mefika

Hima chini kichwa ng'ombe
Ile tadi hana tena
Damu katoka kikombe
Kipanga jeuri hana!

'Kalala amekazana
Nyoka nd'o al'omuuma
Mwili ukababukana
Ikawa yake hatima

Baada ya hayo hali inabadilika ambapo nyoka yule yule aliyemwua kipanga, na hivyo kudhaniwa kuwa kawaondolea ndege hatari ya kuangamia anawageuka na kuwafanya kitoweo chake. Mtunzi anasema hivi kuhusu himaya ya nyoka:

Mti sasa wake yeye
Tamaa ndege katowa
Nyoka, nyoka yeye ndiye
Adui wa ndege kawa!

Hata hivyo, hali hii haidumu milele kwani licha ya kuendelea kwa miaka mingi, siku moja ndege wanaporauka wanashangilia kwa kuruka juu ya mti kwa furaha, wanapowakuta siafu chini ya mti waking'ang'ania maiti ya nyoka yule yule



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

aliyekuwa akiwahangaisha. Ajabu ni kwamba nyoka huyu anatafunwa na siafu, viumbe wadogo na dhaifu kuliko ndege wale aliokuwa akiangamiza! Mshairi anasema hivi:

'liporauka sabahi
Ndege wakashangilia
Juu ya mti walifurahi
Kuruka na kurukia

Hachunza chini ya mti
Siafu 'meng'ang'ania
Nyoka 'meshiba mauti
Vita vimemzidia!

Kamaizi siku hiyo
Kweli kiumbe dhaifu
Awe na jingi kamio
Ana mwisho kisadifu!

Usawiri wa wahusika wa aina hii unadhihirisha kwamba mazingira ya kijiografia yana mengi yanayoweza kutungiwa, bora tu washairi wawe na jicho la udadisi. Katika shairi hili, mshairi amewatumia wahusika ambao ni rahisi kupuuzwa kwani maisha yao huenda yakachukuliwa kama yasiyo na uhusiano wowote na maisha ya binadamu. Maisha ya wahusika kama wadudu, kwa sababu ya udogo wao wa kimaumbile, huenda yasitiliwe maanani. Ni nadra sana kumpata mtu mzima akijishughulisha na maisha 'duni' ya wadudu, hasa kwa lengo la kuwatumia kama wahusika katika utunzi wake. Hata hivyo, tunapoyatilia maanani tunaona kuwa jinsi viumbe hawa wanavyoingiliana ndivyo sisi pia huingiliana katika maisha yetu ya kila siku.

Msomaji anaweza kuijenga taswira ya maisha ya msituni kwani usimulizi wake unamjia kwa njia ya kuvutia badala ya usimulizi 'mkavu' juu ya maisha ya binadamu. Baadaye anaweza kulichambua shairi hili hatua kwa hatua kwa kudadisi maana ya ndani iliyowasilishwa na kila mhusika.

Matumizi ya ndege kama mhusika yanajitokeza pia katika shairi liitwalo 'Ndege na Mwanadamu' (uk. 154). Mshairi anaanza kwa kueleza jinsi ndege mwenye sauti tamu hunaswa kwa ulimbo na mitego na kutiwa tunduni ili kumliwaza bwana. Lakini ndege yule yule hulaumiwa baadaye kwa madai ya kuwa na sauti mbovu inayokera *watukufu wenye ghera na kuwaharibia usingizi. Hatimaye* watukufu hawa wanaamrisha ndege yule awindwe na kuchinjwa kwa madai ya kuharibu usalama kwa sauti yake mbaya. Ndege yule anawindwa kwa bunduki na apatikanapo anaishia chunguni.

Hapa mshairi ameyasawiri mazingira ya kijiografia kwa njia sahili kwa kuzingatia mazingira anayoishi ndege na jinsi yanavyompa faraja binadamu licha ya utovu wake wa shukrani. Mshairi anasema hivi:

Ndege mghani ndege
Sauti nzuri 'kitoa
Mwenyewe itakuponza
Kuitiliza maashiki
Kuja ndege kukunasa
Kwa ulimbo wa mitego
Kisha utiwe tunduni
Kumliwaza bwana!

Katika ubeti huu mshairi anatujengea taswira ya masikizi ambapo tunaweza kuisikia sauti ya kuliwaza ya ndege. Usawiri huu unatokana na hali ya kawaida ya

kimaumbile ambayo ni rahisi kupuuzwa, sawa na maisha ya msituni tuliyotazama hapo juu.

Jinsi ndege huyu anavyodharauliwa mbali inaweza kudhihirika katika ubeti wa pili ambapo mshairi anasema hivi:

Ndege sauti bovu
Sauti hiyo huwakera
Watukufu wenye ghera
"Unaturusha usingizi!"
Kwa *hamasa* watanena
"Muinde, muinde...
Mchinje mchinje...
Sautile baya twaliiza!
Laharibu usalama
Usalama 'tapotea!"

Jinsi ndege huyu anavyowindwa inasikitisha. Tazama kwamba anawindwa kwa bunduki! Hili linadhihirisha jinsi nguvu zilizopita kiasi hutumika dhidi ya wanyonge wasio na uwezo wala nia yoyote ya kujihami. Kwa kawaida ndege huwindwa kwa silaha ghafi kama panda au kombeo au hata kuwanasa kwa ulimbo. Matumizi haya ya bunduki pia yanadhihirisha chuki ya hali ya juu. Nia ya mwindaji huyu ni *kuhakikisha kuwa ndege huyu hana nafasi yoyote ya kunusurika*! *Maana* yake ya ndani ni kuwa matajiri wanaponuia kuwaangamiza maskini hufanya hivyo kwa njia ambayo nafasi ya kunusurika ni haba mno.

Msako unaofanywa ili kumpata ndege anayewindwa unaweza kuonekana vyema akilini. Mshairi anaueleza hivi katika ubeti wa tatu:

Basi utawindwa
Utawindwa ndege
Utawindwa
Tena kwa bunduki
Utawindwa
Na ufumwapo
Utaishia chunguni!

Shughuli hii ya uwindaji pamoja na ndege anayewindwa ni mambo ya kawaida tu. Lakini jinsi uwindaji huu unavyotekelezwa, kinachowindwa na sababu ya kuwindwa vinalipa shairi hili upekee. Usomaji wake unavutia zaidi hasa pale msomaji anapoifuatilia kadhia hii kwa makini ili kuishuhudia hatima ya mhusika huyu tunayetangamana naye kila siku katika mazingira tunayoishi wala tusijishughulishe naye.

Maana ya ndani ya shairi hili inashadidiwa na ubeti wa mwisho mshairi anapousaili ubora anaoweza kutendewa binadamu akashukuru. Mshairi anaeleza hivi:

Sasa niu'ze
"Ubora ni upi?'
Nami 'takujibu
"Ubora ni kuwa,
Mwanadamu DAIMA
Mwanadamu KAMILI!"

Mshairi hapa anadokeza jinsi binadamu daima hujiona bora kuliko wanyama wote wanaopatikana katika mazingira yetu kiasi cha kuwaangamiza jinsi atakavyo, licha ya manufaa waliyo nayo kwake.

Mazingira ya msituni yanajitokeza tena kupitia shairi liitwalo 'Huu msitu' (uk. 155-156). Katika shairi hili mshairi anatujengea taswira kamili ya hali ilivyo mle msituni ambamo mna miti midhaifu na michofu inayoshindania nafasi na ile mirefu, minenefu na miangafu isiyohofu chochote. Katika ubeti wa pili mshairi anaifafanua miti ya *aina ya kwanza kwa kusema hivi:*

Katika huu msitu
Kuna miti iliyodhofu 			is'o na kani
Kuna midhaifu 			'metwama chini
Kuna na michofu 			'loachwa njiani
Kuna mitilifu 			il'o hatarini
Kila kitu huwania juu
			Katika huu msitu

Miti iliyoelezewa hapa ni kinyume kabisa na miti hii iliyofafanuliwa katika ubeti wa tatu ambapo mshairi anasema:

Katika huu msitu
Kuna il'o mirefu 			'meshika kani
Kuna minenefu 			'metamakani
Kuna miangafu 			'nong'ara majani
Kuna is'o hofu 			kwa mengi makini
Kila kitu hugombea juu
			Katika huu msitu

Mshairi pia anatusawiria hali ya kiza kinachotanda mle msituni na kuiangamiza miti ya chini, ilhali ile mirefu na minenefu imo shwari kwa vile vilele vyake vinaufikia mwangaza. Hili ni dhihirisho la ushindani uliokithiri katika maisha ya siku hizi ambapo wenye nguvu huwakandamiza wale wasio na uwezo.

## 2.3 Mazingira ya Kijamii

Mwandishi yeyote hawezi kujiepusha kamwe na maswala ya kijamii yaliyomzunguka anapoitunga kazi yake. Hii ni kwa sababu mwandishi ni mwanajamii na anaathiriwa kwa kiasi kikubwa na mambo yale anayopitia maishani, yale *anayoambiwa, kuyasoma au kuyashuhudia yakiwakumba wanajamii wenzake.* Jambo hili humpa mshawasha na kariha ya kuyatungia maswala ya kijamii yanayompendeza au hata kumchukiza na hivyo kuwatumia wahusika ambao ni viwakilishi vya wanajamii halisi.

Katika **Dafina ya Umalenga** (1984) tunayapata mashairi kadha yanayodhihirisha hali mbalimbali zinazowakumba wanajamii. Hali hizi zinafafanuliwa vyema kupitia wahusika ambao pia wanadhihirisha shughuli mbalimbali za kijamii.

Jamii yoyote ulimwenguni huuthamini sana ulezi wa watoto kwani ndio msingi wa jamii. Mshairi anapoyatunga mashairi yanayohusiana na hali hii hawezi kamwe kujiepusha na usawiri wa wahusika kama vile watoto, wazazi na walezi. Kwa mfano, kupitia shairi liitwalo 'Uhunzi' (uk.32), mshairi anaulinganisha ulezi na uhunzi kwa kuwatumia wahusika wanaopatikana katika shughuli zote mbili, yaani watoto, *walezi na wahunzi. Maudhui ya ulezi yanamzunguka mtoto na hivyo* kumfanya kuwa mhusika mkuu katika shairi hili. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema hivi:

> Mwana mchanga hulewa, tangu akali mkembe
> Hulewa kupembejewa, maovu yasimkumbe
> Huku akiongolewa, kwa viziwa tembetembe
> Uhunzi si wa vijembe, na tabia hufuliwa.

Katika ubeti huu, mshairi anayasimulia mahitaji ya ulezi tangu mtoto akiwa mdogo, ambapo hubembelezwa na kukingwa kwa maovu ya kila aina, huku akiongolewa kwa maziwa ili atulie. Hili ni dhihirisho kuwa jamii humchukulia mtoto kama

mhusika muhimu, ambaye huchukua sehemu kubwa katika shughuli za jamii husika, kwa lengo la kukiendeleza kizazi kilicho na afya nzuri.

Isitoshe, mtoto anapoendelea kukua mahitaji ya ulezi huzidi kuongezeka ambapo mafunzo ya maadili hufuatia. Mafunzo hayo huanza taratibu kwa mtoto kukanywa asije akawa mzembe au kuwa na tabia mbaya zisizomfaa kiumbe. Hili linaelezwa katika ubeti wa pili mtunzi asemapo:

Muda a'nzapo kukuwa, hufunzwa uchembechembe
Lisofaa akemewa, 'sije akawa mzembe
Tabiambi k'ondolewa, zisomfana kiumbe
Uhunzi si wa majembe, na tabia hufuliwa

Katika ubeti huu, mshairi amemtumia mtoto kama mhusika ili kuendeleza maadili ya kijamii kupitia ushairi. Mshairi amedhamiria kuonyesha umuhimu wa kuwa na jamii inayoweza kujitegemea na pia yenye nidhamu kupitia mafunzo yanayoendelezwa tangu utotoni.

Ili kudhihirisha uzito unaotiliwa katika malezi, mshairi katika ubeti wa tatu anazilinganisha tabia za mtoto ambaye hakulelewa vizuri na zile za ng'ombe. Neno ng'ombe hutumika sana katika fasihi kama kejeli au bezo na aghalabu huashiria ujinga na kutokuwa na tahadhari. Katika muktadha huu, ng'ombe ni mhusika wa *kitashbihi kwa kuwa mtoto analinganishwa na ng'ombe kwa kutumia kilinganishi* 'ja'. Ni wazi kwamba mtoto asiye na nidhamu hajihadhari anapofanya jambo lolote. Matokeo yake ni kuwa haongokewi na pia hudharauliwa na wanajamii. Mshairi anasema hivi:

Na tabia hufuliwa, zisifanane na ng'ombe
Kwepushwa kubeuliwa, ja ng'ombe asiye pembe
Akuwe kuongokewa, akaapo awe jumbe

Uhunzi si wa majembe, na tabia hufuliwa

Ulinganishi mwafaka wa mlezi na mhunzi unajitokeza vyema katika beti za tano na sita, ambapo mshairi anatoa mfano wa jinsi kazi hizi mbili humshughulisha azitendaye. Ubeti wa tano unaeleza jinsi mhunzi hujitahidi na kuifua chuma hadi ikawa tayari kwa kuundia vifaa mbalimbali. Nao ubeti wa sita unaeleza jinsi mlezi hujikaza katika ulezi kwa kunyoosha tabia za mtoto hadi anapokuwa laini kimaadili, bila kujali wanachosema watu. Mshairi anasema hivi:

Msani huvugutiwa, mifuo shuti ivimbe
Na chuma kuchocholewa, kikaiva ombeombe
Hadi kikisha kolewa, hufua sime na vyembe
Uhunzi si wa majembe, na tabia hufuliwa

Na kiumbe vivyo sawa, mlezi na amtimbe
Timbwa ya kubobodowa, zilo njema zimpambe
Asisikize kwambiwa, lilumbwalo asilumbe
Uhunzi si wa majembe, na tabia hufuliwa

Ulinganishi huu ni ishara tosha kwamba mshairi anaielewa fika jamii yake, na hivyo kuweza kuyalinganisha majukumu yanayotekelezwa na wahusika mbalimbali bila kukosea. Ili afanye hivi ipasavyo, sharti mshairi awe amezichunguza kazi zote mbili kikamilifu na kuhitimisha kuwa kuna mahali zinapolingana licha ya kutumia 'vifaa' tofauti. Katika uhunzi kifaa kikuu ni chuma ilhali katika ulezi kifaa kikuu ni mtoto.

Kupitia shairi liitwalo 'Peku' (uk. 14) mshairi anavitaja vifaa viwili (peku na ungo) ambavyo hutumiwa katika kupepeta nafaka, ambazo ni shughuli za kijamii. Uteuzi huu wa wahusika unatokana na kazi zifanywazo na wenyeji wa pwani alikozaliwa na kukulia.Ungo ni kifaa kipya na bora zaidi kinapolinganishwa na peku ambacho ni

kifaa kikuukuu. Hata hivyo, vifaa hivi viwili vinalingana kwa kuwa vinatengenezwa kwa chane za miale kutokana na shughuli ya usukaji inayotekelezwa na wapwani. Ungo likishachakaa huwa si ungo tena bali huitwa peku.

Mshairi anatumia tashihisi katika shairi zima ambapo peku linaongea na ungo. Katika ubeti wa kwanza mshairi anaanza kwa kusema hivi:

Niliko ndiko ujako, peku lamwambia ungo
Sinyetee upya wako, kuwekwa juu ya vyango
Likakupa danganyiko, binadamu waongo
Peku lamwambia ungo, niliko ndiko ujako

Katika shairi hili mshairi amevitumia vifaa hivi kuwakilisha mabadiliko wanayopitia wanajamii kama vile kuzeeka, kwa njia ya ubunifu. Anawatahadharisha walimwengu dhidi ya kujiinua kwa sababu ya ujana kwani siku moja watakuja kuzeeka na kuwekwa kando sawa na peku.

Onyo analolitoa mshairi linatokea vyema zaidi katika ubeti wa pili na wa tatu, ambapo peku linalisimulia ungo jinsi lilivyotengezwa na fundi na kutiwa nakshi. Kisha lilipelekwa sokoni ambako lilichaguliwa na wanunuzi kwa hamu kuu. Baada ya matumizi ya muda mrefu hadi kuchakaa, liliangikwa palipo na moshi na mlale. Katika ubeti wa pili mshairi anasema:

Huko nilikokuwako, kwa fundi mfanya nyungo
Kanileta kwenye soko, na wenzangu mlolongo
Ikashuka kokokoko, uchaguzi kwa mpango
Peku lamwambia ungo, niliko ndiko ujako

Ubeti wa tatu unafafanua yaliyolipata peku, ambalo hapo awali lilijivunia kuwa ungo pale mshairi asemapo:

Nisiwe nalo sumbuko, kwa masiku na miongo
Ni juu ya viangiko, penye moshi wa kaango
*Haiva mnyinyiriko, mweusi kama mpingo*
Peku lamwambia ungo, niliko ndiko ujako

Katika beti hizi tunashuhudia hali halisi ya kijamii, ambapo chombo kipya huthaminiwa kuliko kile kilichochakaa. Hii inatokana na hali ya kimaumbile ambapo kwa kawaida binadamu huvutiwa zaidi na kitu kilicho na sura au sifa zozote nzuri kuliko kile kilichopoteza sifa hizi. Ndiposa mwandishi akatusawiria hali hii *kwani inaweza kung'amulika kwa urahisi hasa iwapo msomaji anazielewa shughuli* za wanajamii waliorejelewa, vyombo watumiavyo na utamaduni wao kwa jumla.

Shairi la 'Mnazi' (uk.24) tulilorejelea katika sehemu ya mazingira ya kijiografia pia linadhihirisha hali fulani za kijamii. Mshairi anazitaja shughuli mbalimbali zinazohusiana na mnazi pamoja na mazao yake na kudhihirisha jinsi wapwani huuthamini mmea huu. Kwa kuwa mshairi ameyatungia mashairi yake katika *mazingira ya pwani, ni wazi kwamba anaielewa jamii hii* vyema na hivyo kudhihirisha shughuli za jamii yake katika shairi hili.

Kutokana na tajriba hii ya kijamii, mshairi ameweza kumlinganisha mwanajamii mjinga na mnazi pamoja na sehemu zake kadha zisizoweza kutambua zinapodhulumiwa. Ndiposa mshairi akasema hivi katika ubeti wa tatu:

Mjinga ni nazi, asiyejijuwa
Kamba ya mkwezi, nikumbile fuwa
Huchongwa na ngazi, ukenda gemewa
Na kowa fungizi, kuwa kufungiwa.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Katika ubeti huu mshairi anatoa mifano ya mambo ambayo nazi hufanyiwa, kama vile kufungwa kamba na mkwezi na kuchongwa ngazi ili mkwezi akwee kwa urahisi anapokwenda kugema. Taswira hii inamjia msomaji kwa urahisi iwapo anaielewa shughuli ya ukwezi na ugemaji inayotekelezwa na wapwani.

Shughuli nyingine zinazonasibishwa na nazi na ambazo mshairi anazitaja ni kama vile ukunaji nazi, ukamuaji na utumiaji wa tui (ubeti wa kwanza). Katika ubeti wa pili mshairi anaitaja shughuli ya ukwezi, ambapo mtu hupanda juu ya mnazi ili kuziangua nazi kwa matumizi mbalimbali.

Matumizi ya mnazi na sehemu zake mbalimbali yanafafanuliwa kuanzia ubeti wa tano. Baadhi ya matumizi yaliyotajwa ni kama vile utengenezaji wa tembo, uchongwaji wa fuvu ili kuundia vifaa mbalimbali na uvimbaji wa nyumba kwa makuti yake. Licha ya wema wote huo, makuti yaliyosalia hukumbwa na balaa ya kuchomwa. Hatimaye mnazi hukatiwa shinani na gogo lake kukaliwa.

Kwa kuzingatia shughuli hizi za kijamii, mwandishi amefaulu kuutumia mnazi kama mhusika anayetangamana na binadamu, sio tu katika matumizi yake bali pia kama mhusika asiye na uwezo wa kujitetea, na hivyo kufaa sana katika ulinganishi wake na mjinga.

Swala la ushirikina linajitokeza katika shairi liitwalo 'Mpewa sumu hafile' (uk.28-29) mshairi anapowasawiri wahusika wawili wanaotokana na uhasama miongoni mwa wanajamii. 'Mpewa sumu' ni mhusika anayehujumiwa na 'mwenye kupika' lakini hujuma hii inamdhuru mwenye kupika kwani mkusudiwa hana hatia yoyote.

Uteuzi wa wahusika hawa unatokana na tajriba ya mshairi aliyezaliwa na kukulia katika jamii ya Waswahili ambamo imani ya uchawi hujitokeza sana. Si ajabu mshairi anasema hivi katika ubeti wa kwanza:

Pulikizani wapule, Shuara nikitamka
Msambe napiga kele, kudhani nina mzuka
Vuani mato muole, miuja iliyotuka
Mpewa sumu hafile, afile mwenye kupika.

Mshairi ambaye hujulikana kwa lakabu la Shuara anaanza kwa kuwaomba wasikilizaji wake wategee masikio kumsikia akitamka. Anawaambia wasije wakampuuza kwani hana wazimu wala hapigi kelele bure. Anawataka watazame kwa makini wayaone maajabu au miujiza iliyotokea, ambapo atiliwaye sumu hafi bali afaye ni anayeitengeza.

Utangulizi huu unaashiria kwamba mshairi hatungi vivi hivi, bali huanza kwa kuwachunguza binadamu halisi pamoja na matangamano yao na kuwatumia kama wahusika katika utunzi wake. Migogoro inayozuka miongoni mwa wanajamii inasaidia zaidi katika kuwajenga wahusika wanaoashiria asili ya migogoro hiyo, athari zake na utatuzi wake. Hali hii inaweza kuthibitishwa kupitia maelezo anayotoa mshairi katika ubeti wa nne:

Na kisa'che ni utole, na kwina kutotosheka
Mtaka'che na cha yule, kwa twaana na mashaka
Vunju likajaa tele, lisiweze takasika
Mpewa sumu hafile, afile mwenye kupika.

Asili ya ugomvi huu inafafanuliwa katika mshororo wa kwanza ambapo mshairi anasema kuwa kilichosababisha haya yote ni wivu na tamaa. Katika mshororo wa pili mshairi anasema kuwa mtu mmoja hakuridhika na kilicho chake bali alikitaka cha mwenzie kwa fujo. Matokeo yake yanapatikana katika mshororo wa tatu ambapo mshairi anasema kuwa mzozo huu ulizidi kiasi cha kutotatulika.

Katika beti zinazofuatia, mshairi anaendelea kuufafanua ugomvi huu. Yaelekea mgogoro huu ulianza zamani kwani katika ubeti wa tano mshairi anaeleza kuwa uchu huu ni wa tangu kale. Mshairi anafichua hivi:

Uchu ni wa tangu ule, ule wa myaka na myaka
Si wa leo ni wa kale, kale zisohisabika
Leo kauchocha ndole, wambaje! Atabubuka?
Mpewa sumu hafile, afile mwenye kupika.

Ubeti huu unadhihirisha kuwa ili mshairi aweze kuwasawiri wahusika wake kikamilifu pana haja ya kutafiti juu ya mizozo inayowakumba. Pana haja ya kuirejelea asili ya mizozo hii, kufuatilia jinsi inavyoendelea kujengeka na matokeo yake. Hili litasaidia katika kuwasawiri wahusika waliojengeka kikamilifu na hivyo kuzitolea hisia za mshairi vyema kuhusiana na swala analolitungia. Ndiposa kufikia mwisho wa shairi hili mshairi anaeleza kuwa licha ya kuliwa njama ya kutiliwa sumu, aliyepangiwa hayo hakudhurika bali aliyeyapanga ndiye aliyedhurika.

Shairi liitwalo 'Mwosha' (uk.43) linagusia imani ya dini ya Kiislamu ambapo maiti huoshwa kabla ya kuzikwa. Mshairi anadokeza kuwa ijapokuwa mwosha ndiye huziosha maiti, siku itatimia ambapo yeye pia atakuwa maiti na hivyo kuoshwa. Mshairi anatanguliza shairi lake kwa maneno haya:

Sikuye itimiapo, mwosha naye ataoshwa
Pale watu aoshapo, na yeye atanyooshwa
Atalazwa papo hapo, penginewe hatapishwa
Mwosha naye ataoshwa, sikuye itimiapo.

Kwa mujibu wa Khan na Msami (1984) katika utangulizi wa **Dafina ya Umalenga**, mshairi ameathiriwa na mafunzo ya kidini aliyoyapata kutoka kwa walimu wake katika sehemu za Vanga. Pia amezisoma tungo za washairi wa kale kama vile Muyaka bin Haji (1776-1840), Mwalimu Sikujua (1810-1889), Ali Koti (1776-1834) *na Mwengo bin Athmani (1728-1800) ambao walikuwa mashekhe.*

Makuzi haya bila shaka ndiyo yaliyochangia uchaguzi wa wahusika hawa wanaohusiana moja kwa moja na imani ya kidini ya mshairi, ambalo ni swala la kijamii. Ni kupitia utangamano na hali mbalimbali za maisha ambapo mshairi ameyafahamu mengi kuhusiana na dini yake, na hivyo kuweza kuyalinganisha na matukio mengine maishani. Hali hii inajitokeza vyema katika ubeti wa pili mshairi *asemapo:*

Hakuna liso malipo, kukopwa na kukopeshwa
Na hilo ni tangu hapo, silo kwambwa limezushwa
Mwosha pale utendapo, jifahamu wakumbushwa
Mwosha naye ataoshwa, sikuye itimiapo

Katika ubeti huu, mwosha analinganishwa na mkopa na mkopeshaji ambapo hatima yake ni kulipa. Mshairi anasema kuwa hali hii imekuwapo tangu kale wala si uzushi kwani hakuna jambo duniani lisilo na malipo, liwe jema au bovu. Ndiposa mshairi anasisitiza katika ubeti wa tano kuwa baada ya mwosha kuwa mwoshwa kile *kilichokuwa chake, na hivyo kumtia kiburi kitatwaliwa na kukabidhiwa walio hai.* Mshairi anatoa kauli hii:

Vilivyomtia tepo, vitakuwa vyahamishwa
Na amri kuwa papo, pasiwe cha kubakishwa
Vitwaliwe vilivyopo, na watu kukabidhishwa
Mwosha naye ataoshwa, sikuye itimiapo

Mshairi anamalizia kwa kusema kuwa hata wale waoshaji wa kukodishwa waliokuwa wakibishiwa hodi kutokana na umaarufu wao wameshaoshwa. Hili ni onyo kwa waoshaji wengine wenye kiburi kuwa wao pia wataoshwa na kutoweka wasikumbukwe tena. Katika ubeti wa mwisho mshairi anasema hivi:

> Wangapi walokuwapo, woshaji wa kukodishwa
> Kwa kila siku kuchapo, wabishiwa kuamshwa
> Wawapi? Mbona hawapo, hawapo wamesafishwa
> Mwosha naye ataoshwa, sikuye itimiapo.

Katika shairi hili, mwosha na mwoshwa wametumiwa kama wahusika wa kiistiari kuwakilisha watu wanaojiona kama watadumu milele. Onyo analotoa mshairi ni kwamba yale tunayowatendea wenzetu tuwapo na uwezo fulani tutatendewa yayo hayo tutakapoukosa uwezo huo na wengine kuchukua mahali petu.

Hali nyingine ya kijamii iliyoathiri uteuzi wa wahusika katika utunzi wa Mbega (1984) ni ile ya uchumba na ndoa. 'Si wamwe' (uk.64-65) ni shairi lililo na wahusika wa kike walio na tabia zinazotofautiana kwa hali mbalimbali. Mshairi anadhihirisha tajriba kubwa aliyo nayo kutokana na kusafiri kwingi anapowataja wanawake wa *maeneo mbalimbali katika ubeti wa tatu asemapo:*

> Sambe walio Unguja, hata Jomvu na Changamwe
> Bagamoyo na Mkwaja, wa Kilwa na Kitungamwe
> Sianie hela ngoja, uole yao mashemwe
> Wangawa ni kundi moja, lakini wake si wamwe.

Hapa mshairi anadhihirisha umuhimu wa kuyaelewa vyema mazingira ya kijamii ili mtunzi anapowasawiri wahusika watokanao na jamii mbalimbali asibambanye tu. Ujumbe huu unashadidiwa katika ubeti wa nne, ambapo mshairi anawashauri



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

wanaume juu ya umuhimu wa kuwapeleleza wanawake vilivyo wawapo na haja ya mke ili wasiudhike baada ya kufanya uchaguzi usiofaa. Mshairi anasisitiza:

> Kwamba ukiwa na haja, peleleza usikimwe
> Jifanye babu Mjaja, kila pahala utumwe
> Wenende huku ukija, uone kumwe na kumwe
> Wangawa ni kundi moja, lakini wake si wamwe.

Licha ya tahadhari hii kuhusu wanawake, mshairi anaonekana kuwaelewa vyema wanaume kwani katika ubeti wa pili anadokeza kuwa wanaume pia wana dosari zao.

> Waume siwo wamoja, na wake nao si wamwe
> Wengine wao mafuja, si wake ni wake simwe
> Wana chungu ya miuja, wala lao lisisemwe
> Wangawa ni kundi moja, lakini wake si wamwe.

Ulinganishi huu unathibitisha umuhimu wa kuwaelewa wanajamii na tabia zao ili kuwatumia ipasavyo kama wahusika katika ushairi. Pana haja ya kuchunguza taasisi za kijamii kama vile ndoa ili kuweza kuzisifu au kuzikosoa kupitia usawiri bora wa wahusika.

Hali kama hii pia inajitokeza katika shairi liitwalo 'Uke wenza' (uk.69) ambapo mshairi anawatumia wake wenza kama wahusika. Hili linatokana na jamii aliyokulia mshairi ambapo mwanamume anakubaliwa kuoa zaidi ya mke mmoja. Licha ya kukubalika huku, mshairi ameichunguza jamii yake na kushuhudia visa vya ugomvi kati ya wake wenza.

Mshairi ametumia nafsi ya kwanza kwa kujisawiri kama mhusika anayelalamikia ugomvi kati ya wakeze wawili. Inaonekana kuwa mhusika huyu amewachunguza

wakeze kwa muda kabla ya kulalamika. Ndiposa katika ubeti wa kwanza anashangaa iwapo kuna jambo lingine linalowafanya kugombana mbali na kile awapacho. Anaanza kwa rai zifuatazo:

> Hebu leo nambiani, wala pasi na kificho
> Nijuwe ni kitu gani, nitambuwe mtakacho
> Mna kingine nyoyoni, au kile niwapacho?
> Ni kipi mgombeacho, wake wawili nyumbani?

Imebainika kuwa mhusika huyu anawatunza wakeze vyema kutokana na jinsi anavyojitetea katika beti zinazofuatia. Katika ubeti wa pili anashangaa ni kipi awanyimacho kinachowafanya kuwa na undani. Kuanzia ubeti wa tatu anatoa mifano ya mambo mazuri awafanyiayo bila kuwabagua. Anasema kuwa anawatosheleza kwa chakula na mavazi na hata anapowanunulia vifaa vya urembo huwachagulia vilivyo bora kabisa na kuwakabidhi hadharani.

Kuanzia ubeti wa tisa, mume huyu anasema kuwa wanaishi pale kwa raha wala yeye hawaudhi kwa lolote. Hapa anawaingiza wahusika wengine ambao ni majirani kwa kuhisi kuwa ndio wanaowachongea wakeze na kuwashauri wajiepushe nao. Usawiri wa kundi hili jipya la wahusika unatokana na hali ya kijamii ambapo majirani huchangia pakubwa jinsi watu wanavyotangamana pale nyumbani. Huu ni ukweli wa kijamii ambao hatuwezi kamwe kuukwepa.

Kufikia mwisho wa shairi, mshairi anatufichulia sababu kuu ya ugomvi huu. Mume anahisi kuwa ugomvi kati ya wakeze unasababishwa na wivu na hivyo kuwashauri waupunguze.

Usawiri wa wahusika hawa kwa jumla unatokana na uhalisia wa kijamii ambapo mzozo unaojadiliwa hutokea katika ndoa. Kwa hivyo wahusika hawa, matendo yao

na hisia zao ni rahisi kuaminika kwani ni viwakilishi halisi vya wanajamii na maisha yao ya kila siku.

Wahusika wa aina hii pia wanapatikana katika shairi liitwalo 'Ni heri mke muole' (uk.67-68). Shairi hili linazungumzia unyumba uliojaa kelele, maringo na uzinifu. Mke mchanga anayezungumziwa hatulii nyumbani kwani daima yu mbioni akijifaragua na wanaume wengine. Hali hii inaelezewa bayana katika ubeti wa tano *mshairi alalamikapo:*

Kutwa ni huyu na yule, wajao kumchukuwa
Umkanyapo na lile, papo izuke daawa
Na kesho pia yayale, si kwamba yatapunguwa
Ni kheri mke mule, kama wanawali hawa.

Mhusika mwingine anayetajwa hapa ni mume aliye taabani. Licha ya kujaribu kumkanya mkewe dhidi ya utovu huu wa maadili, mke huyu hajali kamwe. Ubeti wa sita unafichua jinsi mke huyu hujishaua mbele ya waume wa kando. Mshairi anaeleza:

Na *ukumbini pa tele, kama waloarifiwa*
Kwakwa na vigelegele, pashinda paloolewa
Kabisa hapa'sumile, madhali amechachawa
Ni kheri mke muole, kama wanawali hawa

Waume hawa wa kando ni wahusika wengine ambao mshairi anawaingiza ili kuonyesha kuwa kuharibika huku kwa wake pia kunachangiwa na wanaume watoro.

Wahusika wengine wanaojitokeza ni wazazi. Hawa wanaonekana wakimuunga mkono mke huyu mtoro baada ya mumewe kulalamikia tabia zake. Kuanzia ubeti wa saba mshairi anaeleza jinsi mume huyu anavyoandaliwa kikao cha kumuumbua. Ubeti wa nane unaeleza jinsi wazazi wanavyomkemea maskini mume huyu:

Watakujia wavyele, na jamvi kutandikiwa
Kisha wambiwe kefule, huyu hukumnunuwa
Tulijuwa tangu kale, lakini tulighumiwa
Ni kheri mke muole, kama wanawali hawa.

Baadhi ya mambo wanayotaja wazazi hawa katika beti zinazofuatia ni kuwa mwanao ametiwa ugonjwa kwa kusumbuliwa na mumewe na kwamba waja kumchukua. Kisha wazazi hawa wanayaficha makosa ya binti yao ili wapate kumtoza mumewe ada kwa kisingizio cha kumsumbua mwanao. Hatimaye mke *huyu anafanywa kumtawala mumewe kutokana na msimamo wanaouchukua wazazi* wake.

Mshairi anamlinganisha mke wa aina hii na mke mkuu aliyeolewa na kutulia kwake. Mhusika huyu anasifiwa kwa kuvijua vipengele vya ndoa vifaavyo kufichwa na kufichuliwa na hivyo kujichungia heshima. Tazama jinsi mhusika huyu anavyosawiriwa katika ubeti wa kumi na moja:

Ni kheri mke muole, wa kwachwa na kuolewa
Avijuwa vipengele, kuficha na kufichuwa
Litajisiri jambole, ajichungie muruwa
Ni kheri mke muole, kama wanawali hawa.

Wahusika wote katika shairi hili, kama tulivyoona katika shairi lililopita, wana uhalisia mkubwa kwani wanadhihirisha jinsi jamii zetu zilivyo siku hizi. Swala la kutoaminiana katika ndoa ni nyeti mno, hasa siku hizi ambapo wake kwa waume wanajimudu kiuchumi na hivyo kuhisi kuwa wanaweza kujiendeshea maisha watakavyo.

Mohamed (2002) katika **Jicho la Ndani** pia amezingatia mazingira ya kijamii katika usawiri wake wa wahusika. Shairi lake liitwalo 'Watoto pacha' (uk.36) ni dhihirisho kuwa tabia za wanajamii zinaweza kumwongoza mshairi katika uteuzi wa wahusika wake.

Katika shairi hili, mwandishi amewasawiri watoto pacha wanaolingana kwa mengi, tangu kuzaliwa kwao hadi utu uzima. Anawalinganisha watoto hawa na haki na amani, ambayo pia ni maswala ya kijamii. Ubeti wake wa pili unasema hivi:

Mfukuze haki mweke ghaibuni
Useme hutaki kumwona machoni
Amani hafiki labuda tufani
Ni watoto pacha haki na amani.

Usawiri huu una misingi ya kijamii kwani watoto pacha hawabandukani kutokana na uhusiano wao wa karibu unaoanzia tangu mimba itungwapo. Watoto hawa hawalingani kwa sura tu, bali kwa tabia. Huwa wanapendana kiasi kwamba unapomtenga mmoja, mwenzake atamtafuta kwa udi na uvumba hata awe mbali kiasi gani. Tazama jinsi mshairi anavyoueleza uhusiano huu katika ubeti wa kwanza:

Mmoja 'kiwepo hapatamakani
Mwengine endapo hawi ye'makini
Pindipo alipo mwenzi hamuoni
Ni watoto pacha haki na amani!

Ujumbe huu huu unaendelezwa katika ubeti wa tano ambapo mshairi anasisitiza kuwa iwapo utaiondoa haki usitarajie amani ila vurugu. Anailinganisha hali hii na uavyaji wa mtoto mmoja kati ya pacha huku ukitarajia kumpata mwenzake salama. Mshairi anatoa kauli hii:

Umfiche haki utaraji nini?
Kumwavya hutaki wataka amani
Amani hafiki ila hamkani
Ni watoto pacha haki na amani!

Ulinganishi huu wa haki na amani ni dhihirisho kuwa mshairi ameweza kuyatafsiri vyema mazingira yake ya kimaumbile na kuyalinganisha na hali na matukio mbalimbali ya kila siku. Ndiposa kufikia mwisho wa shairi anawashauri wanaohubiri amani kuwa iwapo wanataka pawepo na amani lazima kila mtu atendewe haki. *Mshairi anasisitiza:*

Enyi wahubiri hilo tambueni
Nawapa habari izingatieni
Kwenu si vizuri haki kuihini
Ni watoto pacha haki na amani!

Watoto wametumiwa kama wahusika pia katika shairi liitwalo 'Watoto wanaopendwa!'(uk.57) ambapo mshairi amezichunguza tabaka mbili za wanajamii. Lipo tabaka la wale anaowaita watoto wanaopendwa na lile la watoto wasiopendwa. Uteuzi huu unatokana na hali ya kitabaka inayojitokeza tatika takribani jamii zote ulimwenguni. Mshairi anayafafanua mazingira mema na mabaya yaliyowazunguka watoto wa tabaka zote mbili, tangu kutunga kwa mimba. Kuhusu watoto wanaopendwa, mshairi anasema hivi katika ubeti wa kwanza:

Watoto wanaopendwa
Ujaji wao hulindwa
Mimba zao zikitunga
Kila kitu kitatendwa
Kabla hata kuzawa…

Katika ubeti huu mshairi anaonyesha jinsi watoto wanaozaliwa katika jamii za kitajiri hupangiwa vyema hata kabla hawajazaliwa, walikinganishwa na wale wanaozaliwa katika jamii za kimaskini. Mazingira yanayowakabili watoto wasiopendwa tangu kutungwa mimbani ni ya kuhuzunisha. Mshairi anayafafanua *kama ifuatavyo kuanzia ubeti wa 14 hadi wa 16*:

Watoto wa watu
Si sisi mijitu
Tus'o ulinzi kitu

Sisi tusiopendwa
Mama zetu hutiwa mimba
Pasi na kujua
Mababa wanaporudi kujilewea

Ndipo mimba kwa kisirani huingia
Bila hata mama kuwa na hisia!
Na hata wangekuwa ni mamoja
Kubeba jiwe na kiumbe!
Wangefanyaje, makapi ya muwa?
Roho huruma zina
Roho amani zinaona
Roho mapenzi 'mejaa
Yote lakini yanadidimia!

Mshairi hapa hakuwazingatia wahusika watoto pekee bali amewaangazia wahusika wengine wanaoshiriki katika uzazi. Wazazi wa watoto wanaopendwa huupangia vyema uzazi ilhali wale wa watoto wasiopendwa huwapata watoto kisadfa! Isitoshe, mshairi ameufafanua uraibu wote wanaoupitia watoto wanaopendwa kama vile

kushonewa viguo, kufuliwa vikuku, vinjuga na vipuli vya dhahabu (ubeti wa pili). Hao pia wataundiwa vitanda vya pembea, kuvishwa nguo za kuwazuia baridi na uchafu (ubeti wa tatu) na pia kulishwa vyema miongoni mwa mazuri mengi.

Kuanzia ubeti wa saba mshairi anaeleza jinsi watoto wanaopendwa hushughulikiwa kabla na baada ya kuzaliwa. Wao huzaliwa hospitalini na kutunzwa na wakunga vilivyo huku baba akisubiri nje kwa shauku. Mtoto anayezaliwa hupokelewa kwa furaha bila kujali iwapo ni wa kike au wa kiume, mradi anayependwa keshazaliwa! Baadaye hutunzwa kwa makini na kila wawapo wanyamavu au kulia huitiwa daktari. Maisha yao hujaa raha.

Katika beti hizi mshairi amewaingiza wahusika wengine kama vile walezi na wakunga kama wahusika wajenzi wanaosaidia kuonyesha jinsi watoto wanaopendwa hushughulikiwa. Hili ni dhihirisho kuwa watoto hawa hawatunzwi tu na wazazi bali pia watu wengine wanaolipwa kwani wazazi wao wanajimudu kiuchumi.

Hali hii ni kinyume kabisa na jinsi watoto wasiopendwa wanavyotunzwa. Vya tunu na tamasha wanavyopata watoto wanaopendwa havipatikani hapa. Hata mama zao hawana maziwa ya kuwanyonyesha. Mshairi anawafafanua hivi katika ubeti wa 18:

Mama, machuchu ni ngozi,
Kifuani yananing'inia
Machuchu machafu
Na makavu ya kunyonyea
Ndio watoto wao
Wanaojinyonyea
Hakuna maziwa ya ziada!

Usawiri huu unanuiwa kuonyesha jinsi wazazi wa kimaskini pamoja na wanao hukumbwa na hali ngumu maishani. Ubeti huu kwa mfano unajenga taswira ambapo msomaji anaweza kuwaona wahusika hawa mawazoni na kuwaonea huruma.

Isitoshe, mshairi anatusawiria mazingira machafu wanamozaliwa na kukulia watoto hawa katika ubeti wa 19 pale asemapo:

Watoto wasiopendwa
Popote utawakutia
Kwenye vumbi na tope
Ua hata njiani
Na vichochoroni pia
Ndimo wanamozaliwa
Ndimo pia hatimaye wanamoishia
Kukwepa maradhi na balia
Ndimo tuishimo sisi
Ndimo tunamokuwemo
Sisi tus'o na ulinzi
Sisi tusiojua mapenzi
Tusiopata na duhushi
Ya baba na mama pia!

Mshairi anamalizia kwa kueleza dhiki za kuchukiwa, kutusiwa, kusutwa na kusimangwa wanazopitia watoto wasiopendwa. Anahitimisha kuwa si vyema kusema baba na mama yetu ni mmoja!

Ili kufaulu katika usawiri wa wahusika wa aina hii, sharti mshairi awe ameichunguza jamii yake vilivyo na kushuhudia jinsi watu wa tabaka mbalimbali

wanavyoishi na pia kutangamana na wale wa tabaka tofauti. Sharti awe amechunguza furaha zao na dhiki zao pamoja na kinachochangia hali hizo.

'Ole wangu' (uk.63) ni shairi lililo na mhusika ambaye ni mshairi mwenyewe pamoja na viungo vyake kama vile moyo, uso na mikono. Mshairi amevitumia viungo hivi kama wahusika wa kimetonumia, ambapo vinawakilisha watu wenye tabia zinazotofautiana. Masimulizi yanatolewa katika nafsi ya kwanza hali ya umoja *ambapo mshairi anavirejelea viungo hivi pamoja na yeye mwenyewe katika hali ya* kujisemea. Shairi linaanzia kwa maneno haya:

Ole wangu mimi moyo
Ni mnyonge mtepetevu
Laini n'lokosa ushupavu
Mwenye macho magubivu
*Macho* 'lojaa kuvu
Moyo unaohofu na kuchelea
Ole wangu mimi moyo!

Ubeti huu unazungumzia hali ya kijamii ambapo mtu hujipata katika hali ya unyonge na hofu kiasi cha kutoweza kujitetea hata anapohisi kwamba yuadhulumiwa. Unyonge uliodokezwa hapa upo katika jamii zetu, ambapo wanyonge aghalabu huogopa kujitetea kwa kuhisi kuwa wao ni dhaifu wanapolinganishwa na 'wenye nguvu' wanaowadhulumu. Wengi wao wameshikilia kuwa *mwenye nguvu sharti apishwe*, hata pale wanaweza kufanya juhudi na kujikomboa.

Katika ubeti wa pili mshairi anautumia uso kama mhusika aliyeumbwa akiwa mwenye haya na hivyo kuzoea kukiri kinaya kinachoendelezwa na wanafiki. Uso huu pia umepoteza hisia kiasi kwamba hauwezi kuyakimbia maovu. Badala yake

unayarutubisha maovu hayo, si kwa sababu unayapenda bali unayakubali kwa kuwaogopa wayatendayo. Mshairi anasema hivi:

Ole wangu mimi uso
N'lioumbwa na haya
N'liozowea kukiri kinaya
N'siokimbia mauya
N'*liopoteza hisia*
Uso unaojali kuridhia
Ole wangu mimi uso!

Mshairi hapa anaisawiri jamii ambayo imejaa wanyonge wasiojua jinsi ya kuyaepuka maovu kutokana na shinikizo wanazowekewa na walio juu yao, ama kiuchumi au kiutawala. Lao huwa kuyakubali yanayotendwa na wakuu hao hata kama ni mambo yasiyotarajiwa kutoka kwao.

Mikono nayo inarejelewa katika ubeti wa tatu ambapo tunaiona ikiwa na ulemavu kiasi cha kukosa kutoa tahadhari na pia kukosa bidii ya kukomesha kiburi, na badala yake inaendeleza ujeuri katika jamii. Mikono hii, sawa na moyo tuliojadili hapo juu inawakilisha watu katika jamii ambao wameukubali unyonge na hivyo kuwatia moyo wanaoendeleza maovu.

Mshairi anajitokeza waziwazi kama mhusika katika ubeti wa mwisho anapoililia hali yake ya kujilimbikizia maudhi kwa kuchelea kufikwa na madhara yanayomzingira. Anakiri kuwa amekubali kusikiliza porojo zinazotolewa na walio juu na kushangaa ni lini atashindwa kuivumilia hali hii ya unyonge.

Shairi hili kwa jumla lina wahusika wanaodhihirisha hali ya unyonge uliokithiri miongoni mwa wanajamii wanaojichukulia kama viumbe dhaifu, na hivyo

kutofanya lolote ili kujiondoa katika unyonge huu. Matokeo yake ni kwamba wanaodhulumu wanaendelea kudhulumu ilhali wanyonge wanao uwezo wa kujikomboa.

Uteuzi wa wahusika sawa na huu unajitokeza katika shairi liitwalo 'Moyo wangu umefumba' (uk.64) ambapo mhusika ni moyo wa mshairi. Usimulizi wake pia upo katika nafsi ya kwanza ambapo moyo wake umeathiriwa pakubwa na mapenzi. Mapenzi ni swala la kijamii ambalo hutokana na maingiliano kati ya watu na hivyo kupata kuzungumziwa na wasanii kote duniani. Mashairi mengi yanayozungumzia mapenzi aghalabu huwa na moyo, malaika, maua na nyota kama wahusika. Hawa hutumika kuelezea hisia nzito na pia kuulinganisha urembo wa wapendwao na ule wa mazingira ya mshairi.

Katika shairi hili kuna wahusika wawili wakuu wanaoingiliana moja kwa moja. Mhusika wa kwanza ni mshairi mwenyewe anayemrai mhusika wa pili, ambaye ni mpenzi wake aridhike na penzi lake. Mshairi amechagua kutumia kiwakilishi 'wewe' badala ya kumtaja anayempenda kwa jina lake halisi. Moyo nao umehuishwa kiasi cha kuweza kutenda mambo sawa na binadamu. Mshairi anakiri hivi:

Moyo wangu umefumba tokea kuingia wewe
Kama tumba kama tumba hifadhi yako na iwe
Wewe ni ua la mimba na chipukizi ikuwe
Na furaha imewamba imekuzunguka wewe
Moyo wangu umefumba!

Ubeti huu unaonyesha jinsi watu hutamaniana kiasi cha kuibua hisia nzito. Hisia hizi ndizo zinazomfanya mshairi kumwahidi ampendaye kuwa kamwe hataingia mwingine wa kuwatenganisha. Hii pia ni hali halisi ya kijamii ambapo mapenzi wakati mwingine hukatizwa na tamaa. Mara nyingine yule anayedai kupenda huwa

na mpenzi wa kando. Ndiposa mshairi anamhakikishia mpenziwe hivi katika ubeti wa tatu:

| | |
|---|---|
| Moyo wangu umefumba | hata'ngia mwenginewe |
| Na uhozi ukitamba | makao yako mwenyewe |
| *Nyonda zinazokupamba* | *tele tele zichukuwe* |
| Na mimi nitaziramba | raha ul'o nazo wewe |

Moyo wangu umefumba!

Licha ya hayo, wakati mwingine huzuka mahasidi ambao hujaribu kuuharibu uhusiano huu. Ndiposa katika ubeti wa mwisho mshororo wa pili mshairi anawarejelea mahasidi hawa bila kuwataja majina. Anamhakikishia ampendaye kuwa juhudi zozote wanazofanya hao mahasidi zitaambulia patupu kwani penzi lao li thabiti.

| | |
|---|---|
| *Moyo wangu umefumba* | *ndani umejaa* wewe |
| Mishale wanayotunga | itagonga kwenye jiwe |
| Haipigi ikalenga | pendo letu waliuwe |
| Itadunda itagonga | na lengo lao lisiwe |

Moyo wangu umefumba!

Mshairi amewatumia wahusika wa aina mbili katika shairi hili. Apendaye na apendwaye ndio wahusika wakuu. Kisha kuna wahusika wajenzi kama vile mpenzi wa kando na mahasidi ambao tumerejelea hapo juu. Hawa wametumiwa ili kushadidia yanayosimuliwa na apendaye, ambaye ni moyo wa mshairi.

Hali ya uhalifu na ufisadi inarejelewa kupitia wahusika wezi katika shairi liitwalo 'Wevi' (uk.73). Kupitia shairi hili fupi la ubeti mmoja, mshairi anayasawiri mazingira ya kijamii ambamo mna wezi wa tabaka tofauti. Mshairi anasema atamshambulia mwizi tajiri na kumhurumia mwizi maskini kwani wezi hawa *wanatofautiana. Shairi hilo lasema hivi:*

Wevi wote, ninawachukia
Na moyoni, sitawasifia
    Ela baina yao
Niambiwe yupi kumshambulia
    N'*tasema na kujibu*:
'Mwizi tajiri    'tamshambulia
Mwizi fakiri    'tamwonelea
    Kwa sababu kuna
    Wevi na wevi!'

Mshairi hapa amewateua wahusika wezi ili kuukashifu wizi kama jambo lisilokubalika katika jamii. Hata hivyo, angependa kusisitiza kuwa wezi hawa huiba kwa sababu tofauti. Matajiri walinganishwapo na maskini hawaibi kutokana na uhitaji bali huongozwa na tamaa. Ndiposa mshairi anasema atamshambulia mwizi *tajiri na kumwonea huruma mwizi maskini kwani kuna wevi na wevi!*

Uteuzi huu wa wahusika pamoja na usawiri wao kwa jumla umetokana na weledi wa mshairi wa mazingira yake ya kijamii, ambapo ameyachunguza mambo ambayo huwafanya wanajamii kuwa na tabia fulani. Hili ni dhihirisho kwamba tabia mbalimbali zinazoshuhudiwa miongoni mwa wanajamii hazitokei tu bali zina visababishi vyake.

Mashairi mengine mafupi yaliyo na wahusika wanaodhihirisha hali za kijamii ni kama vile 'Mmoja na mwengine' (uk.74) na 'Punda' (uk.75). Katika 'Mmoja na mwingine' mshairi anawalinganisha wahusika wawili, mmoja msalihina (mfuasi wa dini) na mwingine mtoro sana. Mshairi anasema hivi:

Mmoja msalihina    husali nini?
Na ye' kizuwizi hana    umma kuhini

Mwengine mtoro sana    msikitini
Haramu hajaiona    yu safi moyoni
Yupi msalihina?

Uteuzi wa wahusika hawa umeongozwa na maswala ya dini na ufisadi ambayo ni maswala ya kijamii. Mshairi amewatumia wahusika hawa kuwakilisha watu halisi kwa lengo la kuonyesha jinsi watu hao huikejeli dini kupitia vitendo vyao visivyoakisi mafunzo ya kidini. Katika ubeti huu mshairi anamlinganisha mtu anayejidai kuwa muumini huku akiwahini wenzake, na mwingine asiye muumini bali yu safi moyoni kwani hatendi lolote haramu. Anashangaa ni yupi muumini.
Katika shairi liitwalo 'Punda' (uk.75) mshairi amemchagua mnyama anayejulikana sana hapa Afrika Mashariki kama mnyama wa huduma. Hata binadamu ajaribu vipi kumgeuza, hawezi kamwe kuubadilisha uhalisia huu. Mshairi anasema:

Punda kubadili soji    hakumfanyi si punda
Hata msu'ze kwa maji    na manukato 'kipenda
Na kisha umwite Haji    na soji kutomtanda
Katu hageuki- punda!

Mshairi hapa amegusia maswala ya dini, kazi na mapambo ambayo yanatokana na mazingira yake ya kijamii. Swala la kidini linajitokeza pale mshairi anasema kuwa hata punda akibadilishwa jina na kuitwa Haji (muumini wa dini ya Kiislamu ambaye amewahi kwenda Maka) bado ataendelea kuwa punda. Hata ukimbadili ule mfuko wake wa kubebea mizigo (soji) au kuuondoa kabisa habadiliki kamwe. Msuze hata majini au kwenye manukato, punda ni yule yule!

Ujumbe unaosisitizwa hapa ni kuwa hata tunapojaribu kuufunika ukweli kiasi kipi tutakuwa tunapoteza muda. Mshairi amechagua kumtumia punda kwa sababu taswira yake inajengeka akilini kwa urahisi.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Mwanamke amesawiriwa kama mhusika katika shairi liitwalo 'Mwanamwari wa kesho' (uk.109) ambapo mshairi anaeleza matumaini yake kuwa mwanamke wa baadaye atakuwa huru kuliko yule wa wakati huu. Uteuzi huu umeongozwa na swala la kijamii ambapo mwanamke, hasa katika tamaduni nyingi za Kiafrika, *huchukuliwa kama kiumbe dhaifu anapolinganishwa na mwanamume.* Mshairi anaanzia hivi:

> Mwanamwari wa kesho,
> atazaliwa vyengine
> mwembamba au mnene
> Mweusi au mweupe
> *Makini au mahepe*
> atatoka huru
> mimbani mwa mama'ake!

Katika ubeti huu mshairi anatabiri siku ambayo mwanamke atazaliwa akiwa huru licha ya hali yake ya kimaumbile kama vile wembamba, unene, rangi au uwezo wa kiakili.

Ubeti wa tatu nao unatabiri hali mpya ya malezi ambapo mwanamke atalelewa kwa furaha wala si kwa huzuni, bila kubaguliwa kwa misingi yoyote ile. Malezi haya hayatajali iwapo mwanamke huyu ni msafi au mchafu au iwapo ameolewa au ni mjane bali mwanamke huyu 'mpya' atakuwa na uhuru kamili. Mshairi anasisitiza:

> Mwanamwari wa kesho,
> atalelewa vyengine
> kwa furaha si mavune
> Msafi au mchafu
> *Mjane au mwolefu*

atakwenda huru
nchini mwa baba'ake!

Mshairi anapomalizia anasema kuwa mwanamwari wa kesho hatakuwa mtumwa tena licha ya kuwa mwanamke. Mwanamke huyu pia hatatawishwa tena wala kuishi akilalamika. Hatakashifiwa tena kwa kuishi na wanaume nje ya ndoa japo kwa kujichagulia wala kwa umalaya. Mshairi anamweleza hivi:

Mwanamwari wa kesho,
Si mtumwa tena ingawa ni mwanamke
Si mtawa tena ingawa yu ndani mwake
Si mtete tena ingawa umbile lake
*Si hawara tena ingawa hiari yake*
Si malaya tena hata hivyo watamke
Atakuwa huru
usoni mwa baba'ake

Ubeti huu unaeleza jinsi jamii inavyomchukulia mwanamke hata ingawa wanaume pia ni wa kulaumiwa kwa hali zinazowakumba wanawake. Kwa mfano, uhawara na umalaya hauwezi kuendelezwa na mwanamke tu pasipo na mwanamume. Lakini jamii humkashifu tu mwanamke na kumdhalilisha bila hata kumtaja mwanamume. Ndiposa mshairi akamchagua mwanamke kama mhusika wake ili kujaribu kuirekebisha hali hii.

**2.4 Mazingira ya kisiasa**

TUKI (2004) inalieleza neno siasa kama 'itikadi inayofuatwa na kundi au jamii fulani ambayo ni msingi wa kuendesha uchumi, utamaduni na mwenendo mzima wa maisha ya jamii hiyo'. *Itikadi ni imani au mambo ambayo mtu anaamini kuwa ni kweli.*

Kutokana na maelezo haya tunaweza kusema kuwa imani hii ya wanajamii ndiyo itakayoyafanya maisha yao kuwa bora au mabaya. Kazi nyingi za fasihi zimeandikwa kuonyesha migogoro ya kisiasa inayokumba mataifa mengi ulimwenguni kwa lengo la kutafuta suluhisho la migogoro hii. Waandishi wa kazi *hizi wamepata msukumo wa kuziandika baada ya kushuhudia hali mbaya* zinazowakumba wananchi kutokana na dhuluma wanazotendewa na watu walio mamlakani au waliohodhi nyenzo za kuzalisha mali. Lengo la waandishi hawa huwa kuwazindua wanaonyanyaswa ili wajikomboe. Waandishi hawa pia hudhamiria kuwaonya wanaodhulumu kuwa siku zao zayoyoma kwani udhalimu hautaendelea milele.

Nyingi za kazi hizi huwa na wahusika walio na uwezo mkubwa na hivyo kuwanyanyasa wahusika wengine walio na uwezo mdogo au wasio na uwezo wowote. Ili kujikomboa kutokana na dhuluma hizi, mara nyingi mwandishi humsawiri mhusika au wahusika wanaowashinikiza walio na uwezo kuwapa nafasi ya kuzifurahia rasilimali za taifa. Nafasi hii isipotolewa wale wanaonyanyaswa aghalabu *huungana na kuwaondoa wanyanyasaji kwa nguvu. Zipo pia kazi za* kizalendo zinazotungwa ili kuisifia mifumo bora ya kisiasa pamoja na viongozi bora.

Utafiti huu umedhihirisha kuwa baadhi ya wahusika wanaopatikana katika mashairi ya Kiswahili wanatokana na hali nzuri au mbaya zinazosababishwa na mifumo ya kisiasa. Katika baadhi ya mashairi tunapata wahusika wanaolilia hali zao zilizosababishwa na mifumo mibaya ya kisiasa iliyoathiri ugawaji bora wa rasilimali *za taifa. Baadhi yao wanaonekana kuwa washaamka na hawako tayari kudhalilishwa* tena.

Baadhi ya mashairi yana wahusika dhahiri ilhali mengine yanamsawiri mshairi kama kiakisi cha mwangwi wa kilio cha haki kinachotolewa na wanyonge. Katika

mashairi ya aina hii, mshairi anajisawiri kama mhusika na hivyo kutoa maoni yake na ya wanajamii wenzake kuhusu mifumo mibaya ya kisiasa na mapendekezo juu ya jinsi ya kuiboresha.

Katika diwani ya **Jicho la Ndani** (2002) kuna mashairi yaliyo na wahusika waliosawiriwa kwa lengo la kudhihirisha hali mbalimbali za kisiasa. Shairi liitwalo 'Moyo unaniuliza' (uk.87) linazua mjadala baina ya mshairi na moyo wake ambapo moyo unataka kujua maana ya uhuru. Jibu linalotolewa ni kwamba maana ya uhuru ni 'ndugu kumtesa ndugu'.

Mjadala huu unapofika mwisho tunapata jibu kuwa ndugu hawanyanyasani kwa sababu ya rangi wala kabila bali kwa sababu ya tamaa kubwa iwafanyayo kupigana kwa maneno, silaha na udanganyifu wa kila aina. Ndiposa mshairi akasema hivi katika ubeti wa mwisho:

"Uhuru," unaniuliza,
"maana yake nini?"
Jibu: "Ndugu kumtesa ndugu!"
Na wewe unakataa!
"Kwa nini?" Unaniuliza,
Tatizo si rangi wala kabila,
tatizo ni utashi wa jalala."
"Vipi, ati vipi?" Unauliza:
"Kwa maneno, silaha na hadaa!"
Na hayo yote wewe wakataa!

Wahusika hawa bila shaka wametumika kuelezea dukuduku zilizo mioyoni mwa wanyonge ambao, kutokana na mifumo mibaya ya kisiasa hawajafurahia matunda ya uhuru.

Viongozi dhalimu wanaoogopewa na wananchi wazalendo wanasawiriwa kupitia shairi liitwalo 'Simwabudu mtu' (uk.42) ambapo mshairi kama mhusika anakariri kwamba hawezi kumwogopa kiongozi kama huyo. Katika ubeti wa kwanza mshairi anashangaa kwa nini watu wamche binadamu mwenzao na kumwona kama Mungu *na kuapa kuwa yeye hawezi kuingia katika hatia kama hiyo. Katika ubeti huo* mshairi anasema hivi:

| | |
|---|---|
| Kiongozi as'o razini | wamchaje? |
| Kumtia Uunguni | 'takuwaje? |
| Siingii hatiani | na viweje! |

Simwabudu mtu!

Kupitia ubeti wa mwisho tunaona jinsi wanyonge hutetemeka miguuni wanapowaona wakuu wa aina hii. Mshairi anakiri:

| | |
|---|---|
| Watetema maguuni | 'tetemeje? |
| Umwonapo usoni | hofu ije |
| Kwake yeye wewe duni | 'taridhije? |

Simwabudu mtu!

Mshairi anasema hawezi kamwe kukubali hali kama hii inayowatia wanyonge hofu mara tu wawaonapo wenye nguvu. Bila shaka mshairi amemsawiri mhusika jasiri asiyewahofu wakuu kwa lengo la kuizindua jamii ili ijikomboe kutoka kwa utumwa huu.

'Wapenda haki' (uk.51) ni shairi linalowasawiri wahusika wasiotetereka katika msimamo wao wa kutaka haki. Mshairi anawasifu watu wa aina hiyo kwa kusema kuwa hawaudhiki daima wala kuvunjika nyoyo wanapotetea haki. Anaongeza kuwa wapenda haki husonga mbele bila wasiwasi wowote na kwamba hawachoki,

kutikisika wala kunung'unika hadi taabu zao zinapogeuka kuwa haki. Mshairi anahitimisha kwa maneno haya:

Wameavywa tabu wapenda haki
katu hawachoki
wala hawatikisiki
kamwe hawanung'uniki
Mpaka tabu zao zigeuke haki!

Hili ni shairi lingine lililo na wahusika wasiowacha mabwana na wako tayari kuumia katika harakati za kupambana na mabwana hao. Pia linatoa uzindushi kwamba wanyonge hawafai kuukubali unyonge wao bali wanafaa kuzipigania haki kwa uwezo wao wote.

Mshairi amelitumia donda ndugu kama mhusika anayewawakilisha wakoloni wakongwe na wakoloni mamboleo katika shairi liitwalo 'Donda ndugu' (uk.114). Swala hili ni nyeti hadi wa leo katika mataifa mengi ya Kiafrika ambayo yaliirithi mifumo mibovu ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kutoka kwa wakoloni.

Katika ubeti wa kwanza mshairi anaeleza jinsi alivyoridhishwa na kuondoka kwa wakoloni na kudhani kuwa mambo yangetengenea. Lakini alishangaa kuona kuwa ukoloni mamboleo ulichipuka ghafula kama donda ndugu ambalo haliponi kamwe licha ya kuota kovu. Mshairi anasema:

Nilipoona li' kavu limefumba sawasawa
Kuwa limeota kovu labda limepuchiwa
Na harufu yake mbovu yote imeondolewa
Kumbe ndani tepetevu lapukucha halepowa
Donda ndugu!

Kuanzia ubetu wa pili mshairi anaeleza jinsi donda hili la ukoloni mamboleo lilivyozidi kuenea kwa kuingiliwa na wadudu waliolipekecha kiasi cha kutouliwa na

dawa iliyotiwa. Wadudu hawa wanaweza kulinganishwa na Waafrika waliourutubisha ukoloni mamboleo kiasi cha kuupa nguvu hadi ukakita mizizi.

Ubeti wa nne unawasawiri wahusika waliopewa maumbile tofauti kama njama ya kuwatenganisha. Hawa wanatumiwa kuonyesha jinsi ukoloni ulivyowatenga Waafrika kwa misingi mbalimbali. Katika ubeti huo mtunzi anasema:

Huyu kamvika ndevu yule sharubu kapewa
Huyu yu kijivujivu yule kijani akawa
Huyu amejaa kovu yule safi amekuwa
Huyu mjini mtovu yule shamba atakiwa
Donda ndugu!

Katika ubeti wa tano na ule wa sita, mshairi anasisitiza umuhimu wa umoja ili kuliondolea mbali hili donda ndugu. Ubeti wa tano unasema kuwa kutokana na ushirikiano, donda hili sasa limetibuliwa na maumivu yamejaa. Wahusika hawa wanaoshirikiana ni kielelezo cha wazalendo wanaozidi kupambana ili kuondoa *ukoloni mamboleo*.

Mwishowe mshairi anashangaa ni kwa nini ushirikiano huu hauendelezwi na watu wanaozigutuka njama za wadhalimu na hivyo wakawa huru. Haya yapo katika ubeti wa mwisho usemao:

Kwa ni' hatuwi werevu njama tukazitambuwa?
Tukaujuwa wokovu ambao tumefichiwa
Umoja wetu mpevu hiyo kwetu ndiyo dawa
Katu hatuwi 'tulivu kama hayo hayakuwa
Donda ndugu!

Kwa jumla mshairi amewatumia wahusika wa aina kadha katika shairi hili ili kudhihirisha jinsi wakoloni walivyoingia Afrika na hata baada ya kuondolewa athari

zao zikasalia kutokana na vibaraka wao. Amewatumia wahusika wengine kuonyesha umuhimu wa kushirikiana ili kuondoa mifumo mibaya ya kisiasa, kiuchumi na kijamiii iliyoachwa na wakoloni.

Katika shairi liitwalo 'Nyumba ya ndoto' (uk.126) mshairi anaitumia nyumba kama mhusika anayeliwakilisha taifa bora waliloahidiwa wazalendo na viongozi waongo. Mshairi anaanza kwa kusema kuwa imepita miaka mingi tangu kuahidiwa nyumba hii ambayo mpaka sasa haijakamilika. Kisha anaeleza jinsi viongozi wamekuwa wakitoa visingizio vya aina mbalimbali, mara fundi aliwatapeli vibarua, au hakukuwa na vifaa muhimu.

Katika ubeti wa kumi mshairi anaonekana kukata tamaa anapokiri kuwa yeye hudhani hii ni nyumba ya ndotoni au ya hadithini ambayo hubomoka mara tu ijengwapo. Anasema:

> Pengine mimi hudhani,
> ni nyumba ya mawazoni
> ionekanayo;
> na wal'ojaliwa kuona...
> Pengine mimi hudhani,
> ni nyumba ya hadithini
> ya paukwa pakawa,
> nyanya 'lotusimulia!
> Bali sasa tu wakubwa,
> twajua haiwezi kuwa...
> Pengine mimi hudhani,
> ni nyumba ya karata,
> inayoporomoka,
> kabla ya kwisha kujengwa...



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Usawiri wa nyumba pamoja na watu kama wahusika katika shairi hili ni dhihirisho kwamba mshairi anaweza kuwasilisha ujumbe wake kupitia aina mbalimbali za wahusika.

**2.5 Mazingira ya Kiuchumi**

Mshairi, sawa na waandishi wengine na wasanii kwa jumla huangazia maswala nyeti yanayoibuka katika jamii yake. Hii ni kutokana na hali ya kuwa mshairi ni mwanajamii, na hivyo huyaelewa vyema matukio katika jamii yake.

Hali ya kiuchumi ni mojawapo wa mambo ambayo mshairi hawezi kupuuza anapotunga, hasa ikizingatiwa kuwa ulimwengu wa kisasa unaegemea zaidi upande wa mfumo wa kibepari. Huu ni mfumo wa kiuchumi unaowawezesha watu wachache kumiliki rasilimali na njia kuu za uchumi wa nchi.

Mfumo huu huendeleza ubinafsi ambapo watu walio na nafasi ya kuchuma mali huichuma bila kuwajali wenzao ambao hawakubahatika. Matokeo yake huwa kuzuka kwa tabaka. Tabaka la juu ni lile la matajiri kupindukia ambao aghalabu huwatumia watu wa tabaka la chini kujinufaisha. Tabaka la kati linajumuisha watu walio na uwezo wastani wa kiuchumi. Hawa si matajiri kupindukia wala maskini hohehahe. Nalo tabaka la chini ni lile la maskini kupindukia. Ili mshairi aweze kuwasawiri vyema wahusika katika tabaka hizi ni lazima aifahamu vyema hali ya kiuchumi ya wanajamii wenzake. Mshairi pia anaweza kuitungia hali yake binafsi ya kiuchumi kama kiwakilishi cha jamii pana inayomzingira.

Utafiti huu umedhihirisha kuwa washairi huwachota wahusika wao kutoka kwa tabaka mbalimbali zilizojengwa na mifumo ya kiuchumi. Wahusika hawa hutumika kuonyesha migogoro iliyopo baina ya wanaodhulumu na wanaodhulumiwa kiuchumi. Imedhihirika pia kuwa watu wanaojishughulisha kwa njia mbalimbali ili kujiendeleza kiuchumi hutumika kama wahusika katika mashairi ya Kiswahili.

Hupatikana pia wahusika wanaojipata katika hali nzuri au mbaya kutegemea jinsi walivyojiendeleza kiuchumi. Baadhi yao hujikuta wakiendelea vyema maishani huku wengine wakikabiliwa na hali ngumu za kiuchumi. Hali hizi zimedhihirika vyema kupitia usawiri wa wahusika wa aina mbalimbali waliojitokeza katika *mashairi kadha katika diwani zote mbili.*

Hata ingawa Mbega (1984) amejaribu kujiepusha sana na mashairi yanayodhihirisha ukinzani katika jamii, mashairi yake machache yanaudokeza, japo kwa mbali. Katika shairi liitwalo 'Ulimwengu' (uk. 23), mshairi anaisawiri jamii yenye wahusika waliojaa ulafi kiasi kwamba wanafanya kila hali kujipatia mali, hata ikibidi kuwaumiza walimwengu wenzao. Mshairi anasema hivi katika ubeti wa pili:

Ulimwengu ghafi, thamani hauna
Bakia ulafi, na kupokonyana
Ukapigwa kofi, na kusukumana
Wapendao safi, huwezi waona.

Mgogoro unaorejelewa hapa unadhihirisha mazingira ya kiuchumi ambayo si shwari. Walimwengu wamejaa maovu kama vile ulafi, kupokonyana, kupigana na kusukumana. Wapendao haki hawapo tena. Ni dunia ya mwenye nguvu mpishe.

Ujumbe huu huu unashadidiwa katika ubeti wa tano ambapo mshairi anausawiri ulimwengu uliojaa pingamizi na udanganyifu kiasi kwamba usipomaizi kinachoendelea utajikuta umeghilibiwa. Mshairi anasema:

Ulimwengu gozi, lililoshupana
Una pingamizi, zisowezekana
Nyakatize hizi, za kudanganyana
Kama humaizi, wenda patikana.

Hapa mshairi anadhihirisha kuwa walimwengu watafanya lolote ili kujinufaisha. Mfumo wa kiuchumi umezua hali ya kutoaminiana ambapo sharti walimwengu wajichunge na walimwengu wenzao ili wasihadaiwe.

Katika shairi hili mshairi amelitumia neno ulimwengu kuwakilisha walimwengu, tabia zao, na mitagusano yao kwa jumla.

Swala la kiuchumi linadhihirika tena katika shairi liitwalo 'Uzee' (uk. 49-50) ambapo mshairi anaishauri jamii juu ya umuhimu wa kujiwekea rasilimali. Wahusika katika shairi hili ni wanajamii kwa jumla, hasa walio na nguvu za mwili za kujichumia mali. Mshairi anawashauri kuwa wawapo na nguvu za kujitafutia riziki, wafanye hivyo kwa njia za haki na waweke akiba ya kuwafaidi siku za usoni ili wasiishilie katika uzee wa kifakiri. Ujumbe huu unadhihirika vyema katika ubeti wa nne na wa tano mshairi asemapo:

> Yafaa sana hadhari, uandae la kujipa
> Sijipende uhodari, kuchuma ukazitupa
> Lipo`le ni tahayuri, la majuto na kuapa
> Uzee wa kifakiri, ni jambo la kuogopa.
>
> Ujana una hatari, pale unapokutopa
> Uyatenzile kwa ari, kununua na kukopa
> Fimbo `ye ni ufakiri, mwishowe kuja kuchapa
> Uzee wa kifakiri, ni jambo la kuogopa.

Katika ubeti wa tano mshairi anawasawiri wahusika vijana ambao mara nyingine hukabiliwa na hatari ya kuchuma kwa tamaa kubwa na kuishilia katika umaskini mkuu. Hii ni taswira kamili ya jamii iliyojaa changamoto za kiuchumi na walimwengu walio katika harakati mbalimbali za kujichumia mali.

Beti za sita na saba zinadhihirisha hali ngumu zinazowakabili wazee maskini. Kupitia beti hizi mshairi anasisitiza umuhimu wa kujichumia mali na kujiwekea akiba badala ya kuwategemea watu wengine siku za uzeeni. Ubeti wa sita unasisitiza kuwa wazee waliokabiliwa na umaskini hatimaye hutupiliwa mbali na *watu ambao hapo awali walidai kuwasaidia. Mshairi anasema hivi:*

Uzee wa kifakiri, msache kuuogopa
Uzidiwapo umuri, kwongea kuzidi hapa
Wambao wakusitiri, wakawa vichopachopa
Uzee wa kifakiri, ni jambo la kuogopa

Mzee asiye na uwezo wa kiuchumi anasawiriwa katika ubeti wa saba, ambapo mshairi anasisitiza kuwa mzee huyu hukonga na kukosa nguvu kiasi cha kutopendeka. Hili linadhihirisha kuwa hali za kiuchumi huchangia pia maingiliano kati ya wanajamii. Mzee huyu habaguliwi tu kwa sababu ya uzee bali pia kwa sababu ya umaskini uliomkabili. Pengine kama angekuwa na mali asingekongoka na kunyauka kwa haraka. Pengine wanaompenda wangeongezeka kwa lengo la kurithi mali yake. Tazama jinsi mshairi anavyomtahadharisha msomaji:

Wakati hujiamiri, haina ziha mifupa
Viungo havina bari, mgongo uwe wanepa
Na uso haunawiri,  ujaa tele vitapa
Uzee wa kifakiri, ni jambo la kuogopa

Mshairi anamlinganisha mzee maskini na njiwa huri katika ubeti wa kumi ili kusisitiza hali mbaya inayomkabili. Huyu ni aina ya ndege mkubwa mwenye mchanganyiko wa rangi ya kijivu na rangi nyeupe ambaye hula nafaka. Ndege huyu akosapo nafaka safi shambani hujitweza kwa kuchakura mapipani akitafuta nafaka

au chochote kinachoweza kuyaendeleza maisha yake. Mshairi anatoa onyo hili kwa mtu yeyote asiyetunza rasilimali yake vyema:

Utabaki njiwa huri, kuchungulia mapipa
Upite 'kijiaziri, na huku walapalapa
Uitamani kaburi, hali kufa waogopa
Uzee wa kifakiri, ni jambo la kuogopa

Ulinganishi wa wahusika hawa wawili unaisawiri hali ya kukatisha tamaa inayoweza kumkabili mtu uzeeni iwapo hatajifanyia mipango mahsusi ya kiuchumi awapo kijana. Ndiposa mshairi akamsawiri njiwa mwenye njaa anayechakura mapipani na kula kipatikanacho humo kwa tamaa kubwa huku akitamani kufa kwa *sababu ya masaibu yaliyomkabili ilhali yuaogopa kufa.*

Taswira hii inajengeka vyema katika akili za msomaji na hivyo kuweza kuitafakari hali halisi inayomkumba mhusika huyu maskini. Ni hali ya kuaminika ya mazingira magumu ya kiuchumi anamoweza kujipata binadamu halisi.

Ushauri kuhusiana na maswala ya kiuchumi pia unatolewa katika shairi liitwalo 'Tumaini' (uk.20) ambapo mshairi anawaonya walimwengu kwa jumla dhidi ya kutojitafutia chao huku wakiwategemea watu wengine. Mshairi anatahadharisha kuwa asiyejichumia chake atakufa maskini. Shairi linaanzia hivi:

Wafa uli masikini, utumaipo cha ndugu
Na chanda kuwa menoni, moyo ukafanya tungu
Kisikufae dhikini, kikawa juu ya ndungu
Ukitumai cha ndugu, wafa uli masikini.

Kwa kurejelea methali kuwa mtegemea cha nduguye hufa hali maskini, mshairi anaonyesha uhusiano wa kijamii ambapo aghalabu ndugu hufaana kwa hali na mali. Hata hivyo kufaana huku ni kwa muda tu. Wakati mwingine anayemsaidia mwenzake huchoka na kumtaka ajitafutie riziki. Kinachoandama ni majuto makuu ambayo *hayasaidii kwa vyovyote vile kwani umaskini utakuwa umeshaingia*. Hali ya kiuchumi ya mhusika huyu itakuwa inaendelea kufifia.

Mshairi anamsawiri ndugu asiye wa kutegemewa katika ubeti wa nne kwa kusema kuwa usikitamani cha ndugu kama huyo kwani huenda mkagombania hali hiyo hadi kukufanya ujute sana. Mshairi anatuonya hivi:

> Ndugu asiye imani, ingawa ya vuguvugu
> Chake usikitamani, pataingia vurugu
> Mtoleane undani, utamani funga vugu
> *Ukitumai cha ndugu, wafa uli masikini.*

Sababu ya mshairi kumsawiri mhusika huyu jinsi alivyofanya ni kuonyesha jinsi maswala ya kiuchumi yanaweza hata kuwagombanisha watu walio na uhusiano wa karibu. Kwa kushadidia ujumbe huu, mshairi kupitia ubeti wa mwisho anatoa mfano wa ugomvi aliopata kuushuhudia. Anasimulia haya:

> Niliyaona zamani, pande hizo za Kiwegu
> Ukazuka ukakani, Ba Mwarizo na Mwadegu
> Ikawa yani ni yani, kisa kuombana mbegu
> *Ukitumai cha ndugu, wafa uli maskini.*

Mwarizo na Mwadegu ni wahusika wanaotumiwa na mshairi kuonyesha jinsi watu huweza kugombana iwapo mmoja atataka kumtegemea mwenzake, japo kwa jambo dogo kama kuombana mbegu.

Shairi hili linadhihirisha kuwa si lazima mshairi awatumie wahusika kuijadili migogoro mikuu ya kiuchumi bali pia maswala madogomadogo ya kiuchumi.

Diwani ya **Jicho la Ndani** (2002) pia inayo mashairi kadha yenye wahusika wanaodhihirisha hali mbalimbali za kiuchumi. Katika baadhi ya mashairi, mshairi amejisawiri kama mhusika anayewawakilisha maskini, huku mengine yakiwa na wahusika dhahiri.

'Watoto wanaopendwa' (uk.57) ni mfano wa shairi lenye wahusika dhahiri wanaotumiwa kuonyesha jinsi watoto waliozaliwa katika jamii zilizo katika hali mbalimbali za kiuchumi hulelewa. Katika shairi hili tunawaona watoto waliozaliwa katika jamii zenye uwezo mkubwa wa kiuchumi wakilelewa kwa anasa, huku watoto wa maskini wakipambana na maisha magumu. Ulinganushi huu wa kitanakuzi unajitokeza vyema katika beti zifuatazo:

Watoto wanaopendwa
vitanda wataundiwa
vya mlezi kusukiwa
kwenye pembea muruwa,
huku wamevishwa visoksi
vikofia na visweta
kuhifadhi viguu vyao
na uchafu na baridi
ya utosi na vifua!
**(Ubeti wa tatu)**
Watoto wasiopendwa
wanapozaliwa
huwa hawana viguo

walivyoshonewa
Hawana soksi
walizonunuliwa
Wala sweta
walizoshonewa
Nani vitanda mlezi
atawachongea?
Na vitu vya michezo
nani atawanunulia?
**(Ubeti wa 16)**

Beti hizi mbili zinadhihirisha kuwa mshairi anaweza kuwateua wahusika ambao watamsaidia kuendeleza maudhui ya umaskini na utajiri. Hali hizi zinadhihirika katika shairi hili kupitia usawiri wa watoto waliotunzwa vyema wakilinganishwa na wengine ambao wako taabani. Wazazi wao pia wanaonekana kuwa walijitayarisha kwa njia tofauti ili kuwapokea wanao kabla hawajazaliwa kama tulivyoona hapo awali. Haya yote yanatokana na hali tofauti za kiuchumi.

Tofauti kati ya maisha ya tajiri na maskini pia zinajitokeza katika shairi liitwalo 'Sauti ya masikini' (uk.102) tunapomwona maskini akilalamikia hali ya kubaguliwa na tajiri. Katika ubeti wa tatu tunamwona maskini akiifafanua himaya ya tajiri hivi:

Mbele umeenea
na nyuma umezongea
Kote umejaa
Pembeni upo
na mbavuni pia
Umetanda Kaskazi
Umedhibiti na Kusi

Matlai ni yako
Na Mande pia!
Kila kitu n'chako
Ela,
*Maumbile ya yetu bia!*
Anga ni letu pamoja
Mito ni yetu shirika
Maziwa na bahari pia

Katika ubeti huu, mshairi hataji tu kwamba tajiri ana mali nyingi bali anayasawiri mandhari inamopatikana mali hiyo. Mali hii imetapakaa kote kiasi kwamba kila kitu ni chake. Hata hivyo maskini anahisi kuwa licha ya tofauti hizi za kiuchumi binadamu wote ni sawa kimaumbile.

Kupitia usawiri wa wahusika tajiri na maskini mshairi anataka kutuonyesha kuwa hali za kiuchumi ndizo huwatenganisha waja na kuwafanya waonekane tofauti ilhali wanadamu ni wamoja.

Kama tulivyoona katika sehemu ya mashairi yanayoyasawiri mazingira ya kijiografia, shairi liitwalo 'Mtango' (uk.130) linadhihirisha tofauti za kitabaka. Maskini anauenzi mmea huu umpao chakula ilhali tajiri anatishia kuung'oa.

Usawiri huu unadhihirisha jinsi watu wa tabaka hizi mbili huishi kwa mikinzano katika maisha halisi kwani wanaishi katika dunia mbili tofauti 'zilizoumbwa' na tofauti zao za kiuchumi. Hali hii inashadidiwa na maneno ya mshairi katika shairi liitwalo 'Vicheko' (uk.134) anapowasawiri wahusika wachekao huku wakisonona kwa *ndani. Anaanza kwa maneno haya:*

Vicheko vya watu wale sijaviona kwengine

Wachekao kwa kelele kwa mengi yao mavune

Huku gego waliona

Kumbe ndani wasonona!

Mshairi anaendelea kusema kuwa vicheko hivi si halisi bali ni tiba ya maradhi ya siku nyingi. Ajabu ni kwamba furaha ya watu hawa ni kama ugonjwa kama inavyodhihirika katika ubeti wa pili ambapo mshairi anatongoa:

Vicheko vya watu wale sijavikuta kwengine

Furaha yao ni ndwele ndiyo tiba ya swenene

Huku gego waliona

Kumbe ndani wasonona!

Katika beti mbili za mwisho mshairi anaendelea kushangazwa na vicheko hivi vilivyojaa dhiki, huku mauti yakiwacheka wachekaji bila wao kunena kitu. Hii ni hali ya kusikitisha iliyosababishwa na hali ngumu za kiuchumi. Ni usawiri wa hali halisi ambayo huwakumba maskini wanaoishi maisha ya uchochole.

Sio maskini tu wanaolalamikia kutoridhishwa na hali ya kiuchumi. Katika shairi liitwalo 'Utambi wa kibatari' (uk.67) tunampata msomi ambaye, licha ya kupata elimu ya juu hajamakinika kiuchumi akilinganishwa na wenzake walioipuuza elimu kwa sababu walizaliwa katika jamii za kitajiri. Anarejelea siku za utotoni na kusema *kuwa yeye alipochochea utambi wa kibatali ili asome*, wenzake waliojiweza kiuchumi walistareheka vitandani huku wakiota juu ya maisha ya anasa ya baadaye. Hata hivyo yeye hajuti kwani ana maarifa kuwapiku wale waliokuwa wakimdharau. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema:

Nilipo' nikichochea utambi wa kibatali

Wao wakiunogea usingizi wa asali

Na ndoto kujiotea ya kesho yao sahili
Lakini sijuti, sijuti asilani!

Tofauti za kiuchumi zinazidi kudhihirika katika ubeti wa tatu ambapo mshairi anaeleza jinsi yeye na wenzake walitofautiana hata kwa upande wa chakula:

Nilipo' kiuma meno kwa uchachu wa tumboni
Wal'o 'kitafuna nono tumbo kawa shuwarini
Bila kweche msumeno ul'o kwereza changoni
Lakini sijuti, sijuti asilani!

Katika ubeti huu mshairi anadhihirisha hali ya umaskini wa kupindukia ambapo msomi huyu hangeweza kujipatia lau cha kuyatuliza matumbo alipokuwa shuleni. Kwa upande mwingine, watoto wa matajiri walitafuna vinono na kujiburudisha vilivyo.

Kuanzia ubeti wa tano mshairi anaeleza jinsi wenzake hao walivyoendelea kiuchumi kufikia sasa ilhali yeye hana chochote ila vitabu alivyojibebea kichwani. Wao wanajifaharisha kwa majumba yenye vitalu pembeni, mashamba makubwa waliyoyapata kwa kuwanyanyasa maskini na pia wana magari. Isitoshe, watu hawa wanawatononesha wanao, marafiki na wazazi wao kwa kila wanachotamani.

Kwa upande wake msomi, vitabu vimempa pumbazo tangu utotoni. Anasema hivi katika ubeti wa tisa:

Vitabu kwangu pumbazo mwandani as'o kifani
Vitabu kwangu liwazo toka kwangu udogoni
Ni mali yangu timizo vimejaa kabatini
Hakika sijuti, sijuti asilani!

Ubeti wa kumi na moja unaeleza jinsi msomi anavyovithamini vitabu. Mhusika huyu anasema kuwa vitabu humpa mawazo kiasi cha kumulika mafichoni na kuona jinsi matajiri huchumia gizani ili kujipatia mali na anasa zaidi. Mtunzi anasema:

| | |
|---|---|
| Na 'vyo hunipa mawazo | kumulika mafichoni |
| Kwenye yao mafichizo | wanamochuma gizani |
| Wawaniapo mjazo | wa raha na burudani |
| Hakika sijuti, sijuti asilani! | |

Usawiri huu wa wahusika unatusaidia kuona jinsi watoto wa matajiri huipuuza elimu kwa sababu ya misingi waliyowekewa na wazazi wao. Vile vile mshairi anawatumia kuonyesha jinsi matajiri hujipatia mali kwa hadaa na kuitumia kuwaharibu watoto wao na kuwaburudisha jamaa na marafiki.

Kupitia wahusika hawa tunaona jinsi watoto wa jamii za kimaskini huithamini elimu tangu wakiwa wadogo kwani wanaitazama kama chombo cha kuwakomboa, sio tu kiuchumi bali pia kimawazo.

**2.6 Kiishilio**

Katika sura hii tumejadili jinsi mshairi anavyoweza kuathiriwa na mazingira ya aina mbalimbali katika uteuzi wake wa wahusika. Hili limefanywa kwa kuzingatia msingi wa nadharia ya ulimbwende unaosisitiza umuhimu wa kuyazingatia maisha ya kawaida, ambapo mshairi anafaa kuwatambua na kuwafuatilia wahusika hao katika shughuli zao ili aweze kuwasawiri ipasavyo katika mashairi yake.

Mazingira ya kihistoria ni muhimu kuzingatiwa kwani yanaturejesha nyuma kiwakati na hivyo kushuhudia tukio linalosimuliwa likitokea. Matukio hayo yanaweza kuwa yanarejelea maisha ya mtu binafsi, kundi la watu, taifa, bara au ulimwengu kwa jumla. Urejeshi huu ni muhimu kwani hakuna jambo linalotendeka

bila kuwepo kwa wakati wa utendekaji wake. Ni wazi kwamba tunapouelewa wakati wa tukio fulani tunaelewa zaidi sababu ya mshairi kuandika jinsi alivyoandika kuhusiana na tukio hilo kwani baadhi ya matukio huturejesha kwenye kipindi maalumu cha kihistoria.

Mshairi pia anaweza kuongozwa na mazingira yake ya kijiografia anapotunga. Nadharia iliyoongoza utafiti huu inasisitiza kuwa hatufai kamwe kujitenga na ulimwengu wetu halisi kiasi cha kuwa na macho yasiyoona na pia masikio yasiyosikia. Hivi ni kumaanisha kuwa mshairi sharti ayasawiri mazingira yake ya *kijiografia kwa kuangalia jinsi wanyama, wadudu, mimea na maumbile mengine* yanavyotangamana na kuyalinganisha na tabia za watu. Ni kupitia usawiri wa aina hii ambapo tunawapata wahusika wa kiistiari, kimetonumia na kitashbihi wanaodhihirika kupitia ujenzi wa taswira.

Mazingira ya kisiasa pia hujitokeza katika usawiri wa wahusika wanaotumiwa na washairi. Hili linatokana na hali ambapo mshairi anamzingatia binadamu katika maisha yake ya kila siku na hivyo kuzishuhudia taabu na raha anazopitia, zikiwa ni pamoja na zile zinazosababishwa na hali za kisiasa zinazomzunguka. Iwapo hali hizi *zinasababisha usumbufu katika maisha ya mhusika, tunamwona* akiwa katika harakati za kujikomboa. Iwapo mambo ni mazuri tunamwona akiwasifu watu kama vile viongozi wa kisiasa au mashujaa walioyaboresha.

Kupitia usawiri wa wahusika kwa kuzingatia mazingira ya kijamii, tunamwona binadamu katika asasi mbalimbali za kijamii ambapo anaingiliana na binadamu wenzake kwa njia mbalimbali. Imani yake kuhusu maisha kwa jumla hujitokeza *kupitia kushiriki kwake katika mambo kama vile ushirikina, kazi,* ndoa na elimu miongoni mwa mengine.

Mambo mengine ya kijamii yanayodhihirika kupitia usawiri wa aina hii ya wahusika ni kama vile ulezi wa watoto na matokeo yake na tabia mbalimbali za watu na jinsi zinavyoyaathiri maisha yao pamoja na yale ya watu wengine walio karibu nao.

Mwisho kabisa kuna mazingira ya kiuchumi. Katika kusawiri wahusika kwa kuzingatia swala hili, mshairi huichunza mifumo ya kiuchumi ya jamii yake na jinsi inavyowaathiri wanajamii kwa jumla. Migogoro baina ya matajiri na maskini ni mojawapo wa mambo ambayo hujitokeza, pamoja na pendekezo la mshairi juu ya utatuzi wake. Ili kufanikisha kazi yake, mshairi huwasawiri wahusika matajiri katika *anasa zao huku maskini wakisononeka kwa ulitima. Mara nyingine* tunawapata matajiri wanaowatumia maskini kwa manufaa yao wenyewe.

Imedhihirika kuwa mshairi anaweza kuwatumia wahusika kutoka kwa mazingira tofauti katika shairi moja ili kuuwasilisha ujumbe wake kikamilifu. Kwa mfano, shairi linaweza kuwatumia wahusika wanaopatikana katika mazingira ya kijiografia kuelezea matukio ya kisiasa na kijamii.

Wordsworth (1798) kupitia mashairi yake kama vile *The Foster Mother's Tale, The Mad Mother* na *The Idiot Boy* anadhihirisha kuwa mshairi huyazingatia maisha ya kawaida ya wahusika pamoja na mazingira mbalimbali walimojikuta ili kudhihirisha uhalisia wao. Huu ndio mhimili mkuu wa nadharia iliyoongoza utafiti huu na ambao umebainishwa kupitia mashairi yaliyohakikiwa.

Katika sura inayofuata tunaangalia aina mbalimbali za wahusika na umbuji wao kishairi. Lengo kuu la mtafiti katika sura hii ni kubainisha jinsi washairi hutumia ubunifu wa hali ya juu kuwasawiri na kuwatumia wahusika wa aina mbalimbali wanaopatikana katika mazingira yao kuwasilisha ujumbe wao.

# SURA YA TATU
# WAHUSIKA NA UMBUJI KISHAIRI

## 3.0 Utangulizi

Ushairi, sawa na kazi nyingine za fasihi huwatumia wahusika wa aina mbalimbali ili kujieleza kikamilifu. *Hill* (1977) anasisitiza umuhimu wa kutumia ubunifu ili kuwaunga wahusika pamoja, wawe viumbe vilivyo hai au vitu visivyo hai. Anasema *kuwa hali hii huyafanya matukio na hali zilizomo kuvutia* kwa kuyahusisha na hali ya kimaumbile na ujenzi wa taswira. Sura hii inachunguza jinsi ubunifu umetumika kuwasawiri wahusika na pia kuonyesha mahusiano baina ya wahusika, hasa pale wahusika wawili au zaidi wametumika katika shairi moja.

## 3.1 Wahusika Binadamu

Mashairi mengi yaliyomo katika diwani zilizoshughulikiwa katika utafiti huu yana wahusika binadamu. Hii inatokana na ukweli kwamba mshairi huwatungia binadamu, na hivyo ujumbe huwafikia kwa uyakinifu zaidi iwapo atawazungumzia *kupitia binadamu waliosawiriwa wakiwa katika maisha yao ya kila siku.*

Mbega (1984) kupitia shairi liitwalo 'Mpewa sumu hafile' (uk.28) anawatumia wahusika binadamu waliounganwa pamoja kupitia usawiri wa matukio yanayosababisha uhasidi baina yao. Mshairi anaeleza jinsi wahusika hawa walivyotenganishwa na uchu wa mmoja wao aliyepanga kumtilia mwenzake sumu. Lakini hali hii inabadilika kwani aliyekusudiwa hakudhurika bali aliyeitengeza *sumu hiyo ndiye anayedhurika.*

Mshairi anadhihirisha ubunifu wake katika ubeti wa saba ambapo anasema kuwa unayemdhania kalala huenda akazinduka. Iwapo atashuku uhusiano baina yenu, anaweza kuukwepa mtego uliomtegea na wewe ukaangamia badala yake. Mtunzi anatahadharisha hivi:

Umdhanie yulele, yulele kutazinduka
Huwa yu ngezi akele, akele akimulika
Akuonapo u vile, u vile asivyotaka
Mpewa sumu hafile, afile mwenye kupika.

Mshairi kwa jumla ameonyesha jinsi binadamu huishi maisha ya kuviziana ili wapate kudhuriana, hususan kwa kuwatumia wahusika wake kiubunifu.

Shairi liitwalo 'Mlezi' (uk.38) linaonyesha uhusiano wa karibu sana uliopo baina ya mlezi na mtoto, ambapo mtoto hajimudu bila mlezi. Ili kuthibitisha utegemezi huu, mshairi kupitia ubeti wa nne anaonyesha jinsi mlezi husumbuka mtoto awapo mgonjwa. Mshairi anasema:

Mwana akiwa hawezi, mlezi huwa asamba
Ramli hizi na hizi, makombe na mitishamba
Na utanda wa hirizi, na miko ya kula vumba
Ajapokuwa mgumba, ana mashumu mlezi.

Mshairi haelezi tu kwamba mtoto humtegemea mlezi bali anaonyesha pia jinsi anavyojishughulisha, hadi akaingilia ushirikina. Ndiposa katika ubeti wa tano mshairi anawahusisha pia waganga kama wahusika muhimu. Hapa mshairi anajaribu kuwaunga wahusika mbalimbali wanaotofautiana katika majukumu wanayotekeleza katika kuyaokoa maisha ya mtoto huyu mgonjwa. Mshairi anasema hivi katika ubeti huu:

Mlezi hajitulizi, kwenye waganga atamba
Akaigea palizi, na vyote vilivyo shamba
Waganga huja vikozi, na mijikoba mitumba
Ajapokuwa mgumba, ana mashumu mlezi.

Wahusika waganga wameingizwa kiubunifu kwa lengo la kuonyesha jinsi mlezi hufanya kila liwezekanalo kuhakikisha kuwa mtoto yu salama. Katika maisha ya kawaida, si kila mlezi atawakimbilia waganga pawapo na shida. Mshairi amewatumia wahusika hawa kusisitiza matatizo ya ulezi na utatuzi wake bali sio *kuusifu ushirikina.*

Katika ubeti wa nane mshairi anasisitiza umuhimu wa mlezi kwa kuwataja shangazi na mkaza mjomba kama wahusika wengine. Lengo hapa ni kuonyesha kuwa si lazima mlezi awe mzazi wa mtoto anayemlea ili amtunze vyema. Anaweza kuwa anamlea mtoto wa kupanga au akawa shangaziye mtoto huyo au hata mkaza mjomba. Kwa maoni yake, mlezi hafai kuvunjiwa heshima kamwe. Ndiposa anasema hivi:

Astahili pongezi, japo mwana wa kuomba
Japo akiwa shangazi, au mkaza mjomba
Usimpe simangizi, wala kashifa kumwamba
Ajapokuwa mgumba, ana mashumu mlezi.

Mshairi pia amelishughulikia swala la unyumba kupitia usawiri wa binadamu wa jinsia ya kike na kiume na kuonyesha jinsi wanavyohusiana nje na ndani ya ndoa. Hili linajitokeza katika mashairi kama vile 'Ni kheri mke muole' (uk.67) na 'Uke wenza' (uk.69). Katika shairi liitwalo 'Ni kheri mke muole' mshairi anaonyesha *jinsi wanawake wakware hujifaharisha na wanaume wengi pasi na haya.* Mshairi anawalinganisha wanawake hawa na mke mkuu aliyetulia kwake na kuiheshimu ndoa yake na kuhitimisha kuwa ni heri mke mkuu.

Wahusika wengine kama vile waume wa kando na wazazi wametumika katika shairi hili kushadidia maudhui ya ndoa. Hawa wanadhihirisha jinsi watu walio nje ya ndoa wanaweza kuchangia kuvunjika kwake. Kwa mfano, waume wa kando ndio wanaoshiriki mapenzi na wake wanaokashifiwa na mshairi.

Kwa upande mwingine, wazazi wa wake hawa wanawaunga mkono wanapowakimbilia baada ya kukosolewa na waume zao. Mshairi amewatumia wahusika hawa kiubunifu kuonyesha jinsi matatizo katika ndoa huzidishwa na watu ambao wanatarajiwa kuyasuluhisha. Katika shairi hili tunawaona wazazi wa mke *wakimchochea dhidi ya mumewe badala ya kuwapatanisha.*

Wahusika binadamu wanajitokeza pia katika shairi liitwalo 'Uke wenza' (uk.69) ambapo mshairi anamsawiri mume aliye na wake wawili wanaogombana. Mshairi amefanikiwa kuwaunga wahusika watatu kiubunifu kupitia usawiri wa ndoa iliyojaa mashaka. Anadhihirisha uhusiano uliokuwa mzuri hapo awali kati ya wake hawa wawili kabla ya wivu kuingia na kuwatenganisha.

Awali mume anashuku kuwa wapo mahasidi kama vile majirani ambao huenda ndio waliowafitini wakeze. Hili ni dhihirisho kuwa uhusiano baina ya wahusika unaweza kuwa na matokeo mazuri au mabaya. Majirani hapa wanaweza kulinganishwa na wahusika wajenzi katika riwaya na tamthilia ambao hujitokeza kwa muda mfupi bila *kupewa nafasi ya kukua. Ni dhihirisho kwamba wahusika katika ushairi huweza* kujengana, sawa na ilivyo katika tanzu nyingine za fasihi. Hili linajitokeza katika ubeti wa kumi ambapo mtunzi anasema hivi:

> Kama kuna mafatani, wanaowatia kicho
> Ikiwa ni majirani, wawaonea kijicho
> Dawa yao wasuteni, wakome wafitinicho
> Ni kipi mgombeacho, wake wawili nyumbani?

Ili kufafanua zaidi uhusiano baina ya wahusika, mshairi katika ubeti wa kumi na tano anataja swala la ukewenza ambapo aghalabu wake wawili nyumbani huwa hawapatani. Awali, kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa tisa mume ameeleza kwamba hana awanyimacho wakeze na hivyo hawana cha kugombania. Lakini hapa

anafichua asili ya ugomvi huu. Anasisitiza kuwa kiwagombanishacho ni wivu. Ubeti huu unasema:

> Nawambia fahamuni, ki nguoni kiwalacho
> Roho zenu zituzeni, mjijuwe kiumacho
> Ya *ukewenza ya'cheni, pasiwe na kigombwacho*
> Ni kipi mgombeacho, wake wawili nyumbani?

'Mwosha' (uk.43) ni shairi linaloangazia uhusiano uliopo baina ya mwosha na mwoshwa. Hawa ni wahusika wawili binadamu. Tofauti yao ni kwamba mmoja wao yu hai na mwenzake ni marehemu. Mshairi anatuonyesha jinsi wahusika hawa huhusiana kwa kawaida, kwani mwosha ndiye humtayarisha mwoshwa kabla hajazikwa.

Mwosha anasawiriwa kama mhusika mwenye maringo. Amesahau kwamba siku yake ya kuoshwa pia itatimia naye atendewe vile vile alivyozoea kuwatendea waliofariki. Mshairi anaanzia shairi kwa kutuangazia hivi:

> Sikuye itimiapo, mwosha naye ataoshwa
> Pale watu aoshapo, na yeye atanyooshwa
> Atalazwa papo hapo, penginewe hatapishwa
> Mwosha naye ataoshwa, sikuye itimiapo

Katika shairi hili, mshairi anabadilishana nafasi za wahusika na kuyafanya mambo kuwa kinyume mbele. Ili kusisitiza jambo hili, mshairi anaeleza mambo yote atakayotendewa mwosha afapo. Haya ni pamoja na kunyunyiziwa maji na kuvishwa mavazi ya maiti, kama anavyosema mshairi katika ubeti wa tatu:

> Ajapotia kiapo, juwa kitapukurushwa
> Wasemi wakutanapo, maji ya ndugu kurashwa



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Na kafani na tendapo, vyote hivyo atavishwa
Mwosha naye ataoshwa, sikuye itimiapo

Mshairi kwa jumla amewatumia wahusika hawa kiubunifu kwa lengo la kuonyesha jinsi baadhi ya watu hujitapa na kujiona kama walio na kibali cha kuwatenda wengine. Anawaonya watu kama hao kuwa sawa na mwosha, siku yao ya kutendewa yale yale waliyowatendea wengine itafika. Kama inavyotambua nadharia *iliyoongoza utafiti huu, watu wa aina hii wanaweza kupatikana katika kijiji* au kitongoji chochote.

Mashairi yaliyo na wahusika binadamu katika **Jicho la Ndani** (2002) ni mengi. 'Posa' (uk.3) ni shairi lililo na wahusika wanaohusiana kinyumba. Shairi zima lina sauti ya mhusika wa kike anayeeleza matumaini yake ya awali aliposikia kuwa kuna watu wanaoleta posa ili apate kuolewa. Alidhani kuwa angepata mume wa kisasa na *pia wa kuaminika lakini mambo hayakuwa hivyo. Badala yake aligundua kuwa* lililokuwa likimposa ni janaume bazazi lenye wake tisa!

Maskini mwanamke huyu analazimika kuivunja ile posa na kubaki na kilio moyoni, huku akitamani kuposwa na mwanamume aliye mkweli wa kuaminika. Kilio chake ki wazi katika ubeti wa mwisho asemapo hivi:

Yu wapi yu wapi wa kuja kuniposa?
Al'o mkweli wa kuaminika,
N'tasema...
Wewe ni wewe n'takayekushika,
N'taposikia unaleta posa!

Mshairi amewaunga wahusika hawa kwa kuitumia sauti ya mwanamke huyu kiubunifu bila ya kuwahusisha wahusika wengine moja kwa moja. Lakini kufikia

mwisho tunaweza kusema kuwa mshairi amewagubika wahusika wengine kadha kwa sauti ya mhusika mmoja. Hawa ni pamoja na mshenga (ubeti wa 5), mume na wakeze tisa (ubeti wa 11) na mwanamume wa kisasa wa kimawazo (ubeti wa 6 na 12). Wahusika hawa wote ni muhimu kwani wanatudhihirishia jinsi dunia *ilivyokosa uaminifu, hasa kwa upande wa ndoa.*

Katika shairi liitwalo 'Mshenzi' (uk.10) tunamwona mhusika anayejitambulisha kama mshenzi kwani kama anavyokiri mwenyewe, ndivyo aitwavyo na matajiri. Mshairi amemtumia mhusika huyu kuonyesha hali ngumu wanazopitia watu maskini huku matajiri wakifurahia anasa. Kama ilivyokuwa katika mfano uliotangulia, tunawafahamu wahusika wengine kupitia sauti ya mhusika mmoja. Sauti *ya mhusika huyu ni mwangwi wa sauti za maskini* wengi. Ndiposa anapozungumza anatumia maneno kama vile 'mifereji kwetu' (ubeti wa 2), 'kwetu ushenzini', 'ulofa wetu' na 'maji yetu' (ubeti wa 3) ili kuonyesha kuwa anazungumza kwa niaba ya watu wengine wa aila yake.

Katika beti zinazofuatia tunaiona sauti hii ikiwakashifu matajiri wasiojali maslahi ya maskini. Isitoshe, matajiri hawa wana tabia za kutisha kama vile kujinyonga kwa kuyakata machango yao kwa dharubu ya upanga! Pia wanayo tamaa na kutoridhika kulikokia mipaka. Hii ni njia ya kiubunifu ya kuwaunga wahusika kadha kupitia *sauti ya mhusika mmoja tu.*

Mbinu hii hii imetumika katika mashairi kama vile 'Njuguni' (uk.14), 'Kifumbatiro' (uk.19) 'Mama'angu' (uk.21) 'Simwabudu mtu' (uk.42) na 'Nichimbie kaburi' (uk.91). Uhusiano wa wahusika wa tabaka mbalimbali umedhihirika kupitia usawiri huu.

Katika mashairi mengine kama vile 'Watoto wanaopendwa!' (uk.57) uhusiano wa kijamii kupitia wahusika binadamu unadhihirika. Mshairi anaonyesha jinsi watoto

wa kitajiri hudekezwa na wazazi pamoja na mayaya kwa kupewa kila wahitajicho, wakilinganishwa na watoto wa kimaskini wanaokua kwa majaliwa ya Mola. Mshairi anayalinganua maisha haya kitanakuzi kwa kuonyesha waziwazi jinsi wahusika hawa wanavyotofautiana katika miktadha yote miwili.

### 3.2 Wahusika Wanyama

Wahusika wa aina hii ni maarufu sana hasa katika masimulizi ya fasihi simulizi. Hata hivyo, yapo mashairi mengi yaliyo na wahusika wanyama, hasa waliosawiriwa kiubunifu ili kuwakilisha tabia za binadamu. Katika baadhi ya mashairi, wanyama hutumika kama wahusika pale mshairi anapotaka kuyasifu mazingira yake ya kijiografia. Nadharia iliyoongoza utafiti huu inatambua umuhimu wa kuyafurahia mazingira yetu badala ya kujitenga nayo na kuyapuuza.

Utafiti huu umebainisha kuwa mengi ya mashairi yaliyo na wahusika wanyama yametungwa kimafumbo na hivyo yanahitaji ufumbuzi. Neno 'mnyama' katika utafiti huu linawajumlisha wanyama wakubwa kwa wadogo (wawe wa majini au nchi kavu), ndege na wadudu.

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) katika utangulizi wa **Jicho la Ndani,** tunaishi katika zama ambapo nchi zetu zinaathiriwa kwa kiasi kikubwa na matendo, kauli, itikadi na vionjo vya mataifa ya kibepari. Ndiposa Mohamed (2002) akayalinganisha maisha ya binadamu na yale ya wanyama wanaoishi kwa kuwindana katika shairi lake liitwalo 'Jicho la ndani' (uk.1).

Anaanza kwa kusema kuwa utazamapo bondeni utawaona wanyama wadogo kwa wakubwa wakila kwa amani. Lakini uwatazamapo kwa makini zaidi utagundua kuwa wako vitani. Wanyama wakubwa walio na nguvu wanawaua wale wadogo na wanyonge. Anatutolea taswira ya simba anayemfukuza paa kwa lengo la kumuua, huku kando kidogo chui analitafuna windo lake. Nyati kwa upande mwingine

wanapigana wao kwa wao, huku fisi wakisogea kwa kuyatamani mafupa. Mbwamwitu na tai nao wanakaribia ili wanufaike iwapo nyati mmoja atamwangamiza mwenzake. Mshairi anahitimisha kwa kusema kuwa hivyo ndivyo binadamu walivyo kwani huwindana kwa bunduki sawa na wawindanavyo wanyama.

Kwa kuwasawiri wanyama wakubwa kwa wadogo na kuonyesha mivutano baina yao, mshairi ametumia ubunifu mkubwa unaohitaji 'jicho la ndani' ili kung'amua ujumbe uliomo.

Mti wenye maua ya kuvutia unasawiriwa kama himaya ya wanyama mbalimbali katika shairi liitwalo 'Kadhia ya mti' (uk.34). Maua yake yanawaalika sio tu wadudu kama vile vipepeo na nyuki bali pia ndege wanaofyonza utomvu wake. Chungu na siafu pia wanafukuzana wakitafuta sukari iliyojazana humo. Lakini raha *hii inakuwa ya muda tu, kwani binadamu kwa tamaa yake anaupura mti ule na* kuondoa tanzuze. Mti huu unapoanza kukauka mijusi inauvamia na kuanza kuvila vidudu vilivyojificha mle, ukawa ndio mwisho wa utulivu uliotawala. Nyoka nao wanajificha matawini huku wakiwavizia na kuwala ndege waliotua pale. Hatimaye mti huu unabaki kukaukia jangwani kwa kuhiniwa na viumbe wasiotaka kuuona tena.

Matumizi haya ya wanyama kama wahusika yanadhihirisha jinsi mshairi alivyo na uwanja mpana wa kutungia kazi zake, bora tu awe na ubunifu. Mshairi hapa anatudhihirishia jinsi wanyama wakubwa kwa wadogo hung'ang'ania riziki ya kila siku katika mazingira ya mbugani. Pia anatuonyesha jinsi binadamu huyaharibu mazingira haya na kuwakosesha baadhi ya wanyama hawa riziki.

Kwa upande mwingine, mshairi anawatumia wanyama hawa kuonyesha jinsi binadamu huijali tu nafsi yake kiasi cha kuwindana na kuangamizana kutokana na

ung'ang'aniaji wa rasilmali. Ndiposa anawatumia wanyama hasidi kama vile nyoka na mijusi wasiojali maslahi ya wadudu kama wahusika wake.

Punda ametumiwa kama mhusika katika shairi liitwalo 'Punda' (uk.75) kuonyesha jinsi binadamu hujaribu kuugubika ukweli ulio dhahiri kabisa. Katika shairi hili, mshairi anasema kuwa hata ufanye juhudi gani kumbadilisha punda atabaki punda tu. Shairi linasema hivi:

Punda kubadili soji     hakumfanyi si punda
Hata msu'ze kwa maji     na manukato 'kipenda
Na kisha umwite Haji     na soji kutomtanda
Katu hageuki - punda!

Mshairi hapa amedhihirisha kuwa mhusika mmoja anaweza kutumika katika shairi fupi kama hili bila kuathiri uwasilishaji wa ujumbe. Ujumbe huu unamfikia msomaji vyema kwani mshairi amemtumia mnyama anayefahamika sana kwa ubebaji wa mizigo. Hata katika dini ya Kikristo, mnyama huyu anafahamika kwa jukumu alilotekeleza la kumbeba Masihi alipokuwa akiingia Yerusalemu. Kwa hivyo taswira aliyoikusudia mshairi haina utata wowote kwani hakuna juhudi zozote zinazoweza kufaulu kumbadilisha punda na kumfanya mnyama mwingine au pengine binadamu!

Shairi lingine fupi lenye wahusika wanyama linaitwa 'Ndege wamekufa' (uk.110) ambapo mshairi anawataja ndege kadha wenye manufaa na kuhuzunishwa na kutoweka kwao huku wakibaki kunguru wasiomnufaisha binadamu. Mshairi hapa amewasawiri ndege wa mwituni pamoja na wafugwao ili kumjengea msomaji taswira kamili ya ndege muhimu waliotoweka wakilinganishwa na hasidi aliyesalia. Mshairi anawachanganua hivi:

Wawapi chiriku wajuao tumbuiza?
Mramba, kasuku ndege wan'o miujiza
Mabata na kuku mno wanotosheleza
Tausi ashiku na ninga wanopendeza
*Hawa mahuluku* wote *tumewapoteza*
Alo baki huku kunguru mviza!

Mshairi anawatumia ndege wema kuwawakilisha watu wazuri wasiodumu.Hawa huangamizwa na waovu wanaobaki wakiuendeleza udhalimu wao. Ndiposa waovu hao wanalinganishwa na kunguru ambaye huchukiza hata kwa sauti yake. Isitoshe, katika shirikina za baadhi ya jamii za Kiafrika, kunguru hudaiwa kusababisha mauti *aliapo karibu na boma.*

Mshairi analitumia shairi la kimasimulizi liitwalo 'Juu ya mti' (uk.150) na kuonyesha jinsi wahusika wanyama wanaweza kutumiwa katika mashairi marefu kuendeleza ujumbe. Katika shairi hili mshairi anatusimulia juu ya mti mkubwa na mrefu uliokuwepo zamani sana na ambao uliwahifadhi vipanga. Vipanga hawa waliwatisha ndege wengine ambao walitoweka ili wasiangamizwe. Licha ya kuwasaka sana hawakuweza kuwapata, bali wakati mwingine walifanikiwa kuwala kuku waliowapata mitaani. Lakini mwisho wa kipanga unafika siku moja anapopukutika kutoka mtini baada ya kuumwa na nyoka.

Utawala wa nyoka unaanza ambapo anayatishia maisha ya ndege kwa miaka mingi, hadi siku moja ambapo ndege wanaonekana asubuhi wakishangilia kifo chake.
Kumbe nyoka yule alikuwa akitafunwa na siafu!

Mshairi ametumia ubunifu wa hali ya juu kuwaunga wahusika hawa wenye sifa na uwezo tofauti kuzisawiri sifa za binadamu wanafiki wanaojifanya kuwatetea wanyonge huku wakiyajali matumbo yao. Inavutia pale mwanzo nyoka

anapojitokeza kama mwokozi wa ndege wanaoangamizwa na vipanga. Hata hivyo, inasikitisha kuona jinsi anavyobadilika na kuwa mwangamizaji wao. Lakini hatima yake inafika anapovamiwa na siafu ambao ni wadudu tu! Hii ni ishara kuwa wanyonge waunganapo wanaweza kuwaondoa wadhalimu walio na nguvu zaidi yao.

Ndege wametumiwa tena kama wahusika katika shairi liitwalo 'Ndege na mwanadamu' (uk.154) ambapo mshairi anatusawiria urafiki wa kinafiki baina ya ndege na binadamu. Mshairi anaanza kwa kuonyesha jinsi binadamu huyu anavyovutiwa na sauti tamu ya ndege fulani na kuamua kumnasa kwa ulimbo na *mitego ili awe akimliwaza. Lakini uhusiano huu unakuwa wa muda mfupi kwani* binadamu anaanza kumkashifu ndege kwa sauti yake mbovu, ambayo anadai inamkosesha usingizi, yeye na watukufu wengine. Hatima ya shutuma hizi ni kwamba maskini ndege huyu anaishilia chunguni licha ya wema wote aliomtendea mwenyeji wake.

Mshairi ameujenga mgogoro baina ya ndege na binadamu kwa ubunifu wa hali ya juu kwa lengo la kutudhihirishia ujanja wa binadamu. Anaanza kwa kutuonyesha jinsi sauti ya ndege huyu inavutia anaposema hivi:

Ndege mghani ndege
Sauti nzuri 'kitoa
Mwenyewe itakuponza
Kuitiliza maashiki
*Kuja ndege kukunasa*
Kwa ulimbo na mitego
Kisha utiwe tunduni
Kumliwaza bwana!

Mambo yanaenda kinyume katika ubeti wa tatu ambapo ndege yule yule aliyewindwa kwa lengo la kufugwa sasa anawindwa ili auliwe. Mshairi anasema:

Basi utawindwa
Utawindwa ndege
Utawindwa
Tena kwa bunduki
Utawindwa
Na ufumwapo
Utaishia chunguni!

Kwa kumtia ndege katika hali ya kudhulumiwa, mshairi anamfanya msomaji kumhurumia ndege na kumchukia binadamu. Hii ni kwa sababu ndege hana hatia yoyote bali anadhulumiwa kutokana na unyonge wake.

Wanyama wa majini wametumika kama wahusika katika shairi liitwalo 'Wingu' (uk.100), ambapo katika ubeti wa tano mshairi anaeleza jinsi mikizi ilivyovivizia vidagaa kwa lengo la kuviangamiza. Hili linatokea baada ya wingu kubwa kutanda na kusababisha mafuriko makali. Mshairi anasema:

Likazinga maonezi wachache walioona
Waovu wakabarizi kwenye giza wakavuna
Ikachaga na mikizi vidagaa kuvibana
Hao wakapiga mbizi kuzamia kwenye vina
*Je, sasa wingu limekwenda?*

Wanyama wakubwa wanawawakilisha watu wenye uwezo wa kisiasa na kiuchumi ambao hunufaika kwa kuwanyanyasa wachochole, ambao wanawakilishwa hapa na wanyama wadogo kama vidagaa. Matumizi haya ya wanyama wa majini kama

wahusika ni thibitisho kwamba tabia za binadamu zinaweza kulinganishwa na zile za wanyama wa aina mbalimbali katika mazingira yao halisi.

### 3.3 Sehemu za Mwili

Washairi mara nyingi huzitumia sehemu za mwili kama wahusika wa kimetonumia. Kwa mfano, badala ya mshairi kutoa maoni yake moja kwa moja anaweza kusema 'moyo wangu wanambia' au 'moyo umekasirika'. Ni wazi kuwa moyo hauwezi *kusema au kukasirika bali ni mwenye moyo huo, ambaye ni mshairi* anayesema au kukasirika. Mshairi hutumia mbinu ya tashihisi anapowasawiri wahusika wa aina hii.

Katika **Dafina ya Umalenga** (1984), mshairi amelitumia chuchu kama mhusika anayewakilisha mamake katika shairi liitwalo 'Chuchu' (uk. 34) ili kuonyesha uhusiano wa karibu aliokuwa nao na mamake mzazi. Mshairi anatudhihirishia jinsi akina mama huwatunza watoto wao kwa mapenzi makuu kiasi kwamba hata wawapo watu wazima hawasahau hisani hiyo. Ubeti wa nne unadhihirisha hali hii pale mshairi asemapo:

Sondoki chuchu ilipo, 'nganisukuma
Sikomi unambiapo, ya kwamba koma
Huilinganisha pepo, yenye huruma

Bila shaka mshairi hatungi shairi hili ili kulisifu chuchu. Anakitumia kiungo hiki azizi kumsifu mamake kwani hapawezekani kamwe kuwa na chuchu bila mama. Anachofanya mshairi ni kuutumia ubunifu wake kulisawiri tukio ambalo taswira yake inajengeka kwa urahisi kwani linatokana na maisha ya kawaida.

Mohamed (2002) katika **Jicho la Ndani** amevitumia viungo kama vile moyo, uso na mikono kama wahusika katika shairi liitwalo 'Ole wangu' (uk.63). Katika ubeti wa

kwanza mshairi anautumia moyo kumwakilisha mtu aliyejaa hofu. Kupitia usimulizi wa nafsi ya kwanza, mshairi anajitia katika nafsi ya mtendewa na kueleza jinsi mhusika huyu alivyojikuta katika hali ya kutoweza kujitetea kwa sababu ya hofu. Ubeti huu unasema hivi:

Ole wangu *mimi* moyo
Ni mnyonge mtepetevu
Laini n'lokosa ushupavu
Mwenye macho magubivu
Na macho 'lojaa kuvu
Moyo unaohofu na kuchelea
Ole wangu mimi moyo!

Katika ubeti huu moyo umepewa uwezo wa kuwa na macho na hivyo kuthibitisha kuwa mshairi hauzungumzii moyo wa kawaida bali analenga binadamu. Moyo huu pia unatiwa dosari ya kutoona vizuri kutokana na hofu.

Katika ubeti wa pili uso unajilaumu kwa kuwa na haya, kukiri kinaya, kutokimbia mabaya na kupoteza hisia. Hili ni dhihirisho kuwa mshairi anawalaumu watu walio na tabia zilizotajwa.

Mikono nayo inalaumiwa kwa kutochukua tahadhari, kupoteza ari ya kukabiliana na pingamizi nzito na kukubali kuendeleza ujeuri. Sawa na uso na moyo, mikono inawawakilisha watu wasiochukua hatua yoyote kuukomesha udhalimu. Utumiaji wa viungo hivi vitatu katika shairi moja ni dhihirisho kuwa mshairi anaweza *kuvitumia viungo vyake kadha kuwakilisha watu wenye sifa tofauti*. Ni dhihirisho pia kuwa ubunifu hauna mipaka na kwa hivyo watunzi hawana budi kuutumia vilivyo katika usawiri wa wahusika wenye sifa mbalimbali watakaowawezesha kuyazungumzia maswala mengi yanayoikumba jamii.

Shairi liitwalo 'Moyo unaniuliza' (uk.87) linaupa moyo uwezo wa kuzungumza na binadamu. Mshairi anautumia ubunifu wake kiasi cha kuuwezesha moyo kuwa na mjadala na binadamu huku ukiuliza maswali na kujibu mengine. Ni dhahiri hata hivyo kuwa ni mshairi mwenyewe aliye na mjadala nafsia. Hali hii inabainika vyema katika ubeti wa mwisho moyo unapoanza kusaili hivi:

> "Uhuru," unauliza,
> "maana yake nini?"
> Jibu: "Ndugu kumtesa ndugu!"
> Na wewe unakataa!
> "Kwa nini?" Unauliza.
> Jibu: Kwa sababu,
> Tatizo si rangi wala kabila,
> tatizo ni utashi wa jalala."
> "Vipi, ati vipi?" Unauliza:
> "Kwa maneno, silaha na hadaa!"
> Na hayo yote wewe bado wakataa!

Uzungumzi nafsia pia unapatikana katika shairi liitwalo 'Moyo wangu u fidla' (uk.6), ambapo mshairi anajadiliana na moyo wake licha ya kuupa sifa kama vile kuimba, kutamba na kucheza samba. Sawa na shairi tulilotangulia kujadili, mshairi anakifanya kiungo hiki kuonekana kama mhusika huru anayeweza kuwasiliana na mtu anayekimiliki na pia kutenda mambo kana kwamba kiko nje ya mwili wake.

Katika 'Jicho geni' (uk.45) tunaona mshairi akilitumia 'jicho geni' kuwakilisha mgeni na 'jicho mama' kuwakilisha mwenyeji. Anaeleza jinsi jicho geni haliwezi kuona wazi yanayojiri ugenini likilinganishwa na jicho mama ambalo huona hata yaliyofichama. Mshairi anatoa kauli hii:

Jicho geni si angavu ingawa nalo laona
Daima hujaa kuvu penye nuru kubwa sana
Sababu lakosa nguvu kuona vil'ofichama

Huona vishehenevu lin'opasa kuviona
Vya juu vielelevu si vya chini vin'o kina
Halina uchangamavu lilo nalo jicho mama

Beti mbili za mwisho zinaeleza kuwa jicho geni hupotosha lionapo kwani huona utulivu na hali iliyotengemaa hata pale palipojaa fujo na shida. Ndiposa mshairi anasema kuwa anatamani jicho lililo kali kiasi cha kupenya kama ekisirei, bila kikwazo chochote hata ingawa matumaini yake huenda yasifike popote. Ni wazi kwamba *jicho hili analolitamani mshairi ni watu wasioogopa chochote, hasa pale* wanapozikosoa hali na sera zisizotamanika.

### 3.4 Maumbile na Vitu Vingine

Kama tulivyoona katika sura ya pili, mazingira ya kijiografia huathiri uteuzi wa wahusika. Wahusika wanyama tuliojadili katika sura hii pia wanatokana na mazingira haya. Nadharia iliyoongoza utafiti huu inasisitiza juu ya umuhimu wa kuyafanya *matukio na hali zinazosimuliwa kuwa za kuvutia kwa kuzihusisha na hali* za kimaumbile na ujenzi wa taswira. Katika sehemu hii tutaangalia jinsi maumbile kama vile mimea, maji na upepo pamoja na vitu vingine kadha vimetumika kama wahusika.

Katika sura ya pili tuliona jinsi Mbega (1984) katika **Dafina ya Umalenga** alivyolitumia nazi kama mhusika katika shairi liitwalo 'Nazi' (uk.24) kuwakilisha mjinga. Katika shairi hili mshairi anaonyesha jinsi mnazi na sehemu zake kadha hutumiwa kwa njia mbalimbali bila hiari yake kwa lengo la kumdhihaki mjinga ambaye hajitetei kamwe hata adhulumiwapo. Matumizi ya mmea kama mhusika

yanabainisha kuwa mshairi anaweza kuijenga taswira kutokana na hali ya kimaumbile na hivyo kuufanya ujumbe wake kuifikia hadhira kwa njia ya ubunifu.

Matumizi haya yanaweza kulinganishwa kwa kiasi fulani na yale ya sehemu za mwili kwani mshairi anatusawiria sehemu mbalimbali za mmea na kutuonyesha matumizi mbalimbali ya mmea huu. Ni kama mshairi anazihurumia sehemu hizi sawa na tulivyotangulia kuona katika 'Ole wangu' (**Jicho la Ndani,** uk.63). Taswira ya nazi inajitokeza vyema hasa kwa mtu anayelifahamu vyema, na hivyo kumwezesha kupata picha kamili ya mjinga kama alivyodhamiria mshairi.

Katika **Dafina ya Umalenga** (1984) tumelipitia pia shairi liitwalo 'Peku' (uk.14) ambapo vifaa vimetumika kama wahusika. Katika shairi hili mshairi ameitumia mbinu ya tashihisi ambapo peku limepewa uwezo wa kuzungumza na ungo licha ya kuwa hivi ni vifaa ambavyo kwa kawaida havina uwezo huo. Kama tulivyotangulia kuona, vifaa hivi vinawawakilisha watu wawili, mmoja mzee na mwingine kijana. Mzee anamwonya kijana dhidi ya kujivunia ujana na kuwadharau wazee kwani hata wao walikuwa vijana kama yeye na sasa ni wazee.

Jambo la kuvutia kuhusu matumizi ya wahusika hawa ni jinsi mshairi alivyojenga taswira ya hatua mbalimbali za maisha wanayoyapitia. Kwa kutumia mbinu rejeshi, mshairi anaturudisha nyuma kwa maisha ya peku wakati lilikuwa jipya kabla halijawa ungo kwa uchakavu. Anasimulia jinsi lilivyopokelewa sokoni kwa taadhima, likanunuliwa na kupelekwa nyumbani ambapo lilithaminiwa sana kabla halijachakaa na kudharauliwa. Peku linalitahadharidha ungo kuhusu hadaa za walimwengu katika ubeti wa saba ambapo linasema hivi:

> Waja haweshi vituko, matusi na masimango
> Siwaone na kicheko, cha kukithiri kiwango
> Watakupa nung'uniko, wakutumbukie nyong'o

Peku lamwambia ungo, niliko ndiko ujako

Kupitia ubeti huu, mshairi amewaunga wahusika watatu kiubunifu ili kuuwasilisha ujumbe wake kikamilifu. Wahusika hawa ambao ni peku, ungo na watu wametumika kuonyesha jinsi kwa kawaida kifaa kipya hufurahikiwa na watumizi wake *ilhali* watumizi hao hao ndio watakaokidharau punde tu kitakapokosa kuwavutia. Hiki ni kielelezo cha jinsi vijana wanapendwa wanapokuwa wachanga *lakini wanapuuzwa wanapozeeka*.

Uhusika wa kiistiari kama huu pia unajitokeza katika shairi liitwalo 'Ukuni wa koko' (uk.18) ambapo mwanamume analinganishwa na ukuni. Mshairi anawatahadharisha wanaume dhidi ya kuyakwepa majukumu yao, hasa pale yanapowapa changamoto. Ndiposa katika ubeti wa kwanza anasema kuwa mume ni ukuni wa koko ambao kwanza hufuka, kisha ukawaka bila matatizo yoyote.

Kisha mshairi anafafanua jinsi ukuni huu ulivyo rahisi kuchanjika na kutumika hata uwapo mbichi, bora tu uchomekwe na kuchochewa vyema. Hii ni ishara kuwa mwanamume hafai kujilegeza kamwe, bali anafaa kujitahidi katika lolote afanyalo ili aweze kufaulu. Katika ubeti wa tatu anasema hivi:

Siufanyie dhihaka, ungiapo penye jiko
M'bichibichi wapika, kikaiva chungu chako
Vyema ukiuchomeka, na kila uchocheako
Mume ukuni wa koko, usipowaka wafuka

Ulinganishi huu wa mume na ukuni wa koko unabainisha jinsi mshairi alivyo na mawanda mapana ya kuchagulia wahusika wake. Bila shaka kuna vifaa vingine vingi vinavyoweza kutumika kama wahusika wa kiistiari, bora tu wasawiriwe kwa njia isiyoweza kutatiza.

Katika **Jicho la Ndani** (2002) kuna mashairi yaliyo na wahusika kama vile miti, ardhi, wingu, mto na nyumba. Kwa mfano shairi liitwalo 'Huu msitu' (uk.155) linasimulia juu ya msitu uliojaa msongamano na mashindano baina ya miti dhaifu na ile mirefu isiyohofu chochote. Miti mirefu inaidhoofisha ile mifupi kwa kuinyima *mwangaza na rutuba. Mshairi anaangazia hivi:*

Katika huu msitu...
Kumezagaa kiza    kimesakini
Kinaangamiza    miti ya chini
'loshiba mwangaza    na vya ardhini
Hayebu wachiza    hayo masikani
Kila kitu huronjea juu
    Katika huu msitu!

Kwa kuitumia miti kama wahusika na kuonyesha uhusiano baina yake, mshairi anathibitisha kuwa mazingira tunayoishi yana maumbile mengi yanayoweza kulinganishwa na binadamu kwa njia nyingi, tena kwa njia ya kuvutia.

Kama tulivyoona katika sura ya pili, wingu limesawiriwa kama mhusika katika shairi liitwalo 'Wingu' (uk.100) kwa lengo la kuyasawiri mabadiliko yaliyotokea baada ya mataifa mengi ya Kiafrika kupata uhuru. Tuliona jinsi wingu hili lilivyosababisha mvua iliyoleta utelezi na maangamizi mengi kwa waja. Shairi linapoanza tunaona hali ya kutisha ambapo kuna radi na pepo kali zinazotishia *kuangamiza kila kitu. Mtunzi anaitoa taswira hii:*

Wingu kama li' masizi    lilitanda lote anga
Radi na zake konyezi    ziliwaka na kuanga
Mvua na michirizi    na pepo kubwa kupunga
Makubwa maangamizi    kila pembe yalifunga
    Je, sasa wingu linapita?

Vitisho vya wingu hili vinaelezwa zaidi katika ubeti wa tano ambapo baada ya mafuriko kuzuka, waovu walibarizi kwenye kiza huku mikizi ikiingia kwa nguvu na kuvibana vidagaa. Hali hii inadhihirisha kuwa wahusika wa aina kadha wanaweza kuchanganywa katika shairi moja na kuungwa kiubunifu, bora tu wawe *wanahusiana kwa njia fulani*. Kwa *mfano, wingu linaposababisha mafuriko* wanyama wakubwa wananufaika kwa kuwala wanyama wadogo.

Usawiri mwingine wa mhusika wa kimaumbile unapatikana katika shairi liitwalo 'Upepo' (uk. 135-137) ambapo mshairi anauchunguza kwa makini upepo unaovuma na kuutumia kama mhusika wa kiistiari. Mshairi anauhuisha upepo na kuupa uwezo wa kuathiri mazingira utakavyo. Athari anazotaja ni kama vile kupuliza mahaba, *kuleta baridi, kumwaga theluji, kuimwagia ardhi maji na kufukuza ukame*. Upepo pia unavuma na kuipeperusha njaa na kiu isiyokatika uiimarishapo mimea ya mahitaji. Uwezo huu wa upepo unadokezwa vyema katika ubeti wa kwanza mshairi asemapo hivi:

Kila siku unavuma
Kuathiri upendavyo
Kusuka kasi au
Kupulizia mahaba
Juu ya mweneo huu
U'vaao mwili wake
Na kuzuru pembe zake!

Ubeti wa nne unausifu upepo kwa kuipeperusha njaa na kumnufaisha sana binadamu. Mshairi anatongoa:

Vuma ukivuma kumwagia maji
ya mvua za kasi
ardhi kuifariji
na kufukuza ukame

udhaniwao utadumu milele

upate kuimarisha

mimea ya mahitaji

kuipeperusha njaa

*na kiu is'okatika!*

Kuathiri

Kubadili

Kuharibu

na kutengemaa!

Katika ubeti wa mwisho mshairi anaupa upepo uwezo wa kunena na binadamu. Anautaka upepo unapotulia hatimaye unong'oneze usalama na kumhakikishia binadamu kuwa hautavuma tena vibaya na kusababisha madhara. Mtunzi anasema:

Na *mwisho* utapotulia

kama vile hupo

kama vile umekimbia!

Wakati tusipokusikia

Upitapo kutunong'oneza salama

polepole kutwambia

utapotuasa

juu ya shwari

juu ya mwema urari

*na mezani* ya *heshima*

ya kila mtu

ya kila kitu

Utakapotuahidi

hutavuma tena vibaya;

milele!

Matumizi ya upepo kama mhusika ni dhihirisho kuwa mshairi anaweza hata kuvitumia vitu visivyoonekana kama wahusika wake. Upepo hauonekani, sembuse kuzungumza na binadamu, ila tu unadhihirika kupitia athari zake.

Mto pia unahuishwa na kupewa uwezo wa kusababisha madhara mengi unapoteremkia nyanda za chini kama inavyobainika katika shairi liitwalo 'Mto' (uk.105). Kama tulivyoona katika sura ya pili, mto huu unasababisha madhara kama vile kuidhuru mimea, kuumomonyoa udongo na kurundika taka mahali pasipotakikana. Madhara haya yanasababisha uhusiano mbaya baina ya mto na binadamu, ambao ni wahusika wa aina tofauti.

## 3.5 Kiishilio

Katika sura hii tumejadili jinsi wahusika wa aina mbalimbali wamesawiriwa katika mashairi kadha. Pia tumejadili jinsi wahusika hawa wameungwa pamoja kiubunifu kwa lengo la kuwafanya wawasilishe ujumbe kwa njia ya kuvutia kama ilivyosisitizwa na nadharia iliyoongoza utafiti huu.

Wahusika waliojadiliwa ni pamoja na wahusika binadamu, wahusika wanyama na sehemu za mwili. Wengine ni wahusika maumbile na vitu vingine. Pia imebainika kwamba wahusika wa aina kadha wanaweza kupatikana katika shairi moja. Wahusika waliojadiliwa wamebainisha jinsi binadamu wenye sifa zinazotofautiana huathiriana, ama kwa uzuri au kwa ubaya bila kuufanya ushairi kuonekana kama sanaa ngumu isiyo na chochote cha kuvutia.

Wahusika binadamu wametubainishia kwamba watu wa kawaida kama wanavyopatikana katika maisha ya kila siku wanaweza kutumika kama wahusika. Nadharia ya ulimbwende inatambua kuwa maisha ya kawaida ya binadamu yanaweza kusawiriwa katika mashairi kupitia uchunguzi wa mambo wanayoyapitia kila siku.

Wanyama waliotumika kama wahusika wamedhihirisha jinsi binadamu anavyolingana na wanyama kitabia anapotazamwa katika mikabala kadha. Mtu mwenye uwezo anayemnyanyasa mwenzake hana tofauti na mnyama mkubwa anayemwinda na kumla mnyama mdogo. Mshairi anaweza kuusawiri uhusiano *baina ya binadamu mnyanyasaji na mnyanyaswaji kupitia wahusika kama simba na* paa.

Sehemu za mwili zinaweza kutumika kama wahusika wa kimetonumia kuwakilisha binadamu na tabia zao zinazotofautiana. Jicho lisiloona waziwazi linaweza kumwakilisha mtu anayejifanya kutoona kinachoendelea katika jamii yake kutokana na woga. Aidha mkono usioweza kujipigania ni kiwakilishi cha mtu dhaifu na *mtepetevu asiyeweza kupambana na maovu katika jamii yake.* Moyo nao utawakilisha nafsi ya mshairi anapotoa maoni yake bila kutaka kujitambulisha moja kwa moja. Katika muktadha mwingine, moyo hutumika sana kumaanisha mpenzi.

Wahusika wengine wanaojitokeza sana katika mashairi ni maumbile na vitu mbalimbali. Mshairi huwatumia hasa anapotaka kuzilinganisha tabia za binadamu na hali za kimaumbile kama vile upepo unaovuma na madhara yake, mvua inayonyesha na kuzua mafuriko, miti mikubwa msituni inayoinyima ile midogo nafasi ya kunawiri au mkondo wa mto unaoyaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine.

Baadhi ya vitu vitumikavyo kama wahusika ni zana za kazi, ambapo matumizi yake na umuhimu vinaotiliwa huweza kulinganishwa na watu katika hatua kadha za maisha. Tumeona jinsi Mbega (1984) alivyomlinganisha kijana na mzee kwa kutumia peku na ungo *mtawalio. Pia amemlinganisha mume na ukuni* wa koko ambao usipowaka hufuka.

Wahusika hawa wanapatikana katika mashairi ya kiarudhi na mashairi huru, na hivyo kudhihirisha kuwa kuwepo au kutokuwepo kwa arudhi hakuathiri kamwe usawiri wa wahusika na uwasilishaji wa ujumbe kwa jumla. Nadharia iliyoongoza utafiti huu inatambua kuwa ushairi sio arudhi na kwamba washairi wanaweza *kujieleza kwa njia kadha kiubunifu bila kujifunga na arudhi. Mojawapo wa njia hizi* ni kupitia matumizi ya wahusika kama tulivyoona katika sura hii.

Imebainika pia kuwa kuna mawanda mapana ambayo mshairi anaweza kuwachagulia wahusika wake bila kujifunga na wahusika wa aina fulani. Kilicho muhimu ni kuyachunguza mazingira anayoishi na kuutumia ubunifu wake kuzieleza hali na matukio mbalimbali kupitia usawiri mwafaka wa wahusika, hasa wanaosaidia katika ujenzi wa taswira.

Katika sura inayofuata tunaangazia jinsi washairi walivyowatumia wahusika wao kudhihirisha hisia mbalimbali. Mtafiti amedhamiria kubainisha wajibu unaotekelezwa na wahusika katika mashairi, hususan udhihirishaji wa hisia za mshairi na athari za wahusika hawa kwa hisia za wasomaji.

# SURA YA NNE

# JINSI WASHAIRI WALIVYOWATUMIA WAHUSIKA KUDHIHIRISHA HISIA MBALIMBALI

## 4.0 Utangulizi

Washairi huyatumia mashairi kama chombo cha kuzieleza hisia zao kuhusiana na hali ya maisha yao binafsi au ya wenzao katika jamii. Hill (1977) anaeleza kuwa *waasisi wa nadharia ya ulimbwende, hasa Coleridge waliyatunga mashairi yaliyonuiwa kuelezea hisia nzito hasa zile za kimapenzi*. Kwa mujibu wa utafiti huu, wahusika katika mashairi ya Kiswahili ni chombo muhimu cha kuwasilishia hisia tofauti za washairi kwani huwa wanawakilisha binadamu halisi.

Collier (1966) anafasili hisia kama msisimko uliosababishwa na kuzuka kwa hatari, iwe dhahiri ua dhanifu, mahitaji mazito kama yale ya chakula au mapenzi; au tukio lingine lolote lisababishalo uzito wa mawazo na hatua ya dharura.

Kwa mujibu wa Microsoft (2004) wanasoikolojia wanatambua hisia tatu kuu, ambazo ni **mapenzi, hasira** na **hofu**. Hisia hizi zinaweza kusababishwa na hali zilizomo ndani au nje ya mwili wa mhusika. Kwa mfano, mhusika anaweza kuhisi mapenzi, hasira au woga anapokumbuka jambo fulani lililotukia hapo awali. Hisia hizi pia zinaweza kutokana na athari za kimazingira kwa mhusika. Kwa mfano, mtu anaweza kukasirishwa, kupendezwa au hata kuogofwa na anayoyaona, kuyasikia, kuyatenda au kutendewa.

Watunzi wa mashairi hutumia wahusika kubaini hisia mbalimbali. Hivyo, msomaji wa kazi ya fasihi anaweza 'kuisikia' sauti ya mhusika, 'kuona' anayoyapitia na pia kuhisi anavyohisi kutegemea jinsi mhusika alivyosawiriwa kiubunifu. Sura hii inachunguza jinsi washairi walivyowatumia wahusika kuzieleza hisia zao kuhusiana

na maswala mbalimbali katika jamii, kwani mshairi huwatumia wahusika kubainisha sifa za kibinadamu azipendazo au kuzichukia.

## 4.1 Mapenzi

Hii ndiyo mayotambuliwa na walimwengu kuwa hisia nzito kuliko hisia zingine zote. Si ajabu kwamba washairi wa kale kama vile Mfalme Sulemani walikosa fasili kamili ya neno hili na kueleza kuwa mapenzi yana nguvu kama mauti. Mshairi huyu *anamsawiri mhusika anayemwambia mpenziwe hivi:*

Nitie kama muhuri moyoni mwako,
Kama muhuri juu ya mkono wako;
**Kwa maana upendo una nguvu kama mauti,**
Na wivu ni mkali kama ahera.
Mwako wake ni mwako wa moto,
Na miali yake ni miali ya Yahu.

Maji mengi hayawezi kuuzimisha upendo,
Wala mito haiwezi kuuzamisha;
Kama mtu angetoa badala ya upendo
Mali yote ya nyumbani mwake,
Angedharauliwa kabisa.
(**Biblia Takatifu,** Wimbo Ulio Bora 8:6-7)

Dondoo hili linaashiria kwamba hakuna chochote kinachoweza kufidia mapenzi, ila mapenzi yenyewe. Uzito wa hisia hii unalinganishwa na kuwaka kwa moto ulio na miale mikali isiyoweza kuzimwa kwa maji mengi, hata yawapo ya mto mzima.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Mohamed (2002), sawa na Sulemani anaitambua nafasi ya mapenzi katika maisha ya binadamu. Katika shairi liitwalo 'Moyo' (uk.15) anasema kuwa uufunguapo moyo utayakuta mapenzi, miongoni mwa mambo mengine. Shairi hili fupi linasema:

Fungua
kizibo
ndani!
Utakuta
damu,
hisia,
mapenzi,
chuki,
na
ushairi
ndani ya
**Moyo!**

Kama tulivyoona katika sura iliyopita, moyo utumikapo katika ushairi huwakilisha binadamu kwani kiungo hakiwezi kamwe kujitenga na mwenyewe. Katika shairi hili moyo unamwakilisha mtu mwenye hisia za mapenzi ambazo zimefichama katika kitovu cha uhai wake, ambacho ni moyo.

Katika shairi liitwalo 'Mama'ngu' (uk.21), mshairi anamtumia mhusika mama kueleza mapenzi kwa nchi yake. Anatanguliza shairi hili kwa kusema jinsi anavyompenda mamake na kumpa nafasi yote moyoni mwake uliojaa huba na mazoea. Mshairi analifungua shairi hivi:

Jina lako tamu mamangu!

Tamu kwenye mate na ulimi
Umechukua nafasi yote
Ndani ya wangu moyo
Umejaza huba na mazoea…

Mama ametumika hapa kama mhusika anayedhihirisha mapenzi makuu yaliyopo baina ya mtoto na mamake, kiasi cha kuchukua nafasi yote ndani ya moyo wa mtoto. Isitoshe, jina la mama linaelezwa kuwa tamu kwenye mate na ulimi.

Ardhi imetumika kama mhusika wa kimaumbile katika shairi liitwalo 'Mpenzi ardhi' (uk.44) ambapo mshairi anaeleza mapenzi yake kwa nchi yake. Katika ubeti wa kwanza mshairi anaisifu ardhi kwa kuitambua kama mzazi, mlezi, mkidhi na mpenzi. Ubeti wa pili unaeleza kuwa hakuna mwingine awezaye kujaa moyoni mwa mshairi hata awapo tajiri kiasi gani isipokuwa nchi yake. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema kuwa licha ya matatizo yaliyoikumba nchi yake, ataendelea kuipenda katika tamu na chungu. Upeo wa mapenzi unafikiwa katika ubeti wa mwisho ambapo mshairi anasema yu radhi kufa akiitetea ardhi yake. Mshairi anasema:

| | |
|---|---|
| Huba yangu kwa we' | imejaa tele chungu |
| Ni tayari kwa we' | kupoteza roho yangu |
| Kesho mimi na we' | na tokea hapo tangu |
| Mpenzi ni wewe | katika tamu na chungu |

Ni wewe mpenzi ardhi yangu!
Ni wewe mbora wa walimwengu!

Mapenzi ya kizalendo yanaibuliwa pia kupitia shairi liitwalo 'Twen'zetu mpenzi' (uk.117) ambapo mshairi anawasawiri wazalendo wawili walio katika safari ya kujisaka kwa lengo la kuyapata maisha bora. Mapenzi haya yanatokana na mazingira yaliyojaa udhalimu unaowafanya wahusika hawa wawili kuhiari

kuondoka na kuelekea mahali pasipo na wasaliti. Uzalendo wao ndio unaorutubisha mapenzi haya kama yalivyofafanuliwa na mshairi katika ubeti huu:

Twen'zetu mpenzi, twende,
N'shike mkono
Na mi n'kushike
Tuhimizane suhuba
Tuchombezane mahaba
Tushikilie rubaa
Rubaa ya leo na kesho…

Ubeti huu unadhihirisha jinsi mapenzi huyafanya mambo magumu kuonekana rahisi kiasi kwamba wapendanao wanaweza kukabiliana na hali ngumu zinazowakumba bila kujali hatari zilizomo. Hapa tunawaona wapenzi wawili wakihimizana kuendelea na safari kwa kushikana mikono na kubembelezana kwa mahaba, huku wakijiunga na kundi la watu wengine wanaoendelea na safari kama yao. Wahusika hawa wawili wametumiwa na mshairi kubaini jinsi mapenzi yalivyo na nguvu ya kuwaunga watu pamoja na kuwapa msukumo wa kutekeleza vitendo, bora tu wawe na lengo moja.

Nguvu ya mapenzi inajitokeza pia katika shairi liitwalo 'Ndiwe wewe' (uk.20) ambapo mshairi anamsawiri mhusika mmoja anayejitolea sabili kuyahami mapenzi, huku akimhakikishia ampendaye kuwa hatomwacha kamwe. Shairi lianzapo tunapata ahadi ifuatayo:

| | |
|---|---|
| Ndiwe wewe | mwenye kuhozi suduri |
| Wewe ndiwe | wa awali na akhiri |
| Ndiwe wewe | ulokithiri uzuri |
| Mwenginewe | sijali sina habari |

Mhusika huyu anamhakikishia mpenziye kuwa ndiye aliyemjaa moyoni, ndiye wa mwanzo na mwisho na pia ndiye aliyejaa uzuri na kamwe hawezi kumtafuta mwingine. Katika ubeti wa tatu mhusika anabubujikwa na hisia hii nzito kiasi cha kumwahidi mpenziwe kuwa iwapo atajitokeza mwingine atamnywesha shubiri! *Isitoshe, anamsifu mpenziwe kwa kukithiri katika pendo limpalo burudani na* kumwepusha na hatari.

Mshairi hayasifu tu mapenzi bali anaonyesha pia jinsi mambo huwa magumu iwapo mapenzi yatatibuka. Anamsawiri mhusika aliyewahi kujitolea na kumpenda mtu aliyeyapuuza mapenzi hayo licha ya juhudi zake za kuyapalilia, katika shairi liitwalo 'N'kupe nini tena?' Kuanzia ubeti wa kwanza hadi wa tatu (uk.52) mhusika huyu *anaeleza juhudi zote alizotia ili kulihifadhi pendo hili. Anasema kuwa alikitoa* chochote alichokuwa nacho pamoja na moyo wake ili kumpendeza mpenziye. Hata hivyo, aliyependwa hakulithamini pendo bali aliishilia kulalamika baada ya aliyependa kutamauka. Mwishowe mhusika huyu anasema hivi:

Sasa unanililiya kunishutumu shitaka
Mengi waniaridhiya huchoki kulalamika
Hisia imekujiya na majuto kukushika
Siwezi kukuridhiya moyoni umenitoka
N'*kupe nini tena*?

Nilitoa nikakupa hukujali kulitaka
Leo unatapatapa na pendo limesharuka!

Mashairi mengine yanayozungumzia mapenzi katika diwani hii ni pamoja na 'Jaribu kunikumbuka' (uk.55), 'Moyo wangu umefumba' (uk.64), 'Nyota ya dawamu' (uk.69), na 'Mimi na We' (uk.70). Mashairi haya yana wahusika, ambao kupitia uhusiano wao tunabainishiwa jinsi hisia hii ilivyoyatamalaki maisha ya waja.

Sawa na Mohamed (2002), Mbega (1984) anaonyesha jinsi mapenzi yanaweza kugeuka na kuwa machungu. Shairi lake liitwalo 'Sikutaki' (uk.62) linazungumzia mapenzi yaliyotibuka na kumwacha mmoja wa wapenzi akijidanganya kuwa bado yuapendwa. Ili kulivunjilia mbali penzi hili bandia, mmoja wa wahusika anamjulisha mwenzake kuwa hamtaki tena hata akijipendekeza kwake. Mshairi anasema hivi:

Sikutaki, nawe nikataa
Hupendeki, umezidi baa
Lilobaki, ni kukuambaa

Katika ubeti huu ni dhahiri kuwa mhusika huyu amechoshwa na mwenzake na ashafanya uamuzi wa kumwacha. Katika beti zinazofuata mhusika anamshauri mpenziwe bandia aachane naye kwani ana ila nyingi. Hili ni dhihirisho kuwa mapenzi yakikosa raha huzua karaha.

Kama tulivyoona katika sura iliyopita, shairi liitwalo 'Si wamwe' (uk.64) linazungumzia mgogoro wa kijamii ambapo mshairi anawatahadharisha wanaume dhidi ya wanawake wajanja wasiothamini mapenzi. Mshairi anaeleza jinsi wanawake wa aina hiyo hujipamba makusudi ili kuwavutia wanaume wasio na habari ya hadaa zao. Ni wazi kuwa wanaume huishilia kuwapenda walaghai hawa na kujipata katika majuto makuu. Ubeti wa nane wa shairi hili unawatahadharisha wanaume hivi:

'Sitamiwe ni Maaja, ukacha Mwana Rugomwe
Mwenye pendo la kiseja, lenye enzi tomwetomwe
Kisha mpige pambaja, mwenda shamba msitumwe
Wangawa ni kundi moja, lakini wake si wamwe

Mshairi anasisitiza kuwa mwanamume hafai kamwe kumwacha mpenziwe wa dhati na kumkimbilia mdanganyifu ampaye pendo la hadaa. Ujumbe huu unadhihirisha

jinsi hisia hii inafaa kutunzwa kwa uangalifu isije kumtia mhusika katika balaa. Uhusiano wa wahusika waliotumika kuendeleza ujumbe huu unaonyesha wazi jinsi ujanja unaweza kuchukuliwa kuwa mapenzi na kumtia mhusika matatani.

Hali ya kutamauka kimapenzi pia inajitokeza katika shairi liitwalo 'Moyo' (uk.66) ambapo mhusika mmoja anamwambia mwenzake kuwa mapenzi yaliyokuwa kati yao hayapo tena. Mshairi anawatumia wahusika hawa kuonyesha jinsi baadhi ya watu huendelea kung'ang'ania mapenzi licha ya kujulishwa wazi na wanaodai kuwapenda kuwa hawapendwi tena. Ujumbe huu wajitokeza katika ubeti wa pili mshairi *asemapo:*

> Shukuru kama wenziyo, moyo hupendezi tena
> Kheri uchunge hadhiyo, wajibu kwako hakuna
> Pendo wapenda pekeyo, upendae akuguna
> Moyo hupendezi tena, shukuru kama wenzio

Katika beti zinazofuatia mshairi anamnasihi aliyekataliwa kuwa hana budi kuikubali hali inayomkabili kwani pendo liingiapo kasoro aghalabu halirekebiki kwa urahisi.

Mashairi mengine yanayojadili swala la mapenzi katika diwani ya **Dafina ya Umalenga** (1984) ni 'Ni kheri mke muole' (uk.67) na 'Uke wenza' (uk.69) ambapo mshairi amebainisha matatizo yanayoikumba jamii katika muktadha wa ndoa, hasa pale pana wahusika kadha wanaobishania mapenzi. Ubishi huu unabainika pale wanawake *wawili wanaohusiana kimapenzi na mwanamume mmoja* wanazozana kutokana na hisia kuwa mmoja wao anapendwa kuliko mwenzake.

**4.2 Hasira**

Katika maisha ya kawaida, wanadamu hujipata katika hali zinazowakasirisha na kuwalazimisha kuidhihirisha hisia hii kwa njia mbalimbali. Baadhi yao huamua kunyamaza wakasirikapo huku wengine wakitokwa na maneno makali. Washairi

wapo katika kundi la pili kwani huchagua kueleza hisia zao badala ya kuzibana, aghalabu kwa kuwabuni wahusika mahususi.

Mohamed (2002) anadhihirisha hasira kuu katika baadhi ya mashairi yake, hasa azungumziapo maswala nyeti yanayowaathiri wanajamii kwa lengo la kuwazindua. Shairi liitwalo 'Mshenzi' (uk.10) linabainisha hasira za mshairi kuhusiana na masaibu yanayowakumba wachochole. Ili aweze kujieleza vilivyo, mshairi anachukua nafasi ya mhusika na kusimulia katika ya nafsi ya kwanza. Mtunzi anaanzia hivi:

> Mshenzi mimi,
> ndiyo mshenzi!
> Mjinga mimi,
> mpumbavu n'naungama,
> nikijua msitari mwembamba
> baina ya ushenzi
> na ustaarabu!

Matumizi ya kishangao katika ubeti huu yanadhihirisha kuwa mhusika anayejiita mshenzi anapaza sauti kwa hasira kwani amesinyika kiasi cha kutoweza kuificha hasira yake. Ni dhahiri, kama inavyobainika katika beti zinazofuatia kuwa mhusika huyu anaishi katika mazingira yasiyopendeza kamwe. Anasema kuwa waishiko hakuna mifereji, barabara za lami wala anasa zozote bali dhiki imetawala.

Licha ya dhiki hizi, mhusika huyu anakiri kuridhishwa na hali ya utu iliyomzingira kwani aishiko hakuna ajinyongaye, kumuua mwenzake, kuiba wala kutawaliwa na tamaa jinsi walivyo matajiri waishio kwingineko. Mshairi anawalinganua wahusika wa tabaka hizi mbili ili kuonyesha kuwa hajakasirishwa tu na dhiki zinazowakumba maskini bali pia na tabia za matajiri zisizo za kiutu.

Mshairi anaonekana pia kukasirishwa na tamaa iliyofuata baada ya mataifa mengi ya Kiafrika kupata uhuru. Wanyama wa aina mbalimbali wanaoung'ang'ania mti katika shairi liitwalo 'Kadhia ya mti' (uk.34) ni wawakilishi wa watu wa tabaka mbalimbali waliojitosa katika ung'ang'aniaji wa rasilimali za mataifa yao. Si ajabu *kuwa anawaita baadhi yao 'mijusi katili'* (ubeti wa 7) na 'nyoka wenye *sumu kali*' (ubeti wa 8).

Swała ła hasira linajitokeza pia katika shairi liitwalo 'Simwabudu mtu' (uk.42) ambapo mshairi analalamikia hali ya kukandamizwa na mtu aliyejitia ubwana na kuwafanya wenzake watwana. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema katu hawezi kumtia mtu huyu Uungu kwani hiyo ni hatia. Katika ubeti wa pili *anamlaumu kwa kuwanyamazisha wasio na uwezo na kushangaa ni vipi atamcha* mtu kama huyo. Katika ubeti wa mwisho mshairi anaonyesha jinsi wanyonge hutetemeka wawaonapo madhalimu. Katika ubeti huo mshairi anasema hivi:

| | |
|---|---|
| Watetema maguuni | 'tetemeje? |
| Umwonapo usoni | hofu ije |
| Kwake yeye wewe duni | 'taridhije? |

Simwabudu mtu!

Kwa kuwasawiri wahusika wa tabaka nyanyasi na tabaka nyanyaswa, huku mshairi akijitia katika tabaka nyanyaswa, hisia ya hasira inajitokeza vyema kwani masafa ujumi yanapungua. Msomaji anapoisoma kazi hii anabebwa kihisia na kujihisi kama msemaji halisi wa maneno yanayotamkwa na mhasiriwa, hasa kibwagizo chake.

Mshairi anaonekana pia kukasirishwa na hali ya dhiki inayowakumba watoto wa maskini huku wenzao wa jamii za kitajiri wakiendelea kutononoka. Kama tulivyoona katika sura iliyopita, watu wa tabaka hizi mbili huishi maisha

yaliyobaidika kama ardhi na mbingu, kama inavyobainika katika shairi liitwalo 'Watoto wanaopendwa!' (Uk.57-62).

Mashairi mengine yanayodhihirisha hasira za mshairi ni pamoja na 'Nichimbie kaburi' (uk.90-99) na 'Chukua siuzi' (uk.101) ambapo mshairi anaonekana kukasirishwa na wadhalimu wanaowashinikiza wanyonge kuziuza haki zao. Katika mashairi haya, mshairi anajitia katika nafsi ya mhasiriwa bila kumtaja waziwazi anayemdhulumu, pengine kwa sababu za kiusalama.

Kwa upande wake, Mbega (1984) amebainisha mambo kadha yanayowaudhi wanajamii kupitia mashairi kama vile 'Nazi' (uk.24), 'Mpewa sumu hafile' (uk.28-29) na 'Ni kheri mke muole' (uk.67-68). Katika shairi liitwalo 'Nazi' tunaona mshairi akikasirishwa na watu ambao hawatafakari juu ya wanayoyatenda wala kutendewa. Ujinga wao unalinganishwa na ule wa nazi ambayo haisaili chochote *inachofanyiwa na binadamu.*

Shairi liitwalo 'Mpewa sumu hafile' linadhihirisha hasira za mshairi kuhusiana na watu wanaowapangia wenzao mabaya bila kujua kuwa mabaya hayo yanaweza kuwarudia. Ndiposa anatusawiria hali ambapo aliyeitengeneza sumu ya kumdhuru mwenzake anahangaika kwa maradhi yaliyotokana na sumu ile ile aliyoitengeneza (ubeti wa 8 na 9). Mtunzi anaeleza hivi:

> Huyule kangia wele, wele alia na jaka
> Nao ndio usalile, ndwee isoagulika
> Hatasalia kisale, ahadi atapondoka
> Mpewa sumu hafile, afile mwenye kupika

Kwa kuisawiri hali ngumu inayomkumba mhusika huyu hasidi, mshairi anaonekana kutopendezwa na watu wa aina hiyo. Mhusika huyu anaugua maradhi yasiyotibika na kuishilia kuaga dunia.

'Ni kheri mke muole' ni shairi linalomulika ndoa na kuwakashifu wanawake wasiotulia katika ndoa zao. Baadhi yao huwakimbila wanaume wengine ilhali wana waume zao na hivyo kuidhiki roho ya mshairi. Ndiposa anawalinganisha wahusika wa kike waliotulia katika ndoa na wale wanaorandaranda na kuhitimisha kuwa ni kheri walioolewa na kutulia. Isitoshe, mshairi anakasirishwa pia na wazazi wanaowaunga mkono wake wasiowatii waume zao badala ya kuwanasihi ili wazihifadhi ndoa zao. Anasema hivi:

> Watafiziba kosa'le, wapate kukuumbuwa
> Ili kusudi wakule, na maovu kutendewa
> Mwana wao atawale, ubaki huna satuwa
> Ni kheri mke muole, kama wanawali hawa

Wazo analotoa mshairi katika ubeti huu ni kuwa baadhi ya ndoa huvunjwa na wazazi wanaowapendelea binti zao hata wawapo makosani. Katika ndoa kama hizo waume hubaki bila uwezo wowote wa kutekeleza maamuzi kama vichwa vya familia. Matokeo yake ni kwamba waume kama hao hutawaliwa na wake zao, jambo ambalo linamkasirisha mshairi.

**4.3 Hofu**

Kanuni moja ya maumbile isiyopingika ni kuwa binadamu hawi shujaa wakati wote bali hukumbwa na hofu mara kwa mara. Hofu hii inaweza kusababishwa na hali zilizomo katika nafsi yake (hali za kisaikolojia) au katika mazingira anayoishi. Wakati mwingine hofu hii inaweza kuhusiana na maisha ya mhusika au yale ya wenzake waliokumbwa na hali zisizomfurahisha. Hali kama hii inapozuka, watu

hujaribu kuieleza kwa njia kadha. Ushairi unatambulika kama njia mojawapo ya kiubunifu ya kuelezea dukuduku za moyoni, ikiwemo hofu.

Mohamed (2002) ameishughulikia hisia hii kupitia mashairi kama vile 'Jicho la ndani' (uk.1-2), 'Jicho geni' (uk.45), 'Ole wangu' (uk.63) 'Kimya' (uk.120-121) na 'Nafasi yangu' (uk.131-133). Katika 'Jicho la ndani' tunaona jinsi wanyama wenye nguvu huwatia hofu wasio na nguvu kwa kuwawinda na kuwafanya kitoweo. Kwa *mfano, simba anapofukuzana na paa kando yake chui analila windo lake, huku* kukisikika kishindo cha wanyama wanaoangushana. Hali hii inahofisha pale mshairi anailinganisha na ile ya watu wanaowindana kwa bunduki, hasa nyakati hizi ambapo swala la usalama limekuwa nyeti kote ulimwenguni.

Shairi liitwalo 'Jicho geni' linaisawiri hali ambapo jicho geni huchelea kuona maovu yaliyofichama na hivyo kuendelea kuyasifu mema yasiyokuwepo. Hii ni ishara kuwa watu huchelea kuyafichua maovu yaliyokithiri katika mataifa ya kigeni wanayoishi na hivyo kuendelea kuyarutubisha maovu hayo. Mshairi amehiari *kuyalinganisha macho mawili ambapo jicho mama, ambalo haliogopi* chochote linaona zaidi ya jicho geni lililojaa hofu na hivyo kukosa kuona maovu. Macho hapa yanapewa uwezo wa kujichagulia yatakacho kuona.

'Ole wangu' ni shairi lililo na wahusika viungo kama vile moyo, uso na mikono. Wahusika hawa wanahofia hali zao iwapo watajitoa waziwazi na kuyakashifu maovu katika jamii. Hii ni ishara tosha kuwa binadamu wanaowakilishwa hapa wamejazwa hofu na wenye nguvu kiasi cha kuchagua kunyamaza badala ya kujitia mashakani.

Katika shairi liitwalo 'Kimya' mshairi anayasawiri mazingira yaliyojaa hofu kiasi kwamba kinachosikika ni mdundo wa moyo unaohofu kesho itakuwaje. Kila mtu

amenyamaa ilhali nyoyo zaumia na mwili kuliwa na funza. Kufikia ubeti wa mwisho mshairi anaonyesha jinsi hofu hii ilivyokithiri kwa kuuliza hivi:

Hivi maisha yanapaswa kutuwama?
Maisha hutuwama au;
Huvyondoka?
Mbona kimya basi?
Sisimizi kimya,
Nyenje kimya,
Sangara kimya,
hata simba?

Kwa kuwatumia viumbe dhaifu kama wadudu na walio jasiri kama simba, mshairi analenga kuonyesha jinsi hofu hii ilivyowaathiri sio tu wanyonge bali pia wenye nguvu na kuyafanya maisha kuonekana kama yamesita kabisa.

'Nafasi yangu' (uk.131-133) ni shairi linalomtia mshairi katika nafsi ya mhusika aliyedhulumiwa na kutiwa hofu kiasi cha kutojielewa kabisa. Mhusika huyu anaeleza jinsi alivyokandamizwa na mzawa pamoja naye aliyemiliki kila kitu, si maji si hewa! Kisha amemwogofya, kumshindilia na kumfanya bwege kiasi cha *kutoona, kutosikia wala kuhisi hata aumiapo. Ni dhahiri kuwa mhusika huyu* anatamani kujikomboa ila anakabiliwa na hofu inayosambaratisha matumaini yake. Katika ubeti wa sita mshairi anatumia viungo kadha kuonyesha jinsi hofu ilivyomjaa mhusika. Mshairi anasema:

Nilivyo nimeparama
Nina hofu ela simhofu!
Macho maangavu ela kipofu!
Sikio li wazi ela si sikivu!
Damu yangu tukutu, ela tiifu!

Hisia nazimezea

Na kuvimbishwa nazo pumzi!

Si hasha nikapasuka!

Mbega (1984) amezisawiri hali za kutia hofu katika mashairi kama vile 'Mwosha' (uk.43) na 'Uzee' (uk.49-50). Katika shairi liitwalo 'Mwosha' mshairi anawaonya watu wawatendao wengine kuwa siku yao ya kutendwa pia itafika nao wajikute wakitendewa yale yale waliyowatendea wenzao. Kwa kuwatumia wahusika wawili, yaani mwosha na mwoshwa, mshairi analisawiri tukio la kuhofisha ambapo mwosha anaaga *dunia hatimaye na kujikuta akipitishwa hatua zile zile alizowapitisha* wafu alipokuwa hai. Katika ubeti wa nne mshairi anasema:

Hapo wote watiwapo, na yeye ataegeshwa

Na kwa kila aliyepo, atahimiza kushushwa

Kitakuwa kipopopo, jifusi kuporomoshwa

Mwosha naye ataoshwa, sikuye itimiapo

Inahofisha kuona vituko anavyotendewa mhusika katika ubeti huu. Inaelekea kuwa jamaa huyu anatiwa kaburini na kufukiwa bila huruma! Jambo kama hili halitokei sana katika maisha halisi kwani wafu aghalabu huombolezwa na hatimaye maiti kuzikwa kwa majonzi, dua na heshima.

'Uzee' (uk.49-50) ni shairi linalozungumzia hali ngumu zinazowakumba watu wasiojiwekea akiba ya kuegemea wakati wao wa uzeeni. Mshairi anamsawiri mhusika aliyekumbwa na umaskini na kuhangaika kiasi cha kutamani kufa katika ubeti ufuatao:

Utabaki njiwa huri, kuchungulia mapipa

Upite 'kijiaziri, na huku walapalapa

Uhamani kaburi, hali kufa waogopa

Uzee wa kifakiri, ni jambo la kuogopa

Ni wazi kuwa mshairi anayahofu maisha kama haya. Ndiposa anatuonya dhidi ya kujitia katika hali inayoweza kutusababishia dhiki ya aina hii.

### 4.4 Kiishilio

Katika sura hii, tumebainisha jinsi washairi walivyowatumia wahusika kudhihirisha hisia kuu kama zinavyotambuliwa na wanasaikolojia. Hisia hizi ni mapenzi, hasira na hofu. Nadharia iliyoongoza utafiti huu inatambua kuwa washairi aghalabu *huyatunga mashairi* yao kwa lengo la kuzieleza *hisia zao* kuhusiana na hali na matukio yanayowakumba wanajamii, ambao ndio hadhira yao.

Tumeona kuwa mapenzi ndiyo hisia nzito zaidi kati ya hisia hizi kwa maana inadhihirisha uhusiano kati ya binadamu na jinsi uhusiano huu unaweza kuelezewa kwa njia mbalimbali. Utafiti huu umebainisha jinsi washairi wa kale, sawa na wale wa wakati huu wamejishughulisha na kuielezea hisia hii.

Katika mifano ya mashairi tuliyopitia tumegundua kuwa mshairi anaweza kutunga kwa lengo la kuyaelezea mapenzi yake kwa mtu au kitu fulani. Baadhi ya mashairi teule yameyasifu mataifa huku mengine yakiwasifu watu wanaopendwa. Yapo pia yaliyo na wahusika wanaowatangazia wapenzi wao mwisho wa penzi lililokuwa *limenawiri hapo awali. Katika mashairi haya, wahusika waliotumika wanadhihirisha* mahusiano ya kuaminika kama yanavyojitokeza katika ulimwengu halisi.

Hasira imeelezewa waziwazi kupitia wahusika wanaoonyesha kutoridhishwa na hali na sera fulani zinazoikabili jamii yao. Hali za kisiasa, kijamii na kiuchumi ni baadhi ya maswala yanayowakasirisha washairi na kuwafanya kuwasawiri wahusika wanaoathiriwa na hali hizo. Ili kulifikia lengo hili, washairi aghalabu huisawiri



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

migogoro na migongano iliyomo baina ya tabaka nyanyasi na tabaka nyanyaswa. Katika baadhi ya mashairi, washairi hujitia katika tabaka la wanaonyanyaswa ili kuweza kuzieleza hasira zao vilivyo.

Washairi pia hutunga ili kueleza hofu zao kuhusu hali na matukio fulani katika jamii. Hofu hizo hujitokeza vyema kupitia wahusika wanaojikuta katika hali ngumu zinazohitaji kushughulikiwa. Sawa na hasira, hisia hii hudhihirishwa katika miktadha ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Mshairi hujitokeza kama mwanajamii anayehofia hali ngumu zinazowakabili wanajamii. Tumeona jinsi Mohamed (2002) alivyohofishwa na tabia ya wanadamu ya kuwindana kama wanyama huku Mbega (1984) akihofishwa na uzee wa kimaskini.

Washairi hawa wametudhihirishia kuwa ushairi ni chombo muhimu cha kutolea hisia, hasa wahusika wafaao wanapotumika. Hii inatokana na ukweli kwamba wanajamii ni malighafi muhimu ya kuzijengea kazi za fasihi na wahusika ndio wawakilishi na viwakilishi vyao. Hisia za wahusika hawa ni hisia za binadamu halisi kwani wahusika huziakisi hali halisi zinazowakumba wanajamii katika harakati zao za kujiendeleza maishani, katika mazingira mahsusi kwa mujibu wa wakati maalum kihistoria.

Katika sura ifuatayo mtafiti anahitimisha utafiti huu kwa kutoa muhtasari wa kila sura, matokeo ya utafiti na mafanikio pamoja na changamoto alizopata wakati wa utafiti. Hatimaye mtafiti anatoa mapendekezo kwa utafiti wa baadaye kuhusiana na swala la usawiri wa wahusika katika mashairi ya Kiswahili.

# SURA YA TANO

# MAHITIMISHO

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii tunatoa muhtasari wa mahitimisho ya sura za awali za tasnifu hii. Tunashughulikia pia matokeo ya utafiti huu kwa mujibu wa malengo ya utafiti na uchanganuzi wa data iliyotokana na uhakiki wa mashairi katika vitabu viteule. Matatizo na mafanikio yaliyoibuka katika utafiti huu pia yanagusiwa. Hatimaye kuna mapendekezo ya mtafiti kuhusu utafiti unaofaa kufanywa.

## 5.1 Muhtasari

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kubainisha jinsi watunzi wa mashairi ya Kiswahili huwasawiri wahusika wao. Lengo kuu lilikuwa kudhihirisha kuwa wahusika katika mashairi, sawa na kazi nyingine za fasihi ni chombo muhimu cha kuendelezea mawazo ya mshairi.

Aidha, utafiti ulidhamiria kubainisha vigezo vinavyozingatiwa na washairi wanapowateua wahusika wao. Ulidhamiria pia kubainisha aina mbalimbali za wahusika wanaopatikana katika mashairi ya Kiswahili na jinsi wahusika hao wanavyohusiana kibunifu ili kufafanua hali na matukio mbalimbali. Hatimaye, utafiti ulidhamiria kubainisha jinsi washairi huwatumia wahusika kutolea hisia mbalimbali ili kuwaathiri wasomaji wao kihisia.

Tasnifu hii imegawanywa katika sura tano ambapo sura ya kwanza imeshughulikia ufafanuzi wa dhana muhimu zilizojitokeza katika utafiti huu. Mada ya utafiti, maswali yaliyojibiwa na utafiti, malengo ya utafiti pamoja na sababu cha kuchagua mada pia vimeshughulikiwa katika sura hii.

Katika sura hii pia pamebainishwa upeo na mipaka ya utafiti, udurusu wa maandishi yanayohusiana na utafiti huu, msingi wa nadharia iliyoongoza utafiti huu, mbinu za

utafiti pamoja na mihimili iliyozingatiwa katika uchanganuzi wa data iliyokusanywa kutoka kwa vitabu vilivyoteuliwa.

Sura ya pili imeshughulikia vigezo vinavyozingatiwa na washairi katika uteuzi wa wahusika. Kigezo cha mazingira ya kiutunzi kimezingatiwa kwa kina ambapo imebainishwa kuwa washairi huathiriwa na mazingira yao ya kihistoria, kijiografia, kijamii, kisiasa na kiuchumi wanapowateua wahusika wao. Hii inatokana na ukweli kuwa fasihi ni zao la jamii na hivyo hueleza yale wanajamii wanayopitia katika maisha yao ya kila siku, zikiwemo tajriba za washairi. Wahusika anaowatumia mshairi ni wawakilishi wa watu halisi pamoja na hali na matukio wanayokumbana nayo katika maisha yao.

Sura ya tatu imejadili aina za wahusika wanaopatikana katika mashairi ya Kiswahili na kubainisha jinsi wahusika hao walivyohusiana au kuathiriana kiubunifu ili kuendeleza mawazo ya mshairi kikamilifu. Aina zilizojadiliwa ni wahusika binadamu, wahusika wanyama, sehemu za mwili pamoja na maumbile na vitu vingine. Imebainika kuwa aina zote za wahusika huwakilisha binadamu na tabia zao. Imebainika pia kwamba wahusika hawa wanapoungwa pamoja kiubunifu hudhihirisha matangamo kama yale ya binadamu halisi.

Sura ya nne imeshughulikia aina za hisia ambazo washairi hudhihirisha kupitia wahusika wao kwa lengo la kuwaathiri wasomaji wao kihisia. Katika sehemu hii pamejadiliwa hisia tatu kuu kama zinavyotambuliwa na wanasaikolojia. Hisia hizi ni mapenzi, hasira na hofu. Imebainika kwamba wahusika hutumiwa na washairi kutolea hisia zao binafsi na pia zile za wanajamiii wengine kuhusu hali na matukio halisi maishani. Katika baadhi ya mashairi yaliyohakikiwa imebainika kuwa wahusika wanaweza kutumika kudhihirisha mapenzi ya mtu kwa mtu mwingine au mtu kwa kitu, ikiwemo nchi yake. Wahusika wengine wanawakilisha watu waliojawa na hasira kuhusiana na hali fulani maishani kama vile ubaguzi wa

kitabaka na ndoa zinazosambaratika. Mhusika pia anaweza kudhihirisha hofu ambazo watu huwasababishia wenzao kwa kuwanyanyasa kitabaka. Pia wahusika wanaweza kutumiwa kuonyesha jinsi watu wanaweza kuhofia hali fulani maishani kama vile kuishi maisha ya kimaskini.

Katika sura ta tano kuna hitimisho la utafiti huu ambapo tunatoa muhtasari wa kila sura, matokeo ya utafiti, matatizo na mafanikio na mapendekezo ya utafiti wa baadaye wa kifasihi.

**5.3 Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu umeshughulikia kwa kina swala la usawiri wa wahusika katika mashairi ya Kiswahili. Imedhihirika wazi kwamba mshairi huathiriwa na mazingira yake ya kihistoria, kijiografia, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Hivyo, wahusika hutumiwa kudhihirisha jinsi mazingira ya mshairi yalivyo katika maisha halisi.

Imebainika kuwa mshairi ni mwanajamii na hivyo huyasawiri matukio ya kihistoria katika jamii kupitia tungo zake. Matukio haya ni yale ameyashuhudia au kuyashiriki kama mtu binafsi au akayashuhudia yakipitiwa na wanajamii wenzake. Mengine yanaweza kuwa wamepitiwa na taifa lake.

Pia imebainika kwamba matukio hayaibuki tu bali mara nyingi husababishwa na watu. Ili mshairi aweze kuyasawiri kwa njia ya kusadikika, ni sharti awatumie wahusika mahsusi. Wahusika hawa ni wawakilishi wa watu halisi waliojulikana katika kipindi maalum cha kihistoria. Wanaweza kuwa watu waliopigania maslahi ya wanajamii kama vile wapiganiaji uhuru kutoka kwa wakoloni wakongwe au wakoloni mamboleo. Imedhihirika kuwa wahusika watumiwapo kuyasawiri matukio na hali za kihistoria huacha athari kubwa zaidi katika ubongo wa msomaji kiasi cha kutosahaulika kwa urahisi.

Imethibitishwa kwamba wahusika pia husawiriwa kutokana na mazingira ya kijiografia ya mtunzi. Kutokana na weledi wa mshairi wa mahali anapoishi, mara nyingi hutokea mashairi yanayowasawiri wahusika kama vile mimea na sehemu zake kama vile maua, matawi na matunda. Hili linatokana na jinsi wanajamii wanavyoithamini mimea hii pamoja na sehemu zake au hata bidhaa zake. Mshairi anapotaka kuusifia urembo wa mtu anaweza kulitumia ua kama mhusika wake kwani urembo wa maua unatambulika na wanajamii wengi. Warembo pia huwakilishwa na ndege kama vile hua kwani ndege huyo anaaminika kwamba ni mrembo.

Miti iliyosongamana msituni kiasi cha ile mikubwa kuinyima ile midhoofu nafasi ya kunawiri itumikapo kama wahusika huwakilisha wanajamii wenye uwezo wanaowanyanyasa wasio na uwezo. Aidha, ndege na nyoka wang'an'aniao maslahi yao msituni ni ishara ya binadamu wenye ubinafsi wa hali ya juu. Mshairi 'anapowawezesha' wadudu kama vile siafu kumwua nyoka anahimiza ushirikiano miongoni mwa wanyonge wanaonyanyaswa na wenye nguvu. Hali kadhalika, mshairi anapoisawiri hali ambapo ndege wenye manufaa kwa mwanadamu wanaangamizwa na kubaki wale hatari ni ishara kuwa watu wema daima hukabiliwa na hatari ya kuangamizwa na wale wazuri na kuuacha ulimwengu uliojaa waovu.

Katika baadhi ya mashairi, uchunguzi umebainisha kwamba wanyama wa porini wanawindana na kuangamizana. Simba amwindaye paa anaweza kulinganishwa katika maisha halisi na binadamu aliyejaa hiana kiasi cha kumkandamiza au hata kumwangamiza mwenzake kwa sababu kama za kisiasa au za kiuchumi. Kuwindana huku sio tu kanuni ya porini kama anavyohitimisha Mohamed (2002) katika shairi liitwalo 'Jicho la ndani' (uk.1-2) bali pia kanuni ya ulimwengu.

Wahusika mimea pia wanaweza kutumika kudhihirisha jinsi wanajamii wanavyoithamini mimea fulani inayopatikana katika mazingira yao. Mohamed

(2002) anautumia mtango kama mhusika wake kuonyesha jinsi watu maskini wanavyouthamini mmea huu ambao kwa matajiri ni duni. Mbega (1984) amelitumia nazi kama mhusika mjinga asiyeweza kujitetea hata anapodhulumiwa.

Mkondo wa maji yanayoiangamiza mimea na chochote inachokumbana nacho ni kiwakilishi cha watu wenye uwezo mkubwa wanaowaangamiza wanyonge. Mshairi anapowatumia wahusika kama hawa huonyesha hali ya kukata tamaa kwa upande wa wanyonge.

Uhakiki umeonyesha kwamba wahusika wanaosawiriwa kwa misingi ya mazingira ya kijamii huzibainisha shughuli, matangamano na migogoro baina ya wanajamii. Wahusika kama vile wake na waume hutumika kuonyesha mahusiano kama yale ya wachumba na waliooana pamoja na mizozo inayoibuka kati yao. Mashairi yenye wahusika wa aina hii yanapatikana katika diwani mbili zilizoteuliwa.

Uchunguzi pia umepata kwamba wahusika wanaorejelea maswala ya kijamii kama vile malezi hutumiwa katika mashairi kuonyesha jinsi wazazi na walezi huyatekeleza majukumu yao vizuri au vibaya. Matangamano ya walezi, wazazi na watoto hujitokeza katika mashairi kama haya. Mohamed (2002) amefanya ulinganishi mwafaka wa maisha ya watoto wa jamii za kitajiri na zile za kimaskini na kudhihirisha kuwa watoto hawa hawazaliwi, kulelewa na kukulia katika mazingira yanayotofautiana tu bali mimba zao pia hutungwa kwa njia tofauti! Wahusika waliotumika hapa ni kama vile wazazi, wakunga, yaya, madaktari na wauguzi.

Utafiti huu umepata kwamba maovu ya kijamii kama vile wizi, wivu na kiburi pia yanaweza kujadiliwa kupitia usawiri wa wahusika wanaoyaendeleza au kuyapinga. Wahusika wanaojitokeza hapa ni kama vile wezi, watu wenye wivu na kiburi na wanajamii kwa jumla walioungwa vyema kupitia ujenzi wa migogoro iliyotokana na

maovu hayo. Baadhi ya tungo za washairi wawili zilizoshughulikiwa katika utafiti huu zimedhihirisha hili.

Tumepata kwamba mazingira ya kisiasa ni muhimu mno katika usawiri wa wahusika kwani huyasawiri matukio na hali zilizomo kwa njia ya kuaminika. Mshairi anapotaka kuzungumzia unyanyasaji wa kisiasa kupitia uongozi mbaya huwatumia wahusika kama vile viongozi dhalimu, vibaraka wao na wananchi wanaonyanyaswa. Mara nyingine huwasawiri wahusika mashujaa wanaojitolea kuikomboa jamii kutoka kwa dhuluma hizi. Migogoro ya kisiasa inayotokana na matukio na hali hizi hujengeka waziwazi kupitia mahusiano ya wahusika hawa. Mifano ya mashairi yaliyo na wahusika wa aina hii ni kama vile 'Simwabudu mtu' (uk.42) na 'Moyo unaniuliza' (uk.87-88) yaliyo katika diwani ya **Jicho la ndani** (2002).

Vilevile imebainika kwamba mazingira ya kiuchumi yanaathiri uteuzi wa wahusika kwani mshairi huwatumia wahusika hao hubainisha hali ngumu wanazopitia maskini wakilinganishwa na matajiri wanaoishi maisha ya anasa. Wahusika wanaojitokeza katika mashairi yanayojadili hali hizi ni matajiri na maskini pamoja na jamaa zao. Katika baadhi ya mashairi tumeona migogoro inayosababishwa na hali ya matajiri kuwanyanyasa maskini. Wapo pia wananchi walio katika harakati za kujichumia mali ili wasiambulie umaskini. Nadharia ya ulimbwende inatambua umuhimu wa kuwafuatilia wanajamii katika shughuli zao za kila siku ili kuweza kuwasawiri vyema kama wahusika.

Imedhihirika kwamba wahusika wa aina mbalimbali hujitokeza katika mashairi ya Kiswahili. Mashairi yaliyohakikiwa katika utafiti huu yamebainisha utumiaji wa wahusika binadamu, wahusika wanyama, sehemu za mwili pamoja na maumbile na vitu vingine. Wahusika binadamu ndio dhahiri zaidi kwani katika usawiri wake huonekana kama binadamu halisi na hivyo kuaminika kwa urahisi. Katika baadhi ya

mashairi yaliyohakikiwa katika utafiti huu, watunzi wamejisawiri kama wahusika kwa kuzungumza katika nafsi ya kwanza. Usawiri wa aina hii ni muhimu kwani msomaji hujihisi kama msemaji halisi wa maneno hayo na hivyo kupunguza masafa ujumi.

Tulitambua kwamba mtunzi anapowatumia wahusika hawa, hudhamiria kuyafafanua maisha ya binadamu halisi kwa kuonyesha jinsi watu hutangamana na wakati mwingine matatizo yakazuka miongoni mwao. Utatuzi wa matatizo haya mara nyingi hupendekezwa kupitia mazungumzo baina ya wahusika au hata maneno ya mhusika mmoja. Maswala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa hujadiliwa kupitia wahusika hawa. Ndiposa baadhi ya mashairi yana wahusika kama vile viongozi na watawaliwa, matajiri na maskini na wahusika wengine wa tabaka mbalimbali. Swala la utamaduni pia huibuka ambapo wahusika kama vile wachawi na watu wenye imani mbalimbali hujitokeza.

Uhakiki umeonyesha kwamba wahusika wanyama wanapojitokeza katika mashairi aghalabu huwa wa kijazanda, ambapo ujumbe wa shairi huwa umefumbwa. Tabia za watu hulinganishwa na zile za wanyama kwa njia kadha bila kuonyesha waziwazi kuwa si wanyama halisi wanaozungumziwa. Mshairi anaweza kuchagua kuwatumia wanyama katili kama vile simba na chui kuwakilisha watu wawawindao wenzao ili kuwaangamiza kutokana na ushindani wa kisiasa, kiuchumi au kijamii. Wanyama wadogo kama vile ndege na wadudu huwakilisha watu wa tabaka la chini. Katika baadhi ya mashairi pia tunawapata wahusika wanyama wakitangamana na binadamu. Kwa mfano, mtu anapomwangamiza ndege baada ya kumfuga kama kivutio ni ishara ya uonevu mkubwa na utovu wa shukrani.

Tulipata kwamba wakati mwingine wanyama wadogo hutumiwa kusisitiza ushirikiano miongoni mwa wanaokandamizwa ili waweze kujikomboa. Kwa mfano, siafu wanapoivamia maiti ya nyoka aliyekuwa akiwaangamiza ndege huku ndege

hao wakiruka na kushangilia ni ishara ya mwisho wa maonevu kama anavyodokeza Mohamed (2002) katika shairi liitwalo 'Juu ya mti' (uk.150-152).

Wanyama pia wanaweza kutumiwa kama wahusika kuonyesha jinsi binadamu hujaribu kuuficha ukweli ulio dhahiri kabisa. Mohamed (2002) amefanya hivi kupitia shairi liitwalo 'Punda' (uk.75) ambapo anasema kuwa huwezi kumbadilisha punda kwa vyovyote vile.

Sawa na matumizi ya wanyama kama wahusika, utafiti pia ulipata kwamba sehemu za mwili zitumikapo pia huwakilisha binadamu na tabia zake. Kiungo hutumika kama mhusika wa kimetonumia kuwakilisha mwenye kiungo hicho. Kwa mfano, mshairi atumiapo jicho, mkono au mguu kama mhusika hadhamirii kuzungumzia kiungo hicho bali binadamu mwenye sifa zinazodhihirishwa na kiungo hicho. Jicho lisiloona vyema linaweza kuwakilisha mtu mwoga ajifanyaye kutoona maovu yanayoendelea katika jamii yake ili asijitie matatani.

Utafiti pia uligundua kwamba mshairi hutumia mbinu ya tashihisi katika usawiri wa wahusika wa aina hii kwani viungo hivi hutenda mambo kama binadamu. Kwa mfano, moyo huweza kumwuliza mtu maswali, uso na mikono ikajionea huruma na chuchu likawa na uhusiano wa karibu sana na mtoto, kama ilivyobainika katika mashairi yaliyojitokeza katika diwani zilizoteuliwa.

Utafiti ulibainisha kwamba maumbile kama vile upepo, mawingu, mito na mimea pia hutumika kama wahusika. Wahusika hawa huwakilisha binadamu wenye nguvu na uwezo wa kufanya mambo sawa na baadhi ya maumbile haya. Aghalabu wahusika hawa hutumika kuonyesha jinsi watu hawa hufanya mambo ya kikatili na yenye madhara makuu kwa watu wasio na uwezo badala ya kufanya ya tija. Kwa mfano, upepo uvumapo kwa fujo husababisha madhara ilhali uvumapo taratibu hunong'oneza usalama. Mawingu yatandapo yana uwezo wa kusababisha mvua ya

heri au ya shari. Vivyo hivyo, mito inaweza kufurika na kusababisha madhara badala ya maji yake kuwafaa watu. Mimea nayo inaweza kuzua ushindani huku iliyo mirefu na minyoofu ikiidhalilisha ile midhoofu na mikondefu, sawa na wafanyavyo walimwengu.

Tulipata kuwa vifaa kama vile peku na ungo pia hutumika kuwakilisha watu walio na tofauti ya umri ili kuonyesha jinsi vijana wanaweza kuwadharau wazee bila kujali kuwa wao pia watazeeka na kupoteza ubora. Mtu pia anaweza kulinganishwa na kitu kama vile ukuni kama alivyofanya Mbega (1984) anapomwita mume ukuni wa koko. *Aidha amemlinganisha mjinga na nazi pamoja na bidhaa zake.*

Utafiti ulibainisha kuwa taifa linaweza kusawiriwa kiistiari kama nyumba kwa lengo la kuonyesha hatua kadha za kimaendeleo lilizopitia. Mohamed (2002) amelilinganisha taifa lililodumaa na nyumba ya karata ambayo huporomoka mara kwa mara na kuwatamausha waja katika shairi liitwalo 'Nyumba ya ndoto' (uk.126-129). Bila shaka taifa ni watu. Hawa ndio wanazidi kuporomoshwa na viongozi wabaya.

Utafiti huu pia umebainisha kuwa wahusika hutumiwa na washairi kutolea hisia mbalimbali. Mshairi anapoeleza sifa za wahusika kama vile umri, nyuso zao na hali wanazopitia huibua hisia fulani nyoyoni za wasomaji wake kiasi cha kuwawezesha 'kuona' , 'kusikia' na kuyahisi yanayowasibu wahusika hao. Hali hii hujitokeza hasa katika mashairi ya hisia ambayo hueleza mawazo na hisia za mshairi bila kutoa masimulizi marefu. Katika mashairi ya aina hii, kila neno linalosemwa na mhusika au kumhusu mhusika huwa na uzito mkubwa. Kwa mfano, mhusika asemapo 'moyo wangu umefumba' anaashiria huzuni au hofu kubwa aliyo nayo kuhusu jambo fulani.

Utafiti uligundua kuwa mshairi anaweza kueleza hisia nyingine kama vile mapenzi na hasira kupitia usawiri wa wahusika wanaohusiana kwa njia tofauti. Hili hujitokeza kupitia nafsi ya kwanza ambapo mshairi huzungumza na ampendaye au kupitia wahusika wengine wa kiume na kike. Imedhihirika kuwa wahusika watumikao hapa ni kama vile maua na ndege kama vilinganishi vya uzuri wa apendwaye. Pia wahusika wengine huzungumzia mapenzi kwa nchi zao.

Tulipata kwamba nadharia ya ulimbwende inatambua dhima ya ushairi katika kuelezea hisia nzito, hasa ile ya mapenzi miongoni mwa hisia nyingine kama mojawapo wa hali anazojikuta binadamu katika maisha yake ya kila siku.

Utafiti ulidhihirisha pia kuwa hasira hujitokeza pale mshairi havutiwi na hali na matukio fulani katika jamii. Wahusika kama vile wezi, viongozi wabaya na mabepari wanapotumika huwakilisha watu wenye tabia zisizompendeza mshairi. Pia hupatikana wachochole wanaokandamizwa na nduli hawa kwa lengo la kujiimarisha kijamii, kiuchumi na kisiasa. Mazingira na hali wanamopatikana wachochole hawa ni za kusikitisha, hasa walinganishwapo na wanaowanyanyasa.

Ili kuwahamasisha wanajamii juu ya umuhimu wa kujikomboa, tulipata kwamba washairi mara nyingine huwasawiri wahusika mashujaa wasiohofu chochote. Mohamed (2002) amethibitisha hili kupitia mashairi kama vile 'Simwabudu mtu' (uk.42) na 'Chukua siuzi' (uk.101) ambapo anafoka katika nafsi ya kwanza kuwa hayuko tayari kuwaabudu wadhalimu wala kuwauzia utu wake.

Utafiti huu umebainisha kuwa wahusika hawapatikani tu katika mashairi ya kimasimulizi kama ilivyodaiwa na Njogu na Chimerah (1999). King'ei na Kemoli (2001) pia wamedai kuwa wahusika hujitokeza tu katika tenzi na mashairi marefu ya kimasimulizi hasa yale ya kimapinduzi. Baadhi ya mashairi yaliyohakikiwa katika utafiti huu ni mafupi, hata kufikia ubeti mmoja na yanao wahusika muhimu.

Wahusika pia wanapatikana katika mashairi ya kiarudhi na mashairi huru yaliyojitokeza katika vitabu vilivyoshughulikiwa.

Maoni ya mtafiti ni kuwa kwa kuwa ushairi wa Kiswahili unaendelea kukumbwa na wimbi la mabadiliko, ni muhimu kufafanua vipengele na mbinu nyingine za kuuhakiki, kikiwemo kipengele cha wahusika.

### 5.3 Mafanikio na Changamoto

Lengo mojawapo la utafiti huu lilikuwa kuangazia uteuzi wa wahusika katika mashairi ya Kiswahili na kubainisha vigezo vinavyozingatiwa katika uteuzi huo. Swala la mazingira ya kiutunzi liliangaziwa kwa kina ambapo mazingira ya kisiasa ya mtunzi yalishughulikiwa. Changamoto iliyojitokeza katika sehemu hii ni kuwa mwandishi wa **Dafina ya Umalenga** (1984) alijikita zaidi katika maswala ya kijamii na kujiepusha na siasa. Kwa hivyo mifano yote inayohusiana na swala hili imetolewa katika **Jicho la Ndani** (2002). Hata hivyo hali hii haikuathiri utafiti huu kwani mifano iliyopatikana ilitosheleza malengo ya utafiti.

Mafanikio makuu yaliyofikiwa na utafiti huu ni kuwa imebainika wazi kwamba wahusika katika mashairi ya Kiswahili ni chombo muhimu cha kuelezea mawazo na hisia za mtunzi. Imebainika pia kuwa ushairi wa Kiswahili unaweza kuhakikiwa kwa kuzingatia wahusika na hivyo kuupa mwelekeo mwingine wa kiuhakiki badala ya kujikita tu katika maudhui, dhamira, umbo na msamiati. Utafiti huu pia unawapa watunzi changamoto ya kuzingatia wahusika wanapotunga bila kujali iwapo shairi linazingatia arudhi au la.

### 5.4 Mapendekezo

Kwa kuwa utafiti huu umeshughulikia usawiri wa wahusika katika mashairi ya Kiswahili, utafiti wa baadaye unaweza kulinganisha na kulinganua usawiri wa



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

wahusika katika mashairi ya Kiswahili na ule wa wahusika katika maandishi ya nathari kama vile riwaya, hadithi fupi au tamthilia.

Pia utafiti huu ulizingatia usawiri wa wahusika katika mashairi yaliyotungwa na watunzi wa kiume tu. Utafiti wa baadaye unaweza kuchunguza jinsi watunzi wa kike huwasawiri wahusika wao, hasa kwa mtazamo wa kijinsia. Watafiti pia wanaweza kulinganisha jinsi washairi wa kike na wale wa kiume walivyowasawiri wahusika wao.

Utafiti wa baadaye unaweza pia kulinganisha na kulinganua wahusika kwa mujibu wa nyakati za utunzi, mazingira ya utunzi, maswala yaliyoshughulikiwa, lugha ya wahusika na kuathiriana kwao.

## MAREJELEO


Abdalla, A (1973) "Ushairi wa Kiswahili: Na Uhuishwe, Usiuliwe." Makala, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Babusa, H.O (2005) "Vigezo Badalia Kuhusu Uainishaji wa Mashairi ya Kiswahili." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Collier, C (1966) **Collier's Encyclopedia.** USA: Macmillan Inc.

EMC Corporation (1996) **Literature and the Language Arts.** Minesota: EMC/ Paradigm Publishing.

Foakes, R.A (1968) **Romantic Criticism.** London: Edward Arnold.

Hill, J.S (1977) **The Romantic Imagination.** London: Macmillan Press Ltd.

Jordan, J.E (1976) **Why the Lyrical Ballads?** Berkeley: University of California Press.

Kezilahabi, E (1974) **Kichomi.** Nairobi: Heinemann.

___________(1976) **Ushairi wa Shaaban Robert.** Nairobi: KLB.

King'ei, K (1999) **Miale ya Uzalendo**, Nairobi: Phoenix Publishers.

King'ei, K na Kemoli, A (2001) **Taaluma ya Ushairi**. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Masinde, E (1992) "Mashairi: Uchambuzi wa Dhamira na Mtindo." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Mazrui, A.M na Syambo, B.K (1992) **Uchambuzi wa Fasihi**. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbega, H.M (1984) **Dafina ya Umalenga.** Nairobi: Longman Kenya.

Microsoft, (2004) **Encarta Encyclopedia.** USA: Microsoft Corporation.

Mohamed, S.A (2002) **Jicho la Ndani**. Nairobi: Longhorn Publishers.

Momanyi, C (1998) "Usawiri wa Mwanamke Mwislamu katika jamii ya Waswahili kama inavyobainika katika Ushairi wa Kiswahili." Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Msokile, M (1993) **Misingi ya Uhakiki wa Fasihi.** Nairobi: East African Educational Publishers.

Ndungo, C.M (1985) "Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Njogu, K na Chimerah, R (1999) **Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu**. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K (1996) "Kiswahili Metapoetry on Prosody", Makala ya Semina, Chuo Kikuu cha Nairobi

_________(2004) **Reading Poetry as Dialogue**. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ombuge, R na Kisia, A (1999) **Uchambuzi wa Mashairi.** Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Ruo, K.R (1989) **Nguzo Za Ushairi Wa Kiswahili.** Nairobi: Macmillan.

Senkoro, F.E.M (1988) **Ushairi: Nadharia na Tahakiki.** Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

TUKI (2004) **Kamusi ya Kiswahili Sanifu.** Nairobi: Oxford.

United Bible Societies (1952) **Biblia Takatifu.** Nairobi: United Bible Societies.

Wafula, R.M (1992) "Nadharia kama Mwongozo wa Utunzi na Uhakiki", Makala ya semina, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Wamitila, K.W (2003) **Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia**. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wordsworth, W (1798) **Lyrical Ballads with A Few Other Poems.** London: Bristol.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY